

MATUMIZI YA TAMATHALI ZA USEMI TEULE KATIKA *UTENZI WA QIYAMA*.

NA

ALOO RONALD ODHIAMBO

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA

SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

OKTOBA 2018

UNGAMO

TASNIFU HII NI KAZI YANGU BINAFSI NA HAIJATOLEWA KWA MAHITAJI YA
SHAHADA KATIKA CHUO KIKUU KINGINE.

SAHIHI

TAREHE

ALOO RONALD ODHIAMBO

(MTAHINIWA)

TASNIFU HII IMETOLEWA KUTAHINIWA KWA IDHINI YETU KAMA
WASIMAMIZI WALIOTEULIWA NA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

SAHIHI

TAREHE

PROF. KINEENE WA MUTISO

SAHIHI

TAREHE

DKT. BASILIO G. MUNGANIA

TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabarukia kwanza kabisa baba yangu mpendwa Gerphas Aloo, kwa kunisaidia kwa hali na mali wakati nilipokuwa ninasoma. Pia mama yangu Grace Mboya, kwa kunipa moyo wa kuendelea na kazi yangu ya utafiti pamoja na kunipa utulivu wa moyo na akili. Pia mke wangu na watoto wangu wpendwa Betty, Diddy na Tj kwa kunivumilia sana nikiwa masomoni. Hata hivyo, sitawasahau kuwashukuru ndugu zangu Benedict na Tyson kwa kunisaidia kwa njia moja au nyingine katika masomo yangu. Aidha, shukrani kwa dhati na mtolea mjomba Toby kwa kunipa malazi na mahitaji mengine katika masomo yangu Mungu ambariki.

SHUKRANI

Kwa kweli kazi hii imekuwa na changamoto nyingi sana, lakini kwa usaidizi wa watu mbalimbali niliweza kukamilisha. Kwanza, ningependa kumshukuru muumba wangu Mungu aishiye milele, kwa kunipa siha akili timamu, pamoja na hekima, ili kufanikisha malengo yangu ya kiusomi. Ni kupitia kwa nguvu na uwezo wake, ambapo niliweza kuitimiza ndoto yangu, ya kupata shahada ya uzamili, katika somo la Kiswahili.

Shukrani zingine nazitolea wasimamizi wangu; Prof. Kineene wa Mutiso na Dkt. Basilio, G. Mungania kwa kunielekeza, hatua kwa hatua, kunikosoa na kunirekebisha kazi yangu pamoja na kunivumilia. Ni kupitia kwa juhudi zao ambapo kazi yangu iliweza kukamilika. Shukrani za kipekee pia zimwendee Prof. Kineene kwa kunipatia *Utenzi wa Qiyama*, kama si yeye nisingeupata.

Shukrani zingine ziwaendee wahadhiri wangu wapenzi walionifunza. Prof. John Habwe, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Iribe Mwangi, Prof. K.W Wamitila, Prof. Mwenda Mbatia, Prof. Rayya Timmamy, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Jerono, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Zaja Omboga na Bw. Sanja Leo. Vilevile wahadhiri wote wa Chuo Kikuu cha Nairobi ambao wengi pia walinifunza na kunisaidia kwa njia moja au nyingine. Mungu awabariki nyote na wape hekima na siku nyingi ili msaidie wengine kama mimi.

Ninawashukuru pia wasomi wenzangu tulioshirikiana na kushauriana pamoja na kuhimizana na kuchukuliana mizigo kama vile Barasa, Cyrus, Otuoma, Mariga, Faith, Irine Kanana, Irine Kilingo, Elizabeth, Gichuki, Barnice, Grace, Naomi, Gloria, Jose, Mulati na Migiro Josphat. Asanteni kwa ushirikiano wenu. Ninawashukuru walimu wafuatao wa shule ya Gititu; Bi.

Naomi Mbithe, Bi Agneta Kisingu, Bi Muinde, Bw Peter Muturi, Bw Onesmus Kamau na Bi. Ng'ang'a kwa kunipatia moyo na motisha ya kufanya kukamilisha masomo yangu.

Sitasahau kumshukuru Chrispine Adede kwa kujitolea kunipigia chapa kazi zangu zote za kusoma pamoja na kupanga na kurekebisha makosa yaliyojitokeza. Barikiwa sana. Kwenu nyote ambao sikuwataja kwa majina na ambao mlinifaa kwa njia moja au nyingine, ninawashukuru sana na Mungu awamiminie baraka zisizo na kikomo.

IKISIRI

Katika utafiti huu, tumeshughulikia matumizi ya takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha katika *Utenzi wa Qiyama*. Utenzi huu ni miongoni mwa tenzi ndefu za kidini na za jadi za Kiswahili. *Utenzi wa Qiyama* una beti 338 na unahusu tukio la hukumu baina ya waumini (Waislamu) na Makafiri (Wakristo) utakaofanywa na Mwenye Enzi Mungu na malaika wake siku ya mwisho. *Utenzi wa Qiyama* ulihaririwa katika miaka ya 1972 kwa mujibu wa dibaji ya mhariri, hata hivyo mtunzi wa utenzi huu hajulikani. Katika utafiti wetu, tumechunguza *Utenzi wa Qiyama*, kwa kutumia uhakiki wa kimtindo. Nadharia hii imetuwezesha kuchunguza kipengele cha tamathali za usemi hasa takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha na tumebainisha kuwa tamathali hizi zimechangia katika kujenga taswira ya Siku ya Kiyama. Katika utafiti wetu, tumenuia kuonyesha kuwa *Utenzi wa Qiyama* una matumizi mengi sana ya takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha na kuwa tamathali hizi tano ndizo kiini cha taswira ya Siku ya Kiyama katika *Utenzi wa Qiyama*. Utafiti wetu umekuwa wa maktabani. Tumesoma mashairi na tenzi nyingi za kale kwa vile tenzi hizi ndizo zinawekea msingi ushairi wa Kiswahili. Aidha, tumesoma majarida, makala ya mtandao na vitabu vinavyoeleza dhana za takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha. Tumesoma *Utenzi wa Qiyama* ili kuelewa matumizi ya lugha ya utenzi huu. Tumedondoa beti zote ambazo zimetumia mbinu za takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha. Tumeanza kuhakiki utenzi huu bila kujua athari itakayotokana na takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha katika *Utenzi wa Qiyama*. Kisha, tumesoma *Utenzi wa Qiyama* na kubainisha vile takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha zinavyochangia kwa kukua na kuendelea kwa athari fulani. Tumetumia maelezo na ufafanuzi wa dhana mbalimbali katika kueleza mchango wa takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha katika ujenzi wa taswira ya Siku ya Kiyama. Matokeo ya utafiti wetu ni kuwa mtunzi ametumia takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha kwa njia ya kufana na kufikia dhamira yake ya kujenga picha ya Siku ya Kiyama. Aidha, kwa kutumia tamathali hizi za usemi, mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* amefaulu kufikisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa huku akitujengea picha halisi ya Siku ya Kiyama kwa kubana ujumbe huo kwa wasiolengwa, kufikia umbuji wa shairi, kuleta tasfida, kujenga mshikamano wa kirejelezi, kuleta mshikamano wa kimtindo, kuleta ucheshi, kuongezea ladha ujumbe kuhusu Siku ya Kiyama, kufafanua na kueleza hisia zake, kuumba utenzi pamoja na kuboresha kazi yake. Kazi hii imefanikisha uelewa wa tamathali hizi na utenzi huu pakubwa.

YALIYOMO

UNGAMO	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI.....	vi
YALIYOMO.....	vii
SURA YA KWANZA.....	1
1.0 Utangulizi.....	1
1.2 Tatizo la Utafiti.....	1
1.3 Malengo ya Utafiti.....	2
1.4 Sababu ya Kuchagua Mada Hii	3
1.5 Upeo na Mipaka.....	3
1.6 Maswali ya Utafiti	4
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada	4
1.8 Msingi wa Kinadharia.....	7
1.8.1 Viwango Katika Uchunguzi wa Nadharia ya Umtindo.....	10
1.8.2 Ukiushi wa Msamiati au Kileksia	10
1.8.3 Ukiushi wa Kisarufi.....	11
1.8.4 Ukiushi wa Kifonolojia	11

1.8.5 Ukiushi wa Kimaandishi au Grafolojia	11
1.8.6 Ukiushi wa Kisemantiki	12
1.8.7 Ukiushi wa Kilahaja	12
1.8.8 Ukiushi wa Sajili au Rejista.....	13
1.8.9 Ukiushi wa Kihistoria au Kimapishi	13
1.8.9.1 Lugha ya Kitamathali na Mtindo	14
1.8.9.2 Uteuzi na Mtindo	15
1.8.9.3 Sarufi na Mtindo	16
1.8.9.4 Usimulizi na Mtindo	17
1.8.9.5 Uchimuzi na Mtindo	18
1.8.9.6 Mtazamo, Itikadi na Mtindo	18
1.8.9.7 Muwala, Mshikamano na Mtindo.....	19
1.8.9.8 Mazungumzo na Mbinu za Kuwasilisha Mawazo.....	19
1.9 Mihimili ya Kinadharia ya Umtindo.....	20
1.10Ufaau wa Nadharia ya Umtindo	21
1.11 Njia za Utafiti	22
1.11.1 Mbinu za Ukusanyaji Data	22
1.11.2 Mbinu za Kuchanganua na Kuwasilisha Data	23
1.12 Hitimisho.....	23

SURA YA PILI.....	25
2.0 UFAFANUZI WA DHANA YA TAKRIRI, TASWIRA, TASHBIHI, TASHIHISI, SITIARI NA MASWALI YA BALAGHA	25
2.1 Utangulizi.....	25
2.2 Tamathali za Usemi na Mbinu Nyinginezo za Lugha	25
2.3 Takriri	26
2.3.1 Aina za Takriri	27
2.3.2 Takriri Irabu au Vokali.....	27
2.3.3 Takriri Konsonanti	28
2.3.4 Takriri Neno au Maneno.....	28
2.3.5 Takriri Silabi	28
2.4 Dhana ya Taswira.....	29
2.4.1 Aina ya Taswira	30
2.4.2 Taswira za Kuona.....	31
2.4.3 Taswira za Mnuso au Harufu.....	31
2.4.4 Taswira za Mguso	31
2.4.5 Taswira za Mwonjo.....	32
2.4.6 Taswira za Usikivu.....	32
2.4.7 Taswira za Mwendo	32
2.4.8 Taswira za Joto.....	33

2.5 Tashibihi.....	33
2.5.1 Aina ya Tashibihi	34
2.5.2 Tashibihi Fiche.....	34
2.5.3 Tashibihi Wazi	35
2.5.4 Tashibihi ya Kiutendi	35
2.6 Mbinu ya Tashihisi	36
2.7 Sitiari.....	37
2.7.1 Aina za Sitiari.....	38
2.7.2 Sitiari Chakavu.....	39
2.7.3 Sitiari Dhana	39
2.7.4 Sitiari Radidifu.....	40
2.7.5 Sitiari Mseto.....	40
2.7.6 Sitiari Sahili	41
2.7.7 Sitiari Changamano	41
2.7.8 Sitiari Kuu.....	42
2.7.9 Sitiari ya Kikaida.....	42
2.7.10 Sitiari Hisi Mseto	43
2.7.11 Sitiari ya Usuli.....	43
2.8 Dhana ya Maswali ya Balagha	43

2.9 Hitimisho.....	44
SURA YA TATU	46
3.0 MATUMIZI YA TAKRIRI, TASHBIHI, TASHIHISI, SITIARI NA MASWALI YA BALAGHA KATIKA <i>UTENZI WA QIYAMA</i>	46
3.1 Utangulizi.....	46
3.2 Takriri	46
3.2.0 Aina za Takriri	47
3.2.1 Takriri Irabu.....	47
3.2.2 Takriri Konsonanti	51
3.2.3 Takriri Neno.....	53
3.2.4 Takriri Silabi	56
3.3 Tashbihi.....	60
3.3.1 Tashbihi za Wakati.....	61
3.3.2 Tashbihi za Moto.....	61
3.3.3 Tashbihi za Mimea na Wingu	62
3.3.4 Tashbihi za Mwangaza	63
3.3.4.1 Taa.....	63
3.3.4.2 Badiri.....	64
3.3.5 Tashbihi za Nywele za Wanyama na ndege	64
3.3.6 Tashbihi za Umeme.....	65

3.3.7 Tashbihi za Wanyama	66
3.3.8 Tashbihi za Hali	66
3.3.8.1 Dhaifu.....	67
3.3.8.2 Yusufu.....	68
3.4 Tashihisi	69
3.4.1 Tashihisi za Upepo	69
3.4.2 Tashihisi za Nchi.....	70
3.4.3 Tashihisi za Kaburi.....	72
3.4.4 Tashihisi za Wanyama.....	73
3.4.5 Tashihisi za Njia.....	74
3.4.6 Tashihisi za Moto	75
3.5 SITIARI	77
3.5.1 Sitiari za Vitu vya Kimaumbile au Kiasili.....	78
3.5.2 Sitiari za Wanyama	80
3.5.3 Sitiari za Vifaa	80
3.5.4 Sitiari za Hali	81
3.6 MASWALI YA BALAGHA.....	84
3.7 Hitimisho.....	93
SURA YA NNE.....	95

4.0 UMUHIMU WA TAKRIRI, TASHBIHI, TASHIHISI, SITIARI NA MASWALI YA BALAGHA KATIKA UJENZI WA TASWIRA INAYOWASILISHA SIKU YA KIYAMA	95
4.1 Utangulizi.....	95
4.2 Umuhimu na Ujenzi wa Taswira.....	95
4.3 Tashbihi na Sitiari.....	96
4.4 Takriri	100
4.5 Tashihisi	101
4.6 Maswali ya Balagha.....	102
SURA YA TANO	106
5.0 Hitimisho na Mapendekezo.....	106
5.1 Utangulizi.....	106
5.2 Hitimisho.....	106
5.3 Malengo ya Utafiti.....	107
5.4 Mapendekezo.....	108
Marejeleo.....	110

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi

Tamathali za usemi ni ufundi ambao unatumwa na msanii ili kufanikisha ujumbe kwa wasomaji. Kipengele hiki humwezesha msanii kuwasilisha ujumbe wake kwa wasomaji wanaolengwa kwa njia inayowanata, kwa njia iliyodhabiti na pia huwezesha kazi ya msanii kuwa na urembo fulani unaowafanya kutochoka wakati ambapo wanasoma kazi ya msanii. Matumizi mazuri ya tamathali za usemi katika kazi ya kifasihi huifanya kazi hiyo kuwavutia watu. Kipengele cha tamathali za usemi humwezesha msanii kupitisha ujumbe wake kwa njia ya mkato na vilevile hufanikisha ujenzi wa taswira.

Katika utafiti wetu, tumechunguza matumizi ya takriri, tashibih, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha katika *Utenzi wa Qiyama*. *Utenzi wa Qiyama* ni miongoni mwa tenzi ndefu na za jadi za Kiswahili. Utenzi huu una asili ya Kiarabu na ulitumiwa kuwafundisha Waislamu kuhusu siku ya mwisho. Utenzi huu wenye beti 338 unahusu tukio la hukumu baina ya waumini na Makafiri kati ya Wakristo na Waislamu itakayofanywa na Mwenye Enzi Mungu Siku ya mwisho. Katika utafiti wetu, tumeshughulikia tamathali hizi tano za usemi kama vipengele vinavyochangia ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama.

1.2 Tatizo la Utafiti

Takriri, tashibih, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha zina mchango mkubwa katika kurembesha kazi na kuifanya ivutie. Kumekuwa na mjadala mkubwa kati ya wataalamu mbalimbali iwapo tamathali hizi za kurembesha na kuifanya kazi ivutie zina mchango katika kujenga taswira inayowasilisha ujumbe. Wanjiru (2014) anasisitiza kuwa kazi ile ambayo haijatumia tamathali za usemi vizuri huchosha kwa kukosa kuvutia. Vivyo hivyo, Wamitila

(2003) naye anatoa kauli yake kuwa, katika ushairi, maana huwasilishwa na mtindo wa kitamathali wala sio ule wa moja kwa moja. Kutokana na mawazo ya wataalamu hawa, utafiti wetu hivyo basi umelenga kutathmini namna tamathali hizi huifanya kazi kuvutia na kujenga taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama. Je, mwandishi anapoiandika kazi yake, mbinu anazoteua huja bila kushawishiwa na mazingira alimo au hujitokeza tu? Je, kila wakati anapozitumia analenga au ananua kuiafikia malengo yepi? Je, kuna tofauti kati ya ujumbe unaowasilishwa wakati ambapo mbinu iliyotumiwa ilikuwa imeteuliwa bila kushawishiwa na mazingira alimo au zilizitokeza tu?

Hata ingawa wataalamu kama Wanjiru (2014), Maundu (2013) na Lugwiri (2011) wameshughulikia tamathali za usemi, kazi hii ni tofauti na yao kwa vile walishughulikia tamathali za usemi chache lakini sisi tumeshughulikia tamathali za usemi tano ambazo zimechangia ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika *Utenzi wa Qiyama* ambao ni tofauti na tenzi walizozishughulikia. Aidha, tumejaribu kubainisha lengo la mtunzi anapotumia tamathali za usemi na kiini cha matumizi ya tamathali hizi tano katika *utenzi wa Qiyama*.

1.3 Malengo ya Utafiti

Malengo ya utafiti wetu ni;

1. Kuchanganua takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha katika *Utenzi wa Qiyama*.
2. Kutathmini jinsi takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha zinachangia ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika *Utenzi wa Qiyama*.

1.4 Sababu ya Kuchagua Mada Hii

Uhakiki wa takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha katika *Utenzi wa Qiyama* umeleta uelewe zaidi wa utenzi huu. Lugha ya utenzi huu na tenzi nyinginezo za Kiswahili za zamani ni chakavu, hivyo hazieleweki na wengi. Aidha, kuna mchanganyiko wa maneno ya Kiarabu na lahaja za Kisiu na Kiamu. Hili huenda likafanya ujumbe wa tenzi kutoeleweka kwa uraisi na kufanya wasomaji wengi kuepuka tenzi hizi. Uhakiki wa takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha umerahisisha uelewekaji wake. Kwa mujibu ya Wa Mutiso (1996:7) wataalamu wameziepuka tenzi hizi kwa sababu ya matumizi ya kilahaja na maneno ya Kiarabu.

Utenzi wa Qiyama ni miongoni mwa tenzi za kale ambazo zimewekea ushairi wa Kiswahili msingi wake na ambao haujawahi kufanyiwa utafiti wowote wa kiusomi katika kipengele cha tamathali za usemi, hasa takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha kwa kutumia uhakiki wa kimtindo.

Tumegundua kuwa, kuna mengi kuhusu matumizi ya takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha yanayodhihirisha ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama. Jambo hili linatokana na kuwepo kwa wingi wa takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha katika *Utenzi wa Qiyama*. Kuwepo kwa wingi wa tamathali hizi tano zinafanya tuakisia kwamba matumizi ya lugha kwa wingi hufanikisha ujenzi wa taswira inayowasilisha ujumbe na vilevile hudhihirisha utunzi wa hali ya juu.

1.5 Upeo na Mipaka

Tumechunguza kipengele cha lugha au tamathali za usemi katika *Utenzi wa Qiyama*. Kwa vile mshairi ametumia tamathali nyingi za usemi ili kujenga taswira inayofafanua na

kueleza Siku ya Kiyama, tumechunguza semi tano ambazo ni; takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha ili kutathmini jinsi tamathili hizi zinachangia ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika utenzi huu. Tumeshughulikia tamathali hizi tano kuanzia ubeti wa kwanza hadi ubeti wa mwisho wa *Utenzi wa Qiyama*.

Katika utafiti wetu, tumeongozwa na nadharia ya Umtindo. Tumehakiki *Utenzi wa Qiyama* na kuchunguza namna takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha zinavyotumika ili kujenga taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika *Utenzi wa Qiyama*. Aidha, tumeshughulikia uamili wa kiumbuji wa takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha na vile tamathali hizi tano zinavyochangia ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika utenzi mzima.

1.6 Maswali ya Utafiti

Utafiti wetu umeongozwa na maswali mawili kuu:

1. Je, takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha zimetumiwa kwa wingi katika *Utenzi wa Qiyama* ili kuonyesha umbuji wa hali ya juu?
2. Je, takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha zina mchango gani katika kujenga taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika *Utenzi wa Qiyama*?

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Mengi yameandikwa kuhusu vipengele mbalimbali vya tamathali za usemi katika tenzi mbalimbali. Hata hivyo, machache yameandikwa na kushughulikiwa kuhusu *Utenzi wa Qiyama* haswa katika kipengele cha tamathali za usemi.

Allen (1972) alikusanya na kutafsiri kwa Kiingereza mashairi sita za zamani na kuandika machache kuyahusu. Mashairi haya ni pamoja na *Utenzi wa Mwana Kupona*, *Utenzi wa Ngamia na Paa*, *Utenzi wa Masahibu*, *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*, *Utenzi wa Ayub* na *Utenzi wa Qiyama*. Aidha, alizungumzia chanzo na itikadi za mashairi ya kale. Kazi ya Allen ni tofauti na kazi yetu kwa vile sisi tumeshughulikia matumizi ya takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha katika *Utenzi wa Qiyama*. Hata hivyo, ni kutokana na tafsiri yake ya *Utenzi wa Qiyama* ndiyo imetusaidia kuelewa zaidi baadhi ya maneno katika utenzi huu. Aidha, utangulizi wake umetuwezesha kufahamu itikadi za waswahili katika enzi za kale jambo ambalo limetuwezesha kuelewa kwa ukamilifu zaidi utenzi wenyewe.

Kuhenga (1977) aliibuka na vigezo sita vya kubainisha tamathali za usemi ambavyo ni pamoja na vigezo vya semi za mlinganisho wa hulka, semi za zinduna, semi za msisitizo, semi za kilinge, semi za mlinganisho wa mwigo na vitumbuizo vya maneno. Inaaminika kuwa uainishaji wake ni wa wazi zaidi. Kuhenga katika uainishaji wake hakuweza kuitolea ufafanuzi dhana ya tamathali za usemi. Kazi yake imetuwezesha kuelewa tamathali za usemi kwa undani na kwa uwazi zaidi. Kazi yake ni tofauti na yetu kwa kuwa sisi tumejikita kwa tamathali tano pekee katika *Utenzi wa Qiyama*.

Wamitila (2003) anatoa kauli yake kuwa katika ushairi, maana huwasilishwa na mitindo ya kitamathali wala sio ule wa moja kwa moja. Vilevile, katika kitabu chake cha (2008) anaelezea haja ya kuweka pamoja tamathali na rasamu. Wamitila aliainisha tamathali na rasamu na kuibuka na makundi manne makuu. Kwanza tamathali au rasamu za maneno, pili tamathali au rasamu za sentensi, tatu tamathali au rasamu za kisauti na nne tamathali au rasamu za tafrika. Hatua ya mtaalamu huyu kujumlisha tamathali na rasamu inalingana na

mawazo ya wataalamu na wahakiki wa fasihi wa Kimagharibi na wala si ukiushi tu bali ni njia inayomwezesha kuleta mtindo wa kiuandishi na kuipa lugha urembo wake. Aidha, Abrahams (1981) ambaye ni mhakiki wa Kimagharibi anasema kuwa hakuna mpaka mkubwa uliopo baina ya kategoria za rasamu na tamathali, hivyo basi, wahakiki wengi hawakubaliani nao. Wamitila anatetea hoja yake kwamba tamathali na rasamu huleta mtindo wa uandishi kwa kusema kuwa huwa tamathali zinatumiwa katika mazungumzo ya kila siku ili kuleta hali ya ukawaida wa lugha katika kiwango kingine. Aidha, tamathali hizi huleta maana mbalimbali zinapotumika katika ushairi. Kazi yake imetunufaisha kwa kufahamu rasamu za tamathali za usemi na makundi yake. kazi hii ni tofauti na yetu kwa vile sisi tumejikita kwa utenzi maalumu na tumehakiki tamathali tano pekee.

Kofa (2009) naye ameangazia uhakiki wa fani katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*. Katika utafiti wake, ameshughulikia lugha au tamathali za usemi kama mojawapo wa kipengele cha fani. Kazi yake ni ya manufaa kwetu kwa vile imetuwezesha kuelewa maana ya tamathali mbali mbali, hata hivyo, kazi yake ni tofauti na yetu kwa vile ametaja tu kijuujuu tamathali mbalimbali bila kuelezea uamilifu wake tofauti na sisi ambao tumetoa uamilifu wa kila tamathali ambao tumejadili katika utafiti wetu. Aidha, ametumia nadharia ya umuundo.

Lugwiri (2011) ameshughulikia tamathali za usemi tatu ambazo ni; sitiari, taashira na tashibiha katika uwasilishaji wa dhamira katika *Utenzi wa Tambuko*. Utafiti wetu ni tofauti kwa sababu tumechunguza aina nyingi zaidi za tamathali za usemi katika ufanikishaji wa taswira katika *Utenzi wa Qiyama*.

Maundu (2013) naye ameshughulikia matumizi ya takriri na sitiari ili kufanikisha fani katika *Utenzi wa Rasi'LGhuli*. Kazi yake ni tofauti na yetu kwa vile ametumia nadharia ya umuundo huku tumetumia uhakiki wa kimtindo. Hata hivyo, kazi yake ni ya manufaa kwetu

kwa vile imetuwezesha kufahamu aina mbalimbali za sitiari ambazo zimetuelekeza katika uchunguzi wa kazi yetu.

Wanjiru (2014) aidha, ameshughulikia matumizi ya istiari, tashbiha na taashira katika *Diwani ya Sauti ya Dhiki*. Ameshughulikia tamathali tatu katika kazi yake. Kazi yake imejikita katika mashairi ya kisasa tofauti na kazi yetu ambayo imeangazia utenzi wa kale wa Kiswahili. Hata hivyo kazi yake ni ya manufaa makubwa kwetu.

Kazi hizi zote ni tofauti na utafiti wetu kwa sababu hazijashughulikia matumizi ya tamathali za usemi katika ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama. Aidha, wahakiki wa kazi hizi hawajahakiki tamathali zote tano tutakazohakiki katika kazi yetu. Kazi hizi hazijaangazia uhakiki wa matumizi ya takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha katika kujenga taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika *Utenzi wa Qiyama*.

1.8 Msingi wa Kinadharia

Nadharia ambayo tumetumia katika utafiti huu ni uhakiki wa mitindo. Nadharia hii imetusaidia katika kuchanganua tamathali za usemi katika kufanikisha kazi ya mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama*. Kwa mujibu wa Buffon (1930) mtindo ni mtu mwenyewe. Mtindo ni vile mtu anavyotumia lugha katika uwasilishaji wake wa ujumbe.

Nadharia ya Umtindo iliasisiwa na Geoffry Leech (1969). Leech alipokuwa akiandika tasnifu yake ya uzamili aliandika makala mbili katika mwaka wa 1965 na 1966 kutokana na mapenzi yake kwa lugha ya Fasihi. Kwa sababu ya kazi hizi, isimu ya kisasa ilihusishwa na usomaji au ufundishaji wa lugha ya fasihi. Mawazo haya ya Leech yalileta ugomvi na utata baina ya wanaisimu na wasomi wa fasihi. Kwa sababu ya ugomvi huu, Leech alichapisha kitabu cha, *A Linguistic Guide to English Poetry* (1969), kwenye kitabu hiki alijadili dhana ya mtindo

kwa kuhakiki kazi za fasihi ili kutatua ugomvi huo uliokwepo baina ya wanaisimu na wanafasihi walioshikilia kuwa uhakiki wa kifasihi na uhakiki wa kazi za kiisimu hutofautiana na kuwa hazina uhusiano hata kidogo. Aidha, Leech alipata motisha wa kuandika kutoka kwa kazi ya Nowotny (1962)

Leech (1969:2) anasema kuwa Umtindo inahusu kuchanganua na kufasiri kazi kwa mkabala wa kiisimu. Mtindo kama taaluma inahusu uchanganuzi wa kiisimu na kifasihi kwa sababu uhakiki wa kifasihi hauwezi kujisimamia kivyake. Misamiati ambayo uhakikiwa katika fasihi kama vile sitiari, taswira, kinyume, kinaya au kejeli, usambamba na jazanda ni vigumu sana kufafanua pasipo na kurejelea dhana za kiisimu. Kimsingi, uwanja wa Umtindo hufanikisha uhakiki wa masuala ya kiisimu na kifasihi.

Leech anadai kuwa malengo ya stadi za elimumtindo ni fasihi na maumbo mengine ya matini ambazo ziliandikwa katika taaluma za matangazo ya kibiashara, utamaduni, siasa ama dini. Aidha, umtindo hubainisha kanuni za kuelezea uteuzi maalum ambao unafanywa na watu wanapotumia lugha kutekeleza shughuli za kijamii, utoaji na upokeaji wa maana, uhakiki wa kidiskosi na wa kifasihi.

Leech alitoa sifa zaidi za Umtindo. Kwanza alisema kuwa umtindo huhusisha matumizi ya dayolojia au mazungumzo ambayo yanahusisha lafudhi za kimaeneo na lahaja zinazotumiwa na wazungumzaji, lugha elezi na sarufi k.v sauti, urefu wa sentensi na sajili. Kwamba dhana ya “Elimumtindo” huweza kutumiwa kubainisha uhusiano uliopo kati ya umbo na athari zake katika viwango mbalimbali vya lugha.

Aidha, Leech anasema yafuatayo kuhusu lugha na fasihi. Kwamba, kwa kiwango kikubwa mtindo ndio huleta athari kwa matini. Mtindo unahusu namna na vile lugha hutumiwa na

haujabanwa katika fasihi pekee, bali ni sehemu ya usemi wowote, kwa vile msemaji ana uhuru wa kuchagua namna ya kuzungumza katika muktadha wake.

Kwa kifupi, Umtindo hurejelea uhakiki wa kazi za fasihi kwa kushughulikia mtindo kisayansi na hufuata utaratibu za kitaaluma. Hivyo basi, mtindo unaweza kufafanuliwa kama nadharia iliyo katikati ya fasihi na isimu. Umtindo huchukua mwelekeo wa kifani na unachunguza mtindo wa kile ambacho kinasemwa au maudhui na namna ambacho kinasemwa au fani.

Nadharia hii imeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali kama vile Wamitila (2003:39) na anasema yafuatayo huku akimuunga Leech mkono. Umtindo ni nadharia inayoweza kutumiwa kuhakiki kazi za kifasihi na zile za kiisimu. Wamitila anatoa kauli kuwa Umtindo hurejelea taaluma ambayo inachunguza lugha. Aidha, inachunguza vile matukio tofautitofauti yanaelezwa katika kazi za fasihi. Umtindo kama taaluma inachunguza lugha na fasihi kwa vile iko kati ya taaluma hizi mbili. Tunaweza kusema kuwa Umtindo inatumiwa kuchunguza vile lugha inatumiwa na wasanii katika kazi za fasihi na kiisimu. Elimumtindo wakati mwingine unashughulika na sifa za kimtindo zinazopatikana katika kazi ya mwandishi na ambazo hutambulisha msanii huyo.

Vilevile, Wamitila anasema kuwa nadharia ya Umtindo huwezesha uchunguzi wa vipengele vya maudhui na fani kwa kumruhusu mhakiki kuchunguza vile lugha imetumiwa katika matini za kifasihi.

Aidha, Crystal na Davy (1969:10) wanachangia nadharia ya Umtindo kwa kusema yafuatayo:

Nadharia hii inachunguza lugha ili kubainisha sifa zake mahususi zinazopatikana katika muktadha maalum kutoka katika sifa za kiisimu ambazo ni za kijumla. Sifa hizi huwa zinapatikana katika muktadha wa matumizi ya lugha. (TY)

1.8.1 Viwango Katika Uchunguzi wa Nadharia ya Umtindo

Leech (1969:42) anadai kuwa nadharia ya Umtindo ina viwango vya uchanganuzi vinavyostahili kuzingatiwa na mhakiki wa matini ya fasihi ili aweze kuhakiki kazi yake kwa njia inayostahili. Leech anataja aina zifuatazo za ukiushi wa kanuni za kutumia lugha zinazotokea katika mtindo mbalimbali wa matini za fasihi. Navyo ni: Ukiushi wa kileksika, ukiushi wa umbo, ukiushi wa kilahaja, ukiushi wa rejista, ukiushi wa matamshi, ukiushi wa grafologia, ukiushi wa kiwakati na ukiushi wa maana.

1.8.2 Ukiushi wa Msamiati au Kileksia

Kwa mujibu wa Leech (1969) ni uundaji wa maneno mapya. Katika ukiushi wa aina hii, mtunzi wa shairi au msanii anaweza akatumia maneno mengi zaidi yanayopatikana katika lugha yake kwa vile mshairi ana idhini ya kufanya hivyo. Wachapishaji, waandishi wa habari na wanasayansi ni baadhi ya waatalamu wanaounda maneno kileksia. Wananchi wa kawaida maranyingi wanajihusisha na uundaji wa maneno mapya kama njia mwafaka ya kueleza mawazo yao wanaposhiriki katika mazungumzo ya kawaida. Maneno mapya huitwa nominounde ikiwa zimeundwa kutokana na nomino zingine. Maneno mapya ya kileksika yanayoundwa na mshairi maranyingi huwekwa katika kategoria ya nomino-unde. Hata hivyo, maneno haya mapya huwa hayadumu yakilinganishwa na yale yanayoundwa wakati wa mazungumzo ya kawaida. Shairi nzuri husomwa kila mara na hadhira na hata na vizazi vya baadaye. Njia ya kawaida ya kuunda nomino ni uambishaji na uambatishaji au kuweka pamoja nomino mbili. Ukiushi wa kileksia ujidhirisha kwa njia tofautitofauti kwa kutegemea muktadha na mazingira tukijikita kwa sitiari.

1.8.3 Ukiushi wa Kisarufi

Leech (1969) anadai kuwa ili kueleza aina tofauti za ukiushi wa kisarufi basi ni vyema kuelewa tofauti kati ya morfolojia na sintaksia. Kuna tofauti kubwa kati ya umbo nje na umbo ndani wa sentensi za Sintaksia. Umbo ndani hutoa maana ya sentensi na umbo nje hudhihirisha namna ambavyo sentensi hutamkwa. Umbo ndani wa sentensi za kisintaksia huwa na sifa za kisemantiki au hubeba maana na umbo nje ni wa kifonolojia kwa vile hudhihirisha namna ya kutamka na mpangilio wa maneno katika sentensi. Umbo nje wa sentensi huwa haizingatiwi sana katika sentensi changamano. Mara nyingi, hazina athari kubwa kwa namna ambavyo sentensi hueleweka.

1.8.4 Ukiushi wa Kifonolojia

Leech (1969) anatoa kauli kuwa miundo ya sentensi za kifonolojia hujikita zaidi kwa umbo nje kuliko zile sentensi za kisintaksia. Ukiushi wa kifonolojia una umuhimu zaidi katika ushairi wa kiingereza kuliko lugha zingine. Tukirejelea baadhi ya tamaduni za Kimerikani India haswa kwa wanaNootka, sentensi nyingi za kifasihi huwa na ukiushi wa kifonolojia hata wakati wanapojihusisha katika mazungumzo ya kawaida.

1.8.5 Ukiushi wa Kimaandishi au Grafolojia

Leech (1969) asema hata kama tahajia huwakilisha matamshi, matamshi yasiyo ya kawaida yanaakisi kazi ya kifasihi iliyoandikwa kwa njia isiyo ya kawaida. Kuna ukiushi wa grafolojia ambayo haipatikani katika mazungumzo. Hii ni sifa ya shairi linalojitokeza kutokana na mpangilio wa mshororo kwa kila ukurasa na tamati zisizo sawa. Mshororo wa kitaipografia na ubeti wa kitaipografia huwa zinafanana katika maandishi yasiyo ya kishairi katika lugha ya kiingereza. Ukiushi wa grafolojia huwa zina uhuru na uwezo wa

kuingiliana na viakifishi vyote katika viwango vya juu. Mwingiliano huu huwakilisha ujumbe kwa namna ya kipekee katika ushairi.

Mshororo wa ushairi unapokosa kuwa sawa na maneno ya kifonolojia kama ilivyo katika mashairi huru, basi ujumbe katika shairi hilo huwa na muundo usiyoweza kudhibitika. Cumming ni kati ya wale wataalamu wanaotumia ukiushi wa kiothografia kama vile; kutoandika kwa herufi kubwa na kutozingatia viakifishi katika mazungumzo, kuchanganya maneno n.k. Kulingana naye, kuwacha nafasi kati ya maneno katika sentensi, kuandika kwa kuzingatia herufi kubwa na kutumia viakifishi ni mbinu changamano na hazistahili kutumiwa tunapozingatia ukiushi wa kitaipografia.

1.8.6 Ukiushi wa Kisemantiki

Leech (1969) anadai ukiushi wa kisemantiki huwa haueleweki lakini huleta maana tu unapotumika katika mukhtadha wa kifasihi. Maana ya kijuujuu ya maneno yasiyoeleweka kwenye tungo humfanya msomaji kutafakari zaidi ili kuweza kufasiri maneno hayo kwa njia mwafaka inayostahili au inayoeleweka. Katika ushairi, uhamishaji wa maana au tanakali za sauti ni mchakato unaomwezesha msomaji kuelewa tamathali za usemi kutokana na kutoeleweka kwa kazi ya kifasihi.

1.8.7 Ukiushi wa Kilahaja

Leech (1969) asema kuwa ni mbinu ya kukopa vipengele mbalimbali za kijamii au za kimaeneo na huwa inajitokeza sana katika maandishi ya kinathari yanayofanywa na waandishi mbalimbali wanaostahili kutunga kwa kutumia lahaja inayoeleweka na kukubaliwa na wengi. Ukiushi wa kilahaja huwa unatumiwa sana na wasimulizi wa hadithi na wachekeshaji.

1.8.8 Ukiushi wa Sajili au Rejista

Leech (1969) anadai kuwa ukopaji wa sajili katika ushairi huandamana na kuchanganya sajili tofautitofauti ama matumizi ya sifa za vipengele vya sajili tofautitofauti katika muktadha moja. Wakati mwingine utofauti huu hautokani na uhusiano wa lugha pamoja na muktadha wa lugha bali huwa unajitokeza na jambo linalozungumziwa.

1.8.9 Ukiushi wa Kihistoria au Kimapishi

Leech (1969) anadai kuwa uwezo wa kutunga mashairi hutegemea uwezo wa mtu wa kuelewa lugha nyingi bila kujali mipaka wa kidailekti na sajili. Mshairi ana uhuru wa kuchagua na kutumia lugha atakayo bila kuzingatia muda au wakati wa kihistoria. Mashairi ya kiingereza hutumia lugha ya zamani. James Joyce (1964) anasema kuwa mshairi lazima aelewe historia ya lugha yake, yaani lazima awe mwanafilolojia. Naye Eliot (1953) anamuunga mkono James Joyce kwa kunena kuwa hakuna mshairi anayeweza kutoa maana ya shairi kivyake. Hili hueleza ni kwa nini washairi wengi wanahisi kuwa wanatumia lugha moja, njia moja ya kuwasilisha ujumbe hata kama lugha imepitia mabadiliko ya kihistoria kwa muda mrefu.

Aidha, Leech anaendelea kudai kuwa kile kinachotazamwa na mshairi kama utamaduni wake wa lugha inaweza ikajumuisha lugha mfu kama vile Kilatini na Kigiriki. Ukiushi wa kihistoria ulipochipuka baada ya kipindi cha viwanda kilihusisha matumizi ya maneno yenye asili ya Kilatini na maana ya maneno yaliundwa kutokana na elementi za Kilatini.

Ubadilishaji uliopo kati ya lugha ya zamani na lugha ya kisasa ilisisitizwa na tahajia na ina athari sawa unapochanganya sajili. Maendeleo ya kiwakati hujirudia na wakati uliopita na wakati uliopo ni moja.

Katika utafiti wetu, tumefuata mwelekeo wa uhakiki wa mtindo. Mwelekeo huu huzingatia mambo mengi muhimu yanayostahili kuchunguzwa katika matini ya kifasihi kama wanavyofafanua Leech (1969), Simpson (2004) na Wamitila (2008:511). Simpson (2004) ameorodhesha na kueleza vipengele vya kimsingi vinavyoangaziwa na kuhakikiwa katika kazi ya fasihi mtafiti anapotumia uhakiki wa Umtindo. Naye Wamitila (2008:513) anatoa ufafanuzi juu ya vipengele hivi. Vipengele hivi ni pamoja na: Lugha ya kitamathali na mtindo, uteuzi na mtindo, sarufi na mtindo, usimulizi na mtindo, uchimuji na mtindo, itikadi, mtazamo na mtindo, muwala, mshikamano na mtindo, mazungumzo na mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo.

1.8.9.1 Lugha ya Kitamathali na Mtindo

Lugha ya kitamathali na mtindo ni kipengele muhimu sana katika mwelekeo wa uhakiki wa kimtindo na ndiyo sehemu muhimu sana katika uhakiki wetu kwa vile tutahakiki matumizi ya tamathali za usemi katika *Utenzi wa Qiyama*. Uhakiki wa matumizi ya tamathali za usemi katika utenzi huu itatuwezesha kubainisha umuhimu wa lugha katika *Utenzi wa Qiyama*. Mhakiki au mtafiti anastahili kuelewa na kutambua tamathali mbalimbali za usemi ambazo zimetumiwa katika kazi fulani ya kifasihi na kuweza kutathmini athari zinazoletwa na mbinu hizo katika kazi. Katika kazi yoyote ile ya kifasihi, tamathali za usemi zilizotumika hupewa nafasi muhimu lugha ya kifasihi inapochanganuliwa. Matumizi mazuri ya tamathali hizi za usemi katika kazi ya kifasihi humwezesha msanii kuwasilisha ujumbe wake kwa njia ya mkato iliyo na mvuto, mnato na mguso kwa wasomaji lengwa. Aidha, tamathali za usemi kama mbinu mojawapo ya matumizi ya lugha hubana ujumbe hadi kwa kikundi kilichokusudiwa na mtunzi na kuwatenga wale wasiokusudiwa. Kwa hivyo,

matumizi ya tamathali katika kazi ya kifasihi huficha ujumbe hadi pale ujumbe inapowafikia watu waliokusudiwa na kuwafaidi wao wenyewe.

Mwandishi wa fasihi hutumia tamathali za usemi nyingi mno kama vile tashibiha, sitiari, kejeli, tashira, kinaya, tabaini, tanakuzi, kijembe, anafora, dhihaka, ritifaa n.k ili kumwezesha kuwasilisha na kueleza maana ya jambo. Hii humwezesha mwandishi kukiuka mtindo ambao wazungumzaji wamezoea. Simpson (2004:41) anadai kuwa wanamtindo waliipa sitiari na taashira nafasi kubwa kwa vile zinahusisha ubunifu mkubwa katika kuhamisha maana kutoka kwa kitu kimoja hadi kingine katika kazi za kifasihi. Mbinu hizi mbili zilizozingatiwa na wanamtindo zinaubunifu wa hali ya juu kwa vile zinawawezesha wazungumzaji kulinganisha vitu ambavyo vina sifa wanavyoelewa. Kwa mfano, fisi na mtu mlafi. Hivyo basi kuna madai kuwa maneno ya lugha nyingi asili yake ni tamathali za usemi kwa sababu tamathali hizi hujaa katika mazungumzo ya kawaida ya kila siku kwa vile mzungumzaji hutumia tamathali moja au nyingine bila kujua wala kutarajia.

1.8.9.2 Uteuzi na Mtindo

Kipengele hiki cha uteuzi ni muhimu sana katika matumizi ya lugha. Mwandishi ana nafasi na uhuru wa kuchagua msamiati anaotaka kutumia katika kazi yake. Mtunzi ameruhusiwa kutumia maneno ya kale, lahaja au hata lafudhi. Vilevile, mwandishi anaweza kuamua kutotumia maneno haya ya kale, lahaja na lafudhi. Huu ndio mtindo wa mwandishi utakaozingatiwa na wanamtindo na vilevile ndicho kitambulisho cha matini ya mwandishi. Mwandishi anapofanya uteuzi wa aina hii, huwa anaongozwa na kanuni za utunzi au pia yanaweza kutokana na mtindo au njia zake za kibinafsi. Aidha, bali na uteuzi wa msamiati kuna vipengele vingine vya matini vinavyofanyiwa uteuzi, navyo ni; mada, mbinu za

kisimulizi, wahusika na mandhari. Hivi vyote huchangia uteuzi wa msamiati na pia ni sehemu ya mtindo kwa vile vipengele hivi huathiriana.

Vipengele vyote vinane vya mtindo vilivyoainishwa na Wamitila (2008:513) ni pamoja na; lugha ya kitamathali na mtindo, uteuzi na mtindo, sarufi na mtindo, usimulizi na mtindo, uchimuzi na mtindo, itikadi, mtazamo na mtindo, muwala, mshikamano na mtindo, mazungumzo na mbinu za uwasilishaji usemi na mawazo sio lazima vitumiwe vyote kwani Simpson (2004) asema kuwa kila mtunzi ana umilisi wa lugha nyingi lakini ameruhusiwa kuchagua ile anayotaka kutumia katika mazingira mahususi na kuwacha mengine. Hii humwezesha mwandishi kumwathiri msomaji akiwa na nia ya kumwezesha kupata ujumbe aliyokusudia. Uteuzi unaofanywa na mwandishi hujenga na pia hukuza dhamira ya matini husika.

1.8.9.3 Sarufi na Mtindo

Simpson (2004) anadai kuwa mhakiki wa kimtindo anastahili kuchunguza matumizi ya lugha kisarufi. Hii humwezesha yule anayehakiki kuangazia miundo ya Kimofolojia na Kisintaksia na kubaini vile mwandishi ameweza kutumia sarufi kwa kuzingatia lugha au utanzu ambao unashughulikiwa. Mshairi anaidhini ya kufupisha maneno (inkisari), kurefusha maneno (mazda) na kutumia tabdila anapopindua muundo wa Kimofolojia. Hii humpa mtunzi nafasi ya kutosheleza mizani katika mishororo na pia huleta urari wa vina na muundo wa shairi. Abedi (1954) anasema kuwa mshairi anapotosheleza idadi ya mizani kwa mshororo na urari wa vina katika kila ubeti, hulifanya shairi liweze kuimbika. Abedi vilevile anadai kuwa shairi si shairi bila kuweza kuimbika bali ni mkorogo tu wa maneno. Kauli hii ya Abedi inatukumbusha kuhusu mgogoro uliopo baina ya wanashairi huru na wanaarudhi.

Kipera cha kishairi aidha, hupenda kupanga kwa kinyume maneno, vishazi na virai kwa kupindua muundo wa Kisintaksia ili kuleta mvuto na uzuri wa shairi bila kusahau utoshelevu wa urari wa vina na msisitizo. Vilevile, ukiushi huu wa Kisintaksia humwezesha mtunzi kudhihirisha umahiri wake wa utunzi katika matumizi ya lugha. Mhakiki huchunguza miundo ya Kifonolojia, Kimofolojia na ya Kigrafonolojia kubaini athari yake katika muundo wa kazi na maana inayoleta katika utungo.

1.8.9.4 Usimulizi na Mtindo

Kipengele hiki hujumlisha matukio na visa vinavyojitokeza kwa utungo na lazima zifuate mkondo au ruwaza mahususi (msuko). Simpson (2004) anasema kuwa usimulizi ni muhimu kwa vile mpangilio wa matukio katika hadithi ndio huamua namna ambavyo hadithi hiyo hufasiriwa. Usimulizi unaopatikana katika hadithi una sehemu tatu ambazo ni mfichuo, kiini na utatuzi. Mawazo haya ya Simpson (2004) ni sawa na mawazo ya Wamitila (2008).

Tenzi za kale za Kiswahili hufuata muundo huu ambapo unapata kuwa kwenye sehemu ya kwanza mtunzi huanza kwa sala kwa kumshukuru Mungu, kisha anaendelea kwa kumwomba Mtume Muhamadi na familia yake. Mwishowe anadokeza kuhusu kisa anachotaka kusimulia na vile kisa hicho kilimjia ama vile alivyopata kisa hicho. Kwenye sehemu ya pili mtunzi hufululiza moja kwa moja kwenye kisa chake na wakati mwingine mtunzi anaweza kusimulia visa vingine vidogo vidogo ambavyo hujenga kile kisa kuu. Hatimaye mtunzi hutamatisha kwa kutoa utatuzi na kuomba dua kwa kumwezesha kutoa kisa chake kwa ukamilifu bila kusahau kumwomba familia ya Mtume Muhammadi kama ilivyo katika *Utenzi wa Qiyama*. Mhakiki wa kimtindo anajukumu la kutathmini mpangilio wa matukio katika matini na kubainisha vile visa mbalimbali vinavyoingiliana.

1.8.9.5 Uchimuzi na Mtindo

Dhana ya uchimuzi na mitindo imefafanuliwa na wataalamu wengi akiwemo Chapman (1974:48) anayesema kuwa uchimuzi ni ukiushi wa lugha inapotumiwa na mtunzi na lengo la uchimuzi katika kazi ni kuweka wazi kitu kinachozungumziwa. Mawazo yake yanatofautiana na ya Kazungu (1982) anayesema kuwa uchimuzi hautokani tu na ukiushi wa vile lugha inatumiwa bali inajumuisha miundo tofautitofauti ya lugha. Hivyo, kwa kumuunga mkono Kazungu tunasema kuwa uchimuzi ni matumizi ya lugha kwa njia ambayo kitu kinachozungumziwa hujitokeza ikiwa wazi zaidi. Wakati mwingine uchimuzi hutokea katika kiwango cha Kisintaksia au Kisemantiki ambapo maneno huweza kupata maana tofauti au maneno huweza kutumiwa kwa njia isiyo ya kawaida au maana tofauti na ya kawaida kwa kupindua muundo wa vishazi au virai ama kwa kutumia mbinu mbalimbali kama ule wa urudiaji wa neno, sauti au dhana. Huu ni uchimuzi unaojitokeza tamathali za usemi zinapotumika.

1.8.9.6 Mtazamo, Itikadi na Mtindo

Vipengele vya mtazamo na itikadi havina tofauti kubwa kwa vile vinafanana na kufaana pakubwa. Itikadi inachanzo chake kutokana na nadharia ya Umaksi na inarejelea imani na msimao ambao msanii anauchukua na unajitokeza katika kazi yake fulani. Aidha, mtazamo hurejelea mkabala wa kile asemacho msanii au mwandishi. Mkabala wa mtunzi hutokana na imani, fikra na msimamo ambao amejenga juu ya jambo, mtu, hali au kitu ambacho kinazungumziwa. Kulingana na Simpson (2004) njia bora ya kutathmini itikadi na mtazamo wa mtunzi katika kazi ya fasihi ni kuchukulia kana kwamba unataka kupiga picha fulani. Halafu mtunzi ajaribu kuwazia sehemu mbalimbali ambazo yeye kama mpiga picha ataiweka picha au kamera yake ili kupata picha zilizobora zaidi. Simpson anasisitiza kuwa

sehemu hizi mbalimbali zinalingana na vipengele katika kazi ya kifasihi, ambavyo vinaelekeza kwenye itikadi na msimano wa mtunzi au msimulizi wa kazi fulani.

Dhana hizi mbili hudhihirika kwa kuteua vipengele kama vile wahusika mandhari, maudhui na matumizi ya lugha. Matumizi ya lugha huhakikiwa na wanamitindo ili kubainisha vile imetumiwa katika ujenzi na ukuzaji wa mtazamo na itikadi ya msanii kuhusu mambo yaliyomo katika matini yake.

1.8.9.7 Muwala, Mshikamano na Mtindo

Wamitila (2008) anaelezea kuwa muwala hurejelea sifa za kiisimu ambazo huonyesha jinsi maneno, virai, vishazi au sentensi zinavyohusiana katika matini yoyote. Anasema kuwa mshikamano kwa upande mwingine hushughulika na maana ya usemi. Muwala na mshikamano hufanya kazi ya mwandishi iwe na umoja pamoja na udhabiti. Sharti mhakiki wa kimitindo achunguze vile mbinu mbalimbali za kiisimu katika matini vinavyoingiliana na kuleta maana na mpangilio maalum kwa matini husika.

1.8.9.8 Mazungumzo na Mbinu za Kuwasilisha Mawazo

Katika mazungumzo na mbinu za kuwasilisha mawazo, yule ambaye anahakiki hupewa jukumu la kuchunguza vile wahusika wanavyozungumza kwa nia ya kuwasiliana au kutoa mawazo yao. Mawazo haya huweza kuwasilishwa katika usemi halisi na usemi taarifa. Kulingana na Wamitila (2008) usemi halisi na usemi wa taarifa hujitokeza katika nafsi ya kwanza au ya tatu na kuwa ni nadra sana kupata nafsi ya pili ikitumika. Mbinu nyinginezo za uwasilishaji wa mawazo ni uwasilishaji halisi huru na uwasilishaji taarifa huru. Katika uwasilishaji halisi huru alama za mtajo hazitumiki katika kuwasilisha maneno halisi ya mhusika. Aidha, uwasilishaji taarifa huru huwa na kuondolewa kwa

maneno ili kudhihirisha kuwa huo ni usemi wa taarifa, kama njia ya mabadiliko. Mbinu hizi mbili huwa zinatumiwa na watunzi wa tenzi kama vile *Utenzi wa Qiyama* ili kufanikisha malengo ya mtunzi.

Mhakiki wa mwelekeo wa mitindo basi anajukumu la kutathmini na kuchunguza mbinu hizi na vile zinavyodhihirika katika kazi anayohakiki, kwa kuangalia vile mwandishi ametumia mbinu hizi katika kufanikisha kazi yake. Aidha, kupitia uhakiki huo ataweza kujua kufanikiwa au kutofaulu kwa mtunzi katika kutumia mbinu mbalimbali.

1.9 Mihimili ya Kinadharia ya Umtindo

- i. Mtindo wa kazi ya fasihi ndio hutumiwa na msanii kuwasilisha ujumbe wake.
- ii. Upo uwiano baina ya ujumbe na lugha katika kazi ya kifasihi na vipengele hivi viwili haviwezi kutenganishwa.
- iii. Lugha ndicho chombo tekelezi kinachosaidia kuelewa ujumbe uliodhamiriwa na waandishi.
- iv. Mwandishi anaweza kutumia lugha yake kiufundi na athari za kiuajumi huwa hazitenganishwa na vile anatumia lugha kisanaa katika kazi yake.
- v. Uhakiki wa kimtindo huhusu kuchanganua vipengele vya fasihi na vya isimu. Vipengele vya fasihi na vya isimu haviwezi kujisimamia kivyao na kujieleza kikamilifu. Matini mbalimbali hufafanuliwa kwa kutumia fasihi na isimu katika uhakiki wa kimtindo. Nadharia hii inachunguza ujumbe na vile ujumbe huo inavyowasilishwa au mtindo.

Mihimili hii ya kinadharia ya Umtindo ni muhimu kwa vile imetosheleza uhakiki wa kazi yetu. Tumezingatia mihimili hii, ili kuweza kuelewa *Utenzi wa Qiyama* na kuafikia malengo

yetu. Aidha, ni muhimu kutaja kuwa, katika utafiti wetu, hatujatumia mihimili yote. Tumetumia mihimili ya pili, tatu na nne. Mihimili ya pili na ya tatu imetusaidia kuchunguza namna tamathali hizi tano, yaani; takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha zinavyoathiri na zinavyotusaidia katika kujenga taswira inayotuwezesha kuelewa Siku ya Kiyama katika utenzi. Mhimili ya nne umetuweze kuchunguza vile takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha zimetumika katika *Utenzi wa Qiyama*.

1.10 Ufaafu wa Nadharia ya Umtindo

Ni bayana kuwa dhana ya mitindo ni pana sana. Mhakiki wa kifasihi hawezi akashughulikia vipengele vyote. Mhakiki anajukumu la kuleta tu baadhi ya vipengele hivyo na kuvishughulikia kama anavyosema Wamitilia (2008:511) ya kwamba ili mhakiki aishughulikie kazi fulani ya kifasihi vyema, ni sharti achague baadhi ya vipengele vya matumizi ya lugha na avichunguze kwani hawezi kuvimudu vyote. Katika kazi yetu, tumehakiki kipengele cha tamathali za usemi. Hivyo basi tumejaribu kuhakiki tamathali kama vile takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha katika *Utenzi wa Qiyama* kwa vile tamathali za usemi humwezesha mtunzi kuwasilisha ujumbe wake kwa njia ya mkato, kwa njia inayovutia, hurembesha na vilevile kuipatia kazi fulani udhabiti wake.

Ullman (1971) anapendekeza taratibu mbili za kuhakiki kazi za kifasihi. Tumetumia utaratibu wake wa kwanza unaosema kuwa mhakiki huteua vipengele vya lugha vinavyotazamiwa kufanyiwa utafiti na kuchunguza athari za kisanii zinazotokana na vipengele hivyo. Hii inamaana kuwa, mhakiki wa kazi fulani atanza kuhakiki kazi hiyo bila kujua athari itakayotokana na vipengele mbalimbali katika matini hiyo. Kisha, mhakiki husoma matini na kubainisha vile kipengele fulani mahususi kinavyochangia kukua na kuendelea kwa athari fulani. Kwa mfano, mhakiki akiwa na nia ya kuonyesha vile tabaini inavyochangia

kazi fulani basi ataanza kwa kusoma matini mzima huku akidondoa tabaini zinazojidhihirisha katika kazi hiyo. Halafu, ataendelea kwa kufafanua, kueleza na kuonyesha kazi inayotekelezwa na tabaini hizo katika matini husika.

Utafiti wetu umefuata utaratibu huu ambapo tumeweza kubainisha au kutambua vipengele mbalimbali vya tamathali za usemi na kuchunguza athari zinazoletwa na vipengele hivi huku tukitilia mkazo vile vipengele hivi vinavyochangia ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika *Utenzi wa Qiyama*.

Utafiti wetu umeongozwa na mwelekeo wa uhakiki wa Umtindo kwa sababu umefanikisha malengo yetu ya matumizi ya takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha katika ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika *Utenzi wa Qiyama*. Aidha, imetusaidia kufafanua dhana mbalimbali ambayo yanastahili kuangaziwa katika uhakiki wa kimtindo ili kuwezesha kueleweka kwake.

1.11 Njia za Utafiti

Tumeshughulikia mbinu mbalimbali za ukusanyaji data. Aidha, tumedokeza vile tumechanganua data yetu na njia ambayo tumetumia kuwasilisha matokeo yetu.

1.11.1 Mbinu za Ukusanyaji Data

Kwa kuwa utafiti huu ni wa fasihi andishi, utafiti wetu umekuwa wa maktabani. Tumesoma mashairi na tenzi nyingi za kale kwa vile tenzi hizi ndizo zinawekea msingi ushairi wa Kiswahili. Aidha, tumesoma majarida, makala ya mtandao na vitabu vinavyoeleza dhana za takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha. Hili limetusaidia kuelewa kwa undani tamathali hizi tano za usemi na matumizi yake. Tumeusoma utanzu wa ushairi kwa mapana katika tovuti ili kuweza kuelewa msingi wa tamathali hizi tano.

1.11.2 Mbinu za Kuchanganua na Kuwasilisha Data

Njia ambayo tumetumia kuchanganua data yetu imekuwa ni sampuli lengwa. Tumesoma *Utenzi wa Qiyama* ili kuelewa matumizi ya lugha ya utenzi huu. Tumedondoa beti zote ambazo zimetumia mbinu za takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha. Tumeanza kuhakiki utenzi huu bila kujua athari itakayotokana na takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha katika *Utenzi wa Qiyama*. Kisha, tumesoma *Utenzi wa Qiyama* na kubainisha vile takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha zinavyochangia kwa kukua na kuendelea kwa athari fulani. Tumefafanua na kueleza maana ya kila moja wapo ya tamathali hizi tano na kuonyesha vile zilivyotumika ili msanii aweze kujenga taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama. Aidha, tumefafanua dhana mbalimbali zinazostahili kuangaziwa katika uhakiki wa Umtindo ili kuwezesha kueleweka wa kila dhana. Tumewasilisha matokeo yetu kwa njia ya maelezo na ufafanuzi huku tumelenga nadharia ya Umtindo na vipengele vya takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha katika *Utenzi wa Qiyama*.

1.12 Hitimisho

Katika utafiti wetu, tumejikita katika Nadharia ya Umtindo ili kuweza kubainisha iwapo nadharia ya Umtindo imetuwezesha kuafikia malengo yetu ya utafiti. Aidha, kazi yetu imeangazia tamathali tano za usemi ambazo ni takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha. Tumechunguza tamathali hizi ili kuweza kubainisha iwapo zimetusaidia kujenga taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika utenzi huu. Ili kuweza kuafikia malengo ya utafiti wetu, tumeweza kugawa pendekezo letu katika sehemu zifuatazo: Tumetoa utangulizi kwa kutoa muhtasari wa *Utenzi wa Qiyama* na tamathali za usemi kwa ujumla. Kisha tumeshughulikia tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada yetu ya

matumizi ya takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha katika *Utenzi wa Qiyama*. Aidha, tumedokeza upeo na mipaka, nadharia tete, vilevile tumeweze kuangazia yaliyoandikwa kuhusu mada yetu, msingi wa nadharia yetu na vile imetufaa katika utafiti wetu. Hatimaye, tumeshughulikia njia mbalimbali za utafiti ambazo zimetuwezesha kufanikisha utafiti wetu kwa kuangazia mbinu za ukusanyaji data na mbinu za kuchanganua data.

SURA YA PILI

2.0 UFAFANUZI WA DHANA YA TAKRIRI, TASWIRA, TASHBIHI, TASHIHISI, SITIARI NA MASWALI YA BALAGHA

2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumeshughulikia kwa kifupi tamathali za usemi na mbinu nyinginezo. Aidha, tumejadili maana ya takriri na aina zake, kipengele cha tashihisi, tashibihi, aina mbalimbali za sitiari na maswali ya balagha. Vilevile tumeweza kujadili mbinu ya taswira na aina mbalimbali za taswira katika sura hii.

2.2 Tamathali za Usemi na Mbinu Nyinginezo za Lugha

Tamathali za usemi zinahusu matumizi ya maneno ambayo yana maana fiche, maneno yenye maana ya kinyume na ile ya kawaida au yasiyo ya moja kwa moja kwa lengo la kurembesha usanii na kufundisha. Tamathali hizi hujitokeza sana katika kazi ya kifasihi na mazungumzo ya kawaida. Kazi yoyote ile iliyo na tamathali huvutia, huwa ina nata na huleta msisitizo kwa kile kinachosemwa. Holman na Harman (1986:2002) wanadai kuwa tamathali za usemi zina husu kutumia lugha kwa kukiuka mtindo ambao watu wamezoea ili kuleta athari au maana fulani.

Kauli hii ina maana kuwa matumizi ya tamathali za usemi huenda kinyume na mazungumzo ambayo watu wamezoea katika maisha yao ya kawaida, inayofuata kanuni na mpangilio mahususi wa maneno wanapozungumza. Katika maisha ya kila siku, mwanadamu hutumia tamathali mbalimbali katika mazungumzo yao ya kawaida bila kujua au kutarajia. Kauli hii huleta maana kuwa asili ya maneno mengi yanayopatikana katika lugha mbalimbali za jamii tofautitofauti ni tamathali za usemi.

Msokile (1993:39) anasema kuwa tamathali za usemi inaweza kuwa nahau, neno au maneno, ama hata misemo zinazotumiwa na wasanii wa fasihi kwa lengo la kutia nguvu na kusisitiza maana ya jambo, mtindo na sauti katika kazi hizo. Msokile anasisitiza kuwa tamathali za usemi huwa zinatumiwa katika kazi ya kifasihi ili kupamba kazi hiyo kwa kuongeza ladha ya lugha.

Mwandishi wa kazi ya kifasihi ana uwezo wa kuathiri msomaji wake kwa kudhihirisha hisia zake kupitia kwa tamathali za usemi na mbinu nyinginezo anazotumia. Takriri na maswali ya balagha ni mifano ya mbinu nyinginezo. Mbinu hizi zinachangia katika kuleta maana katika *Utenzi wa Qiyama*. Mbinu nyinginezo ni mbinu ambazo hazihitaji maana fiche.

Tamathali za usemi huwa zinamsaidia msanii kupanga kazi yake na mawazo yake kwa njia inayovutia. Mwandishi wa kazi ya kifasihi ana uwezo wa kuathiri msomaji wake kwa kudhihirisha hisia zake kupitia kwa tamathali za usemi na mbinu nyinginezo anazotumia.

2.3 Takriri

Kuhenga (1977) na Msokile (1993:61) wanadai kuwa takriri ni mtindo ambao unatumia na msanii kunena kwa ufasaha kimaksudi au msanii akiwa na madhumuni ya kusisitiza au kutilia mkazo yale maneno ambayo yamerudiwa kwa lengo la kusisitiza ujumbe unaopitishwa. Mtindo wa kutumia takriri mara nyingi hupatia jambo linalosemwa na msanii uzito na vilevile jambo hilo linaweza kuwa na udhabiti wa aina fulani ili msomaji aweze kuelewa ujumbe wa mtunzi kwa undani zaidi.

Wamitila (2003:221) anasema kuwa takriri ni urudiaji wa kukariri, wa kutokea mara kadha. Matumizi ya takriri katika kazi ya kifasihi huleta msisitizo mkubwa wa ujumbe na athari kubwa kwa wasomaji. Wamitila anadai kuwa mshairi anaweza kurudia neno au maneno

fulani kwa nia ya kuyasisitiza na kwa njia hii kuzua hisia fulani kwa msomaji na kumfanya ayawazie maneno hayo. Takriri hupatikana katika kiwango cha vina, mizani, sauti, neno, mistari na kifungu. Wamitila anasema kuwa katika ushairi, urudiaji wa sauti ndio kiwango cha chini zaidi.

Kwa maoni yetu, takriri ni mbinu inayotumiwa na msanii kwa madhumuni ya kuthibitisha au kuisitiza jambo linalosemwa. Aidha, mbinu hii humwezesha msomaji kurudiarudia au kusema kauli fulani tena na tena kwa nia ya kuisitiza linalosemwa kimoyomoyo au kwa sauti ili kuleta uthabiti wa aina fulani ili jambo au ujumbe unaopitishwa usisahaulike kwa haraka au kwa urahisi.

2.3.1 Aina za Takriri

Kuna aina nne za takriri, yaani takriri irabu, takriri konsonanti, takriri neno na takriri silabi. Katika sehemu hii tumejadili aina hizi nne za takriri ili kuweka wazi tofauti uliopo kati ya takriri hizi.

2.3.2 Takriri Irabu au Vokali

Takriri irabu ni urudiaji wa sauti unaojitokeza kutokana na urudiaji wa irabu katika kazi ya fasihi. Urudiaji wa irabu au vokali katika kazi ya fasihi hasa katika shairi huleta wizani katika kazi hiyo. Wamitila (2003:156) anasisitiza kuwa takriri irabu hutumiwa au hujitokeza kama sifa ya lugha. Takriri ya aina hii hujitokeza sana katika tenzi za kale kama vile *Utenzi wa Qiyama*, *Utenzi wa Ngamia na Paa*, *Utenzi wa Mwanakupona*, *Utenzi wa Ayubu* n.k. Katika *Utenzi wa Qiyama* mfano ni katika ubeti wa 171 sauti **a** imerudiwa mwanzoni mwa mishororo ya kwanza tatu. Mifano zaidi ni katika ubeti wa 168, 170, 199, 232, 250 na wa 265.

2.3.3 Takriri Konsonanti

Takriri konsonanti huwa inadhihirika kwa kurudia konsonanti. Konsonanti inayorudiwa huwa inapatikana mwanzoni au mwishoni mwa mshororo wa shairi. Takriri konsonanti ni urudiaji unaojitokeza ukiwa wazi sana. Wamitila (2003:195) anadai kuwa takriri konsonanti hujitokeza zaidi katika kazi za kiingereza kuliko za Kiswahili kwa vile katika ushairi wa Kiswahili muundo wa konsonanti hufuatwa na irabu. Kwa maoni yetu, takriri konsonanti ni urudiaji wa konsonanti aidha mwanzoni au mwishoni mwa mshororo wa ubeti katika shairi. Mfano wa takriri konsonanti katika *Utenzi wa Qiyama* ni laki laki lukuki katika ubeti wa 8.

2.3.4 Takriri Neno au Maneno

Takriri neno ni njia ya kurudia neno au maneno katika kazi ya kifasihi kwa lengo la kusisitiza linalosemwa. Wakati mwingine msanii anaweza kurudia neno ili kuleta dhana ya kucheza na maneno katika kazi yake. Kwa mfano katika *Utenzi wa Qiyama* maneno kama vile Neno “taa” limerudiwa kwa wingi katika utenzi huu na msanii. Neno hili limetumiwa katika beti zifuatazo; ubeti wa 32, 179, 222, 237, 243 na wa 244.

2.3.5 Takriri Silabi

Takriri silabi huhusisha urudiaji wa silabi katika utungo. Urudiaji huu ni jumla ya silabi za konsonanti na irabu. Takriri silabi, mara nyingi, hujitokeza mwishoni mwa mshororo katika ushairi. Aidha, ni urudiaji unaoweza kujitokeza mwanzoni mwa mshororo na vilevile katika vina vya shairi. Takriri ya aina hii hujitokeza sana katika mashairi na hudhihirika kwa njia iliyo wazi zaidi kwa msomaji. Mfano katika *Utenzi wa Qiyama* ni katika ubeti za 160 na wa 296. Katika beti hizi silabi **u** imetumiwa kama takriri silabi ya mwanzoni mwa mshororo.

Aidha, silabi **u** na **o** zimetumiwa kama silabi za mwishoni mwa mshororo katika ubeti wa 26 na wa 149.

2.4 Dhana ya Taswira

Mulokozi na Kahigi (1979) wanasema taswira ni mbinu inayotumia picha katika kazi za kisanaa. Aidha, picha hiyo inadhihirika katika mawazo au akili ya msomaji kutokana na ujumbe unaowasilishwa na msanii. Mulokozi na Kahigi (1979) wanatoa kauli kuwa ili picha ijengwe katika kazi ya kisanaa lazima kuwe na matumizi mazuri ya lugha ambayo maneno yake yameteuliwa vizuri, mtunzi lazima awe mwangalifu na maelezo yake yawe dhahiri, yaweze kuhusisha na kujumuisha dhana moja kwa ajili ya kujenga picha na kuleta athari maalum katika akili ya msomaji kutokana na ujumbe unaowasilishwa katika kazi ya msanii.

Naye Njogu na Chimerah (1999:32) wanaeleza kuwa picha katika kazi ya kifasihi huwa inajengwa katika akili ya msomaji kutokana na uwezo wake wa kulinganisha dhana mbalimbali, jambo linalosemwa au chombo ambacho kinarejelewa na picha ambayo imechorwa. Wamitila (2003:197) anadai kuwa taswira ni picha ambazo zinamkujia msomaji akilini wakati anapoisoma kazi fulani ya kifasihi. Aidha, Wamitila anauliza picha hizi hutokana na nini? ama picha hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi ama tamathali za usemi ambazo zimetumiwa katika kazi fulani ya kifasihi? Wamitila (khj) anatoa kauli kuwa taswira au picha mbalimbali huwa zinajengwa kwa kutumia mbinu au njia tofautitofauti, kwa mfano kuna taswira zinazojengwa kutokana na maelezo pekee na taswira hizi hazina maana nyingine zaidi. Taswira hizi hujulikana kama taswira za kimaelezo. Aina ya pili ya taswira kulingana na Wamitila ni taswira za kiishara ambazo huwa zina maana nyingine ya ziada. Wamitila aidha anadai kuwa taswira mbalimbali huwa zinabuniwa kutokana na hisia mbalimbali za kibinadamu. Kwa sababu hii, anasisitiza kuwa kuna picha zinazolenga

kuchochea kutazama, kuonja, kunusa, kusikia n.k. Mfano katika *Utenzi wa Qiyama* ni katika ubeti wa 143 na wa 296 wa ambapo picha ya kuona inachorwa na mtunzi anapotuelezea vile moto iliyo na majoka itakavyowachoma wanadamu huku wakilia na kuangamia kutokana na ukali wa moto na kuumwa na majoka kule Jehanamu.

Senkoro (2011) anadai kuwa ili msanii aweze kujenga picha nzuri basi ni lazima aelewe kikamilifu mambo ambayo yanamzunguka na jamii anamoishi kisha aweze kuyaleta katika kazi yake. Aidha, anasisitiza kuwa ni muhimu kwa msanii kuelewa historia na mambo mengine ya kijumla ya maisha kwa vile yanachangia ujenzi wa picha nzuri katika kazi ya kifasihi. Senkoro anaeleza kuwa picha iliyojengwa vizuri katika kazi huwasilisha ujumbe thabiti na kamilifu kwa msomaji na huwa inaongeza uwezo wa msomaji wa kuhifadhi na kukumbuka ujumbe kwa muda mrefu.

Kwa maoni yetu, taswira ni picha ambayo msomaji anajenga akilini mwake anaposoma kazi ya kifasihi kutokana na maelezo ya mtunzi. Aidha, taswira huleta uhalisia katika kazi ya kifasihi kwa vile msomaji ana uwezo wa kulinganisha kinachoelezwa na hali ya kawaida.

Taswira inapotumika katika kazi ya kifasihi huwa inalenga kutekeleza jukumu la kuchochea hisia za aina fulani kwa wasomaji. Kwa njia hii msanii hupitisha ujumbe wake kwa nguvu kwa wasomaji wake. Picha au taswira iliyojengwa kwa njia nzuri katika kazi ya kifasihi huleta mvuto wa kisanaa kwa kazi hiyo. Hivyo, msomaji huwa anapata motisha ya kutaka kuendelea kusoma kazi hiyo yenye taswira inayovutia.

2.4.1 Aina ya Taswira

Katika sehemu hii tunajadili aina mbalimbali za taswira ikiwemo; taswira za kuona, mnuso, mguso, mwonjo, usikivu, mwendo na joto.

2.4.2 Taswira za Kuona

Taswira ya aina hii inapotumiwa na msanii katika kazi ya kifasihi humwezesha msanii au msomaji kujenga picha ya kuona machoni mwake. Taswira ya kuona humwezesha msomaji kulinganisha anachosoma na hali ya kuonekana katika mazingira ya kawaida. Mfano katika *Utenzi wa Qiyama* ni katika ubeti wa 143 na wa 296 ambapo picha ya kuona inachorwa na mtunzi anapotuelezea vile moto iliyo na majoka itakavyowachoma wanadamu huku wakilia na kuangamia kutokana na ukali wa moto na kuumwa na majoka kule Jehanamu.

2.4.3 Taswira za Mnuso au Harufu

Taswira za mnuso au harufu ni mbinu inayomwezesha msomaji kujenga picha ya harufu katika usomaji wake wa kazi ya kifasihi. Wamitila (2003:197) anatoa mfano wa takriri ya mnuso kutoka katika *Utenzi wa Al-Inkishafi* wakati msanii wa utenzi huu anapolinganisha dunia na mzoga wa mnyama. Dunia inapolinganishwa na mzoga inamwezesha msomaji kujenga picha ya harufu mbaya. Dunia inapolinganishwa na mzoga inamfanya msomaji kuona dunia kama sehemu isiyostahili kwa vile ni chafu na ina uvundo ambao hauvumiliki. Katika *Utenzi wa Qiyama* taswira ya aina hii inajitokeza tunapochorewa picha ya watenda dhambi wakichomeka Jehanamu. Harufu ya vile watu watakavyoungua inajidhihirisha katika ubeti wa 296.

2.4.4 Taswira za Mguso

Taswira ya mguso ni taswira inayomwezesha msomaji kujenga picha ya kugusa kitu au vitu viwili au zaidi vinapotolewa maeleza ya kugusana wakati ana soma kazi ya kifasihi. Mfano katika *Utenzi wa Qiyama* unajitokeza wakati Mtume Muhamadi anapomshika farasi wake ili aweze kumpanda katika ubeti wa 96 farasi anakataa na kumtoroka hadi anapomwahidi

kumtetea siku ya mwisho. Baada ya Mtume kutoa ahadi kwa farasi wake ndipo farasi huyo anamkaribia na kukubali kushikwa na kupandwa.

2.4.5 Taswira za Mwonjo

Taswira hii hujengwa kutokana na hisia za kuonja. Kwa mfano ni taswira ambayo inaweza kutokana na maelezo ya upishi haswa mwandishi anapoelezea namna ya kuandaa mlo au mamkuli mahususi kama vile upishi wa nyama au kuku kwa kuiongezea viungo mbalimbali hadi wakati chakula chenyewe kinapopakuliwa kwenye sahani.

2.4.6 Taswira za Usikivu

Taswira ya usikivu hujengwa na msomaji kutokana na taswira ambazo zinahusishwa na sauti. Katika kazi ya kifasihi, hii ni taswira inayojitokeza msanii anapoelezea namna ambavyo mhusika fulani anavyolia kwa sauti ya uchungu, namna ambavyo mhusika anavyocheka kwa sauti ya furaha, au vile mhusika anavyoimba kwa sauti nyororo au laini. Vitendo hivi vya mhusika humwezesha msomaji kujenga picha ya kusikia akilini mwake. Wamitila (2003:198) anatoa mfano wa taswira hii katika riwaya ya *Siku njema* anaporejelea vile Zawadi analia kutokana na kifo cha Rashidi. Mfano katika *Utenzi wa Qiyama* ni katika beti za 65, 128, 230, 231 na 296. Katika beti hizi sauti za watu zinasikika wakilia kwa maumivu na machungu kutokana na mateso wanaopata motoni. Aidha, katika ubeti wa 65 sauti ya malaika Jibrili inasikika akiwalilia umma kwa sababu ya mateso na hukumu wanaopata kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

2.4.7 Taswira za Mwendo

Ni taswira inayojenga picha ya mwendo kwa msomaji kutokana na matendo ya wahusika katika kazi ya kisanaa. Taswira hii inajengwa kutokana na mwendo wa pole, mwendo wa

haraka, au mwendo wa wastani kwa sababu ya matendo ya wahusika au shughuli zao katika kazi ya kifasihi. Kwa mfano katika ubeti wa 87 tumechorewa picha ya namna ambavyo watu watapita swirati kwa mwendo wa haraka kama umeme katika *Utenzi wa Qiyama*.

2.4.8 Taswira za Joto

Taswira ya aina hii inauhusishwa na joto kwa sababu msanii huwa anatumia maneno yanoyodhihirisha hali ya joto katika kazi yake. Wakati msomaji anaposoma kazi fulani ya kifasihi picha za joto zinaweza zikamjia akilini mwake kutokana na maelezo fulani. Kwa mfano msanii anapoelezea hali ya mhusika anayefanya kazi kwa bidii kukiwa na jua kali. Taswira ya joto inaweza kujidhihirisha wakati msanii anapoelezea hali ya mhusika aliyeota ndoto ya ajabu usiku wa manane hasa anaposhtuliwa na ndoto yake na kisha kuamka kwa mshtuko. Mfano katika *Utenzi wa Qiyama* unajidhihirisha katika ubeti wa 295, 296 na wa 297 tumapoelezewa ukali wa moto utakaowachoma watenda dhambi siku ya mwisho haswa tunapoambiwa kuwa moto ya Jehanamu itawachoma watu kwa fujo.

2.5 Tashibihi

Tashibihi ni ulinganishi wa moja kwa moja. Ulinganishi huu hutumia viunganishi kama vile: “ja”, “mithili ya”, “kama”. “kama vile”, “sawa na”, “tamthili ya” n.k. Leech (1969:156) anena kuwa tashibihi ni tamathali ya usemi iliyo na maana ya kijuujuu ikilinganishwa na jazanda kwa vile jazanda ina maana ya kindani zaidi. Msokile (1993:40) asema kuwa tashibihi ni tamathali ya usemi inayolinganisha vitu vitatu yaani kizungumziwa, kiungo na kifananishi. Kuhenga (1977:15) anasema kuwa neno tashibihi limeundwa kutoka kwa neno shabihi lililo na maana ya kuwa sawasawa, kulingana au kufanana. Kwa mujibu wa Kuhenga, tashibihi ni mtindo wa kusema ambao hulinganisha kitu kimoja au zaidi na kitu kingine au

vitu vingine tofauti. Kwake tashbihi hulinganisha sura ya kitu, rangi ya kitu na namna ya kujimudu kwa kitu au vitu.

Wamitila (2003:193) anadai kuwa tashbihi ni ulinganishi unaodhamiriwa kusesitiza sifa fulani na pia huwa inajenga picha fulani akilini. Wamitila anafafanua kuwa tunaweza kushughulikia tashbihi kama kilinganishi ambapo vitu viwili vinalinganishwa ili kuleta maana fulani, hivyo umuhimu wake hauishi kwenye kilinganishi pekee. Mkondo wa pili wa kufafanua maana ya tashbihi ndiyo bora zaidi kwa sababu mkondo huu hushughulikia tashbihi kama aina ya tamathali za usemi. Maelezo haya ya wataalamu mbalimbali yametusaidia katika kuelewa maana ya tashbihi kwa undaini. Kwa maoni yetu, tashbihi ni ulinganishi wa moja kwa moja unaotumia vilinganishi kama vile “ja”, “kama”, “kama vile” n.k. Aidha, maelezo haya ni muhimu kwa vile yametusaidia katika kutambua tashbihi yaliyotumiwa katika *Utezi wa Qiyama*.

2.5.1 Aina ya Tashbihi

Katika sehemu hii tumeshughulikia aina mbalimbali ya tashbihi kama vile tashbihi fiche, tashbihi wazi na tashbihi ya kiutendi. Aidha, ufafanuzi wa aina hizi za tashbihi zimetusaidia katika kutambua kila aina na vile zimetumiwa katika *Utenzi wa Qiyama*.

2.5.2 Tashbihi Fiche

Tashbihi fiche huwa inalinganisha vitu kwa njia isiyo ya wazi yaani kwa njia fiche. Mhakiki yeyote yule anapohakiki tashbihi fiche katika kazi ya fasihi ni lazima awaze au atafakari zaidi ili kuweza kuelewa maana ya kile kitu kinachowasilishwa na tashbihi hii. Ili mhakiki aweze kuhakiki vyema kazi ya kifasihi ni lazima awe na ufahamu wa sifa na tabia za kilinganishi. Sifa na tabia za kilinganishi zinaeleweka tu katika muktadha wake mahususi wa matumizi

kwa sababu kila muktadha una sifa na tabia zake za kilinganishi. Tashbihi fiche hufasiriwa kwa njia mbalimbali au tofautitofauti kwa sababu ina sifa na tabia za kilinganishi. Kwa mfano, *Joni ni mbwa*. Neno mbwa lina sifa ya ujasiri na ukali. Sifa hizi za mbwa zitatumiwa tu kwa kutegemea muktadha. Mfano wa pili ni *Papa ni sungura*. Neno sungura lina sifa ya ujanja na udanganyifu. Ili mhakiki aelewe sifa anayotaka kati ya ujanja na ujinga ni lazima basi arejeele muktadha wa matumizi wa maneno *Papa ni sungura*.

2.5.3 Tashbihi Wazi

Tashbihi wazi ni tamathali ya usemi inayowasilisha maana kwa njia ya moja kwa moja au kwa uwazi kwa sababu inaeleweka kwa urahisi bila kutafakari wakati wa kuhakiki kazi ya kifasihi. Kwa mfano, tunaweza kusema kuwa Didi ni mjanja kama sungura. Neno mjanja katika mfano huu ndilo msingi wa kumlinganisha Didi na sungura. Neno mjanja linatuelezea wazi tabia ya sungura ambayo imehamishwa moja kwa moja hadi kwa Didi.

2.5.4 Tashbihi ya Kiutendi

Ni tashbihi ambayo inapatikana katika mashairi ya kiutendi na tutumbi. Sifa mojawapo kuu ya tashbihi ya kiutendi ni kuwa huwa inajenga taswira ambayo inahusishwa na kilinganishi ambacho kimetumiwa. Mfano katika *Utenzi wa Qiyama*.

Moto ukatowa ndimi
Ukipiga na zivumi
Kula mtu kamba mimi
Utakao nijiliya (ubeti 295)

Katika mfano huu watu waliowaasi Mwenyezi Mungu wanasikia sauti ya moto inayotisha inayoweza kulinganishwa na sauti ya mazimwi inayojenga picha ya kuwatishia wanadamu

siku ya mwisho. Aidha, sauti hii inajenga picha ya hisia za hofu, mateso na maangamio kwa Makafiri.

2.6 Mbinu ya Tashihisi

Kuhenga (1977:15) anatoa kauli yake kwa kusema kuwa tashihisi ni mbinu inayotumiwa na mtunzi ili kupatia kitu ambacho hakina uhai au kitu cha kidhahania kinaweza kikapewa sifa za kibinadamu. Kuhenga anatoa ufafanuzi kwa madai yake kuwa tashihisi ndiyo mbinu inayopatia vitu ambavyo siyo binadamu kama vile wanyama na wadudu sifa ya binadamu. Hii ni kwa sababu tashihisi inanafsisha ama inafanya kitu kuwa na maumbile.

Njogu na Chimera (1999:91) wanadai kuwa tashihisi ni mbinu ya kitamathali inayoipa kitu ambacho hakina uhai kamilifu sifa za kitu au vitu vyenye uhai ambavyo hujitegemea katika mazingira yake mahususi. Msokile (1993:40) na Senkoro (2011) wanaunga mkono maelezo haya kwa kusema kuwa tashihisi pia hurejelewa kama fasili ya binadamu. Wanathibitisha madai yao kwa kusema kuwa vitu visivyo na uhai na sifa ambazo wanadamu wanazo hupewa sifa hizo. Wataalamu hawa wawili wanaendelea kwa kusema kuwa mbinu hii ya tashihisi ni muhimu kwa kuwa kupitia kwayo vitu ambavyo ni vitulivu vinatiwa nguvu na kuonekana vikiwa katika mwendo wa taharuki na picha. Sifa hii inamwezesha msomaji kuelewa ujumbe kwa njia iliyo wazi zaidi na kupata mvuto uliohabit.

Naye Wamitila (2003:194) asema kuwa ni mbinu inayomwezesha mwandishi kupatia kitu kisichokuwa na uhai uwezo huo wa kuishi. Anatoa kauli kuwa mbinu hii wakati mwingine huweza kutumiwa ili kuleta athari fulani ya kihisia. Kwa maoni yetu, tashihisi ni mbinu inayotumiwa na mtunzi ili kupatia vitu visivyo na uhai uwezo na sifa za kutenda kama mwanadamu. Mfano katika *Utenzi wa Qiyama*.

Moto ukawa kuvuma
Ukiwala zao nyama
Basi ikawa zahama
Na kelele kujutiya. (ubeti 294)

2.7 Sitiari

Sitiari ni ulinganishi usiokuwa wa moja kwa moja. Sitiari inalinganisha vitu viwili au kitu kimoja na kingine bila ya kutumia viunganishi kama vile “ja”, “mithili ya ”, “kama”, “kama vile”, n.k. Leech (1969:151) anadai kuwa mbinu ya sitiari huwa inatumiwa na mtunzi ili kuhamisha maana ya kitu kimoja mapaki kwa kitu kingine bila kurejelea dhana. Leech anaendelea kunena kuwa sitiari inaongozwa na kanuni au kaida inayoitwa kanuni ya sitiari. Leech anaelezea kanuni yake kwa kutumia **F** na **L**. Katika kanuni hii, **F** itachukuliwa kama kilinganishi na **L** ni kilinganishwa.

F = ni kama **L**

(Kilinganishi)

(Kilinganishwa)

Leech anasema kuwa uhamisho wa sitiari hujitokeza tu iwapo kuna uhusiano wa aina fulani kati ya vitu vinavyolinganishwa.

Kuhenga (1977) anadai kuwa neno sitiari lilibuniwa kutoka kwa neno sitiari ambalo linamaanisha funika. Kwake Kuhenga sitiari ni tamathali ya usemi inayolinganisha kitu au vitu vyenye matendo mbalimbali au vitu vyenye hulka tofautitofauti na hali sawasawa ili kufichua hisia. Kwa mujibu wa msokile (1993:40) mbinu ya sitiari hutumiwa sana katika hadithi. Anakiri kuwa mbinu hii hutumiwa kwa njia ambayo imepanuka zaidi katika hekaya na hurafa. Kuhenga anadai kuwa hadithi za hekaya na hurafa huwa zinawahusu wanyama

lakini wanyama hawa wanawakilisha wanadamu kitabia, kimatendo na kisifa. Katika hadithi hizi, matendo ya wanyama yanasimulia matendo ya wanadamu. Hadithi yote huwa ni sitiari.

Wamitila (2003:193) na Njogu na Chimera (1999:91) wanatoa kauli sawa kwa kusema kuwa, mbinu hii ni muhimu katika ujengaji wa taswira. Aidha, sitiari hukuza sifa ya kulinganisha kwa kusema kitu fulani ni kingine. Mfano katika *Utenzi wa Qiyama*: Na pepo hiyo ni kusi (ubeti 23) Na upepo hiyo wadudi (ubeti 24), n.k. Wa Mutiso (2005) asema kuwa sitiari ni tamathali ya usemi inayolinganisha vitu vyenye tabia inayofanana. Aidha, Wa Mutiso anaendelea kusema kuwa vitu hivi viwili vinavyolinganishwa katika sitiari huwa vinatofautiana kimaumbile na kitabia. Lengo kuu la sitiari huwa ni kujenga picha. Lengo hili huafikiwa na msanii kwa kutotumia vilinganishi kama vile, ja, kama, kama vile, n.k.

Kwa maoni yetu sitiari ina misingi yake katika uhamishaji wa maana. Sitiari ni mbinu ya kulinganisha vitu viwili au zaidi bila viunganishi mbalimbali. Dhana ya sitiari hivyo basi, ina stahili kuchunguzwa katika mazungumzo na maandishi wakati tunapochunguza kazi yoyote ile ya kifasihi.

2.7.1 Aina za Sitiari

Wataalamu mbalimbali ikiwemo Leech (1969) na Wamitila (2008) wameweza kuweka sitiari katika makundi mbalimbali. Leech (1969:158) asema kuwa sitiari za aina mbalimbali huzuka kutokana na uhusiano wa maana kwenye matini na maana ya kitamathali. Wamitila (2008:421) anadai kuwa, sitiari za aina mbalimbali zinachanganuliwa kutokana na dhana ya kilinganishi, kilinganishwa na msingi. Dhana hizi tatu zimezewesha mtaalamu huyu kuzuka na aina mbalimbali za sitiari.

2.7.2 Sitiari Chakavu

Sitiari chakavu pia hurejelewa kama istiari fifi kwa sababu ya mpito wa wakati ambayo hufanya taswira iliyorejelewa kama sitiari kutorejelewa hivyo tena kwa vile imepoteza sifa ya mshtukizo ambayo ndiyo sifa muhimu katika sitiari. Sitiari chakavu ni sitiari ambayo maneno yake, virai vyake au kauli zake kama sitiari chakavu zimepoteza uwezo wake wa kitamathali kutokana na hali kuwa zimetumiwa sana. Wamitila (2008:422) asema kuwa, sitiari chakavu imepoteza upya wake na pia ubunifu wake kwa vile zimechakaa na kuwa hafifu. Aidha, Wamitila anatoa mfano kwa kusema kuwa tunapomrejelea mtu fulani kama nyoka katika mazungumzo ya kawaida, basi tunatumia sitiari chakavu kwa vile nyoka ni kilinganishi cha ukatili na uovu ambayo imefifia. Sitiari chakavu ina sifa za michuuko, hivyo basi sitiari hii inaweza ikafafanuliwa kama sitiari michuuko.

2.7.3 Sitiari Dhana

Hii ni sitiari inayotuwezesha kuelewa kitu fulani maalumu kwa misingi ya kitu kingine. Wamitila (2008:423) asema kuwa, ni sitiari ambayo inatokea pale ambapo kitu kilicho katika muktadha mahususi hueleweka kinapowekwa katika mawanda mengine tofauti. Sitiari dhana hutumiwa na wazungumzaji wa lugha fulani kwa ukawaida au kwa mazungumzo yao ya kila siku bila kujua kuwa wametumia sitiari dhana. Sitiari dhana hutumiwa katika taaluma au sajili mbalimbali. Katika sitiari dhana, vitu vilivyo na sifa maalumu zinazohusishwa na muktadha mahususi zinahamishwa kwenye muktadha mwingine. Wamitila (2008:423) anatoa mifano ifuatayo ya sitiari dhana: Maisha ni safari na wakati ni pesa. Katika mfano wa wakati ni pesa, Wamitila anasisitiza kuwa wakati ni dhana dhanaisha na pesa ni dhana dhabiti. Hivyo basi, wakati ni muhimu kama pesa kwa vile bila pesa huwezi ukatenda chochote na vile

utakavyoangaliwa na kuchukuliwa na wengine pia ni tofauti kulingana na kuwa nayo au kukosa kwayo.

Kwa maoni yetu, tunamuunga Wamitila mkono kwa kusema kuwa sitiari dhana ni mbinu inayotumiwa na mtunzi kuhamisha maana ya kitu fulani iliyo na sifa mahususi kutoka kwa muktadha moja hadi mwingine na maana ya kitu hicho kueleweka kivingine kulingana na muktadha huo.

2.7.4 Sitiari Radidifu

Sitiari radidifu ni pana na haielezi wazi vilinganishi vyote viwili vinavolinganishwa. Sitiari hii haiweki wazi kilinganishi na kilinganishwa ila huwa inaelezea vilinganishi bila kutaja kilinganishwa. Wamitila (2008:422) anatoa mfano ufuatao wa sitiari radidifu *akihema alituana kupiga chenga, akageresha na kujitoma ulingoni wa siasa*. Katika mfano huu kuongea kunalinganishwa na kucheza kandanda. Vilevile wanasiasa wanalinganishwa na kucheza kandanda katika mfano huu.

2.7.5 Sitiari Mseto

Sitiari mseto ni sitiari inayojitokeza katika kazi ya fasihi au ushairi tunapokuwa na sitiari nyingi katika sentensi moja zinazorejelea dhana moja. Katika aina hii ya sitiari, sitiari zaidi ya moja hutumiwa kwa pamoja kurejelea dhana. Wamitila (2008:424) anatoa mfano huu “Tusipogeza mwendo wetu katika mjadala huu tutaishia kutumbukia kwenye matatizo makubwa sana tubakie kutapatapa gizani”. Mfano huu una sitiari kama vile mwendo, kutumbukia na kutapatapa gizani. Mwendo humrejelea mtu ambaye anasafiri, kutumbukia kunaashiria shimo au mto na kutapatapa gizani inarejelea giza, maovu au ujinga.

2.7.6 Sitiari Sahili

Katika sitiari sahili msingi wa kilinganishi na kilinganishwa ni wa moja kwa moja. Sitiari sahili ni rahisi sana na mwepesi kubainisha kwa vile kilinganishi huwa na maana moja inayohusishwa na kilinganishwa. Kwa mfano Dama ni simba. Dama analinganishwa na simba labda kwa sifa yake ya ukali yaani ni mkali na hapendi mchezo. Vilevile tunaweza tukasema kuwa ukali wake unatokana na sifa yake ya kuwatendea wengine unyama na ukatili, dhuluma anayowatendea watu wengine. Aidha, ukali wa Dama unatokana na hali yake ya kutovumilia michezo na ucheshi kutoka kwa watu wengine. Mfano wa pili Kerubo ni fisi. Kerubo kulinganishwa na fisi inatokana labda na sifa yake ya kuwa mchoyo na kuwapokonya wengine vitu vyao au kuwa na tamaa kwa vitu au mali ya watu wengine au kutoridhika na vitu ambavyo anamiliki. Vilevile, uchoyo wa Kerubo unaweza ukaletwa na hali yake ya kuwa mbinafsi bila kuwajali wengine.

2.7.7 Sitiari Changamano

Sitiari changamano ni sitiari inayojidhihirisha tunapotumia sitiari zaidi ya moja kuelezea jambo katika sentensi. Wamitila (2008:425) asema sitiari changamano hupatikana tu pale tunapokuwa na sitiari kadhaa. Anaendelea kutoa kauli yake kuwa sitiari sahili hutumiwa kama msingi wa sitiari nyingine. Wamitila aidha anasema kuwa, uchangamano wa sitiari hii huwa inajidhihirika kutokana na kuwepo kwa vilinganishi vingi mno vya kilinganishwa kile kile kimoja. Kwa maoni yetu, sitiari changamano ni sitiari iliyotumia sitiari nyingi kwa pamoja kama anavyodai Wamitila (khj). Wanjiru (2014:35) anatoa mfano huu kwa kutumia neno mvua katika sentensi hii “Mvua iliyonyesha baada ya mapigano makali na wakoloni haikuleta mvua ya amani rohoni mwa wakulima hata baada ya kunyeshewa na mvua hii

wakiwa shambani”. Wanjiru anasema kuwa neno mvua linaweza likalinganishwa na maendeleo, utulivu na mapigano katika sentensi hii.

2.7.8 Sitiari Kuu

Sitiari kuu huwa ni msingi wa kufasiri kazi ya fasihi inayoshughulikiwa kwa vile ni sitiari inayotawala kazi ya kifasihi kutoka mwanzo hadi mwisho. Sitiari hii huwa ni muhimu sana kwa vile huwa inapewa kipau mbele kwa kazi yoyote ile ya kifasihi. Aidha, ni sitiari inayotumiwa kuwasilisha dhamira katika kazi ya kifasihi.

2.7.9 Sitiari ya Kikaida

Sitiari kaida huambatana na utamaduni mahususi. Ni sitiari inayotumiwa katika mazungumzo ya kawaida kwa madhumuni ya kutoa muundo unaostahili wa utamaduni wa kazi ya kifasihi ambayo inahakikiwa. Sitiari kaida hutumiwa na jamii nyingi kote ulimwenguni ili kuelezea dhana mbalimbali. Mfano wa sitiari ya kaida ni “akili ni nywele”, maana yake ni kuwa akili hubeba maarifa mengi yanayoweza kulinganishwa tu na nywele iliyo kichwani mwa binadamu. Mfano wa pili ni “maisha ni kitendawili” inamaanisha kuwa huwezi ukaelewa vile utaishi maisha yako ya hapo baadaye au huwezi ukajipangia maisha kwa vile hujui kama utaishi ama utafariki siku inayofuata. Kwa mfano, katika riwaya ya Wamitila ya *Msimu wa Vipepeo* (2006:1), kifungu cha maneno msimu wa vipepeo ni sitiari iliyotumiwa ili kusimulia hadithi ya wahusika ambao wamefanya maamuzi yanayoathiri mkondo wa maisha yao kwa njia tofauti, kwa kujikuta katika hali ambayo hawaikutarajia, labda kwa sababu ya maamuzi yao yasiyofaa. Aidha, kifungu cha maneno “msimu wa vipepeo” kinaashiria hali ya sitofahamu inayotokea katika maisha ya wanadamu kwa sababu ya wao wenyewe kufanya maamuzi yasiyofaa au yasiyostahili.

2.7.10 Sitiari Hisi Mseto

Sitiari hisi mseto hutekeleza jukumu la kuhamisha hisia ambazo hupatikana kwa kitu kimoja hadi kwa kitu kingine na huleta mchanganyiko wa namna fulani wa hisia na vilevile hisia ambazo zinakanganya kwa kiasi fulani. Kwa mfano, “Ombati ana roho ngumu”. Mfano huu una maana kuwa Ombati ana roho ya chuki, isiyopenda na kuwajali watu. Wa Mutiso (1996:123) anatoa mfano wa sitiari hisimseto wa neno “giza” kwa kusema kuwa neno hili linalinganishwa na uoga, upweke, mashetani, ujinga, kushindwa n.k.

2.7.11 Sitiari ya Usuli

Sitiari ya usuli zinapatikana katika lugha nyingi za ulimwenguni na huwa zinafungamana na utamaduni fulani mahususi. Wamitila (2008:423) anatoa kauli yake kuwa sitiari ya usuli “...ni sitiari inayofungamanishwa na lugha kiasi kwamba wazungumzaji na watumiaji wa lugha hawaangalii tena kama sitiari au hawafikirii tena kama ni sitiari. Naye Wa Mutiso (1996:123) anatoa mifano ya sitiari ya usuli kama vile ‘giza’ na kusema kuwa ni neno ambalo linahusishwa na uoga, kushindwa, msiba, mashetani, wanyama wala watu, uchawi. Mfano wa sitiari ya usuli katika *Utenzi wa Qiyama* ni neno giza linalopatikana katika ubeti wa 262.

2.8 Dhana ya Maswali ya Balagha

Hili ni swali ambalo halihitaji jibu. Leech (1969:184) asema kuwa swali la balagha ni swali lisilokuwa la kawaida kwa vile halihitaji jibu. Anadai kuwa swali la balagha ni swali chanya linaloelekea kulinganishwa na sentensi hasi. Leech vilevile asema kuwa athari ya kidrama ya swali la balagha hutokana na dhana kuwa swali hili linahitaji jibu ila hakuna jibu lolote lililotolewa swali hilo. Aidha, Leech anatoa madai kuwa, huwa ni rahisi sana kuelewa namna ambavyo swali la balagha limetumiwa katika utungo katika uwasilishaji wake wa ujumbe.

Holman (1960) anasema kuwa swali la balagha hutumiwa katika kazi ya kifasihi ili kumchochea msomaji kutafuta jibu na katika mchakato huo msomaji hatakuwa msomaji tu bali atakuwa mshiriki katika uwasilishaji wa ujumbe. Kuhenga (1977:48) anadai kuwa :

Swali la balagha ni msembo wa tashtiti ambao kwayo
mwandishi au mhatibu kwa madhumuni maalumu ya
kuteka fikra za ndani au kuibua maoni ya msomaji
ili atoe kauli ya maana ama aulize swali ambalo
linaweza kuchochea hisia za furaha, majonzi, majuto
au kutenda jambo ambalo linaweza kumsha-
wishi mtu atende jambo fulani zuri au baya.

Kuhenga anaeleza kuwa lengo kuu la swali la balagha ni kuchochea hisia mbalimbali za msomaji wala si kujaribu kupata jibu au kujibu swali hilo. Wamitila (2003:194) adai kuwa ni tamathali ya usemi ya kuuliza maswali yasiyohitaji majibu, kwa vile huenda majibu yake yako wazi kwa wasomaji. Maswali ya balagha yanapotumiwa katika kazi ya fasihi yanatekeleza jukumu la kusisitiza ujumbe au usemi kwa msomaji.

Kwa maoni yetu, tunaweza kusema kuwa swali la balagha linapotumiwa katika kazi ya kifasihi huwa linampatia mhakiki wa kazi hiyo nafasi ya kutafakari zaidi kuhusu ujumbe unaowasilishwa. Kupitia kwayo, mhakiki hupokea ujumbe huo kwa uzito zaidi kwa vile swali hili huchangamsha ubongo wake kwa kuchochea hisia zake kwa vile wakati mwingine halihitaji jibu ama jibu lake liko wazi.

2.9 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia dhana ya takriri, taswira, tashbihi, tashhisi, sitiari na maswali ya balagha. Aidha, tumejadili takriri na taswira huku tukishughulikia aina mbalimbali za takriri na taswira. Baadaye tumeshughulikia tashbihi na sitiari tukijadili aina

mbalimbali za tashbihi na sitiari tukitolea mifano mwafaka kila aina za tashbihi na sitiari hizo. Mwisho tumejadili tashhisi na swali la balagha kwa kutumia mifano maalumu.

SURA YA TATU

3.0 MATUMIZI YA TAKRIRI, TASHBIHI, TASHIHISI, SITIARI NA MASWALI YA BALAGHA KATIKA *UTENZI WA QIYAMA*

3.1 Utangulizi

Katika sura ya pili tumefafanua kwa undani dhana ya takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha. Mbinu hizi tano ni kati ya viambajengo vikuu vya tenzi hasa, *Utenzi wa Qiyama*. Mbinu hizi zimetumiwa pakubwa na msanii katika utenzi huu, ili kujenga taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama. Lengo letu katika sura hii ni kuchanganua na kutathmini mchango wa mbinu hizi katika kujenga au kuleta taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika *Utenzi wa Qiyama*. Tunachunguza kila ubeti ulio na mbinu hizi ili kubainisha mchango wake katika kuleta taswira ya Siku ya Kiyama. Aidha, tumetoa mifano mingi ya kila mbinu ambayo tumeshughulikia na hata tumenukuu baadhi ya beti, ili kuthibitisha na kutilia mkazo ufafanuzi wetu. Baadhi ya mbinu zilizoshughulikiwa katika kila ubeti ni kama zifuatazo.

3.2.0 Takriri

Kama tulivyofafanua katika sura ya pili, Wamitila (2003:221) anatoa kauli yake kuwa takriri ni urudiaji wa kukariri, wa kutokea mara kadha. Mtunzi wa utenzi huu anazungumzia siku ya mwisho ambapo hatima ya kila mtu itabainika. Anazungumzia hali ya watu siku hii ya mwisho. Anazungumzia vile watu watawekwa kwenye mizani na kuhukumiwa. Msanii ametumia takriri nyingi mno katika kujenga taswira inayoonyesha vile Siku hii ya Kiyama itakavyokuwa. Takriri hizi zinatumiwa kuleta hali halisi ya Siku ya Kiyama, baada ya watu wengine kumwasi Muumba wao na wengine kumtii. Katika utafiti huu, tunatumia neno takriri kwa maana ya sauti za lugha, maneno na semi zilizorudiwa katika *Utenzi wa Qiyama*.

Takriri za aina mbalimbali zinapotumiwa na msanii katika kazi huwa zinadhihirisha umahiri wake wa utunzi. Huenda pia mtunzi au msanii akatumia takriri ili kupunguza idadi ya maneno anayoyatumia. Tunaweza kusema kuwa mtunzi hutumia takriri sauti katika kazi yake kwa sababu ya kukosa maneno ya ziada. *Utenzi wa Qiyama* ni miongoni mwa tenzi ndefu za Kiswahili, kwa hivyo, msomaji anaweza akakosa hamu ya kukamilisha usomaji wake iwapo urudiaji wa sauti za lugha, maneno na semi haujatumiwa. Wakati mwingine mtunzi hutumia takriri ili kusisitiza ujumbe ili usisahaulike na kupitia kwayo picha inajengwa katika akili ya msomaji.

3.2.0 Aina za Takriri

Tunashughulikia aina mbalimbali za takriri na tumeonyesha namna ambavyo takriri hizi zimetumiwa na mtunzi ili kuafikia malengo ya kujenga taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama. Tumeanza kwa kushughulikia takriri irabu au vokali.

3.2.1 Takriri Irabu

Katika utenzi huu, takriri irabu imetumiwa kwa wingi na mtunzi kutoka katika ubeti wa kwanza hadi ubeti wa mwisho. Kwa maoni yetu, matumizi ya takriri irabu katika utenzi huu imemwezesha msanii kujenga picha inayowasilisha Siku ya Kiyama, bila msanii kutumia maneno mengi yanayoweza kusahaulika kwa urahisi sana na msomaji. Mtunzi wa utenzi huu ametumia takriri irabu mwanzoni mwa mishororo kadhaa. Ifuatayo ni mifano inayothibitisha madai hayo.

Akaletewa mizani

Akahukumu Manani

Aliketi arishini

Jibrili kamwambiya (ubeti 171)

Mtunzi anatumia silabi **a** mwanzoni mwa mishororo mitatu ili kurejelea nafsi ya tatu umoja. Ujumbe katika ubeti huu unapitishwa kwa kutumia nafsi ya tatu. Ujumbe huu unapopitishwa na msanii, anajenga picha ya mizani itakayotumiwa kupima kiwango cha dhambi ya kila mwanadamu ili ahukumiwe na Manani. Picha hii inaelezea namna ambavyo siku ya mwisho itakuwa siku ya ajabu. Aidha, picha yake Mungu akiketi na kuamrisha malaika Jibrili pia inajengwa. Takriri ya aina hii katika ubeti huu inasisitiza kuwa mambo haya yalisemwa na mtu mmoja. Aidha, idadi ya maneno iliyotumiwa katika kuwasilisha ujumbe na kujenga picha pia inapunguzwa. Njia hii ya urudiaji wa irabu inajenga picha inayowasilisha Siku ya Kiyama kwa urahisi. Picha hii vilevile inaleta taharuki kwa msomaji, ili atake kuendelea kusoma kwa ajili ya kupata picha kamili ya Siku ya Kiyama.

Aidha, kuna baadhi ya beti ambamo mtunzi ametumia silabi katika mishororo miwili ya kwanza pekee. Kwa mfano:

Ameketi kursini
Ametoka arishini
Na nuru yake Manani
Jamii umetangaa (ubeti 147)

Mshairi anatumia irabu **a** katika mshororo wa kwanza na wa pili. Huu ni mtindo mwafaka wa kuondoa uzoefu wa kutumia mtindo mmoja. Mtindo huu humpa msomaji hamu na motisha ya kutaka kuendelea kusoma kazi ya msanii. Mtindo wa kutumia nafsi ya tatu umoja **a** inathibitisha uzoefu wa hali ya juu ya kutumia lugha. Hii ni kwa sababu msanii ameonyesha kipawa chake cha kutumia usimulizi wa nje katika kazi yake. Mshororo huu unatoa picha ya namna ambavyo Mungu anawaamuru watu Siku ya Mwisho ili wahukumiwe. Urudiaji wa

irabu **a** imetumiwa ili kuchora picha ya vile Siku ya Kiyama itakavyokuwa siku ya ajabu kwa wanadamu.

Katika beti nyingi, mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* anatumia silabi **a** ya nafsi ya tatu umoja mwanzoni mwa mishororo ya beti. Mifano ya baadhi ya beti hizi ni kama vile; ubeti wa 168, 170, 199, 232, 250, na wa 265. Hizi ni baadhi ya beti zinazodhihirisha ubingwa wa msanii katika matumizi yake ya lugha. Msanii ameweza kudhihirisha uwezo wake wa lugha kwa kutumia nafsi ya tatu katika utunzi wa *Utenzi wa Qiyama*. Aidha, kupitia urudiaji wa aina hii msanii ameweza kuthibitisha ujenzi wa taswira ambayo inawasilisha Siku ya Kiyama.

Katika *Utenzi wa Qiyama*, takriri irabu pia imetumika mwishoni mwa mshororo. Hata hivyo, haijatumika kwa wingi. Takriri irabu inapotumiwa mwishoni mwa mshororo huleta ridhimu na usawa wa mizani katika kazi hiyo. Tunaweza kusema kuwa mbinu hii inapotumiwa mwishoni mwa mshororo, inadhihirisha kuwa mtunzi anafuata kanuni za kiarudhi zinazosisitizwa na wataalamu mbalimbali kama vile Abedi (1954) anaposema kuwa shairi lisiloweza kuimbika siyo shairi bali ni mkorogo tu wa maneno.

Takriri irabu inapotumika mwishoni mwa mishororo inampa mtunzi uwezo wa kuonyesha ujuzi wake wa lugha. Picha inayowasilisha ujumbe hujitokeza au huchorwa kwa ukamilifu zaidi. Katika *Utenzi wa Qiyama* kuna baadhi ya beti zilizotumia takriri irabu yenye mkeketo sawa mwishoni mwa mshororo wa ubeti wa kwanza. Kwa mfano:

Hapatasaa chuguu

Wala milima mikuu

Wala jabali na tuu

Jamii zitapoteya (ubeti 26).

Katika ubeti huu mshairi anatumia irabu **u** kutoka ubeti wa kwanza hadi wa tatu. Aidha, anatumia vitate yaani maneno yanayotamkwa kwa njia sawa lakini yana maana tofauti mfano guu, kuu na tuu kama mbinu ya kuchora picha inayowasilisha Siku ya Kiyama. Mtunzi anachora picha hii ya siku ya mwisho kwa kusema kuwa hata vitu visivyo na uhai havitakuwa na umuhimu siku hii na vyote vitatambua Siku ya Kiyama. Anasema kuwa hata milima na majabali makubwa yataporomoshwa siku hii ya mwisho. Katika mshororo wa mwisho anathibitisha kuwa watu vilevile hawatawachwa nyuma. Watu wote watapotea ghafla, pindi tu upepo mkali utakapoanza kuvuma. Msanii anatupa picha halisi ya namna ambavyo siku hii itakuwa. Kama milima na majabali yatapotea ni yepi ambayo hayatatendeke wanadamu wa kawaida? Ni siku ya ajabu, ni siku ya huzuni na maangamizo kwa viumbe vyote.

Mfano mwingine wa takriri irabu unaopatikana mwishoni mwa mishororo ni huu:

Nawaliliya ambao
Waloasi Mola wao
Na siku hii ya leo
Ndiyo siku ya kuliya (ubeti 149).

Katika ubeti huu, mshairi anatumia irabu **o** katika mshororo wa kwanza, wa pili na wa tatu. Irabu **o** inatumiwa na msanii ili kuondoa uzoefu wa kutumia silabi moja. Hapa, mshairi anajenga picha ya siku iliyojaa vilio, kelele na maangamizo. Mtunzi aidha, anawarejelea wale watu ambao walimuasi Mungu na anathibitisha namna ambavyo wataangamia na kulia baada ya kutomtii Mungu. Siku hii ni siku ya ajabu sana kwa vile imejaa maangamizo na vilio. Watu watateseka pakubwa. Mshairi anatumia ufundi wake wa lugha hapa ili kutujengea picha halisi ya namna ambavyo mambo yatakavyokuwa. Msanii anajenga siku ya ajabu, siku ambapo watu hawatapumzika. Analeta picha ya siku iliyojaa vilio.

Kwa vile tunachunguza namna ambavyo takriri irabu imetumiwa katika kujenga taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama, tunaweza tukasema kuwa mshairi wa utenzi huu amefaulu kwa kiwango kikubwa kutumia takriri irabu ili kujenga taswira halisi ya siku hii ya masiku, yaani Siku ya Kiyama. Aidha, mshairi amefaulu kutumia takriri irabu mwanzoni mwa mshororo na takriri irabu mwishoni mwa mshororo katika *Utenzi wa Qiyama*.

3.2.2 Takriri Konsonanti

Katika sura ya pili, tulieleza takriri konsonanti kama urudiaji ambapo kwayo sauti za konsonanti ndizo zinazorudiwa. Takriri ya aina hii mara nyingi hujitokeza katika mshororo wa shairi. Katika *Utenzi wa Qiyama* takriri konsonanti imetumika kwa wingi na msanii ili kuleta picha inayowasilisha Siku ya Kiyama. Vilevile, takriri hii imetumiwa kusesitiza kile kinachosemwa. Aidha, mwandishi wa utenzi huu anatumia takriri konsonanti ili kuonyesha ujuzi wake wa lugha na uandishi huku akikamilisha mishororo mbalimbali katika utenzi huu.

Takriri konsonanti inapotumiwa na mtunzi wa kazi ya kifasihi mara nyingi huleta dhana ya kusesitiza jambo. Jambo linaposisitizwa ili lisisahaulike hujenga picha ya kile kinachosisitizwa akilini. Katika *Utenzi wa Qiyama*, takriri konsonanti ya aina mbalimbali imetumika ili kuleta picha ya Siku ya Kiyama. Tunajadili mifano michache kwa lengo la kudhihirisha namna ambavyo takriri konsonanti inachangia ujenzi wa picha ya Siku ya Kiyama. Kwa mfano **Ni laki laki lukuki**.

Sifaze hazioleki

Wala hazimunaiki

Ni laki laki lukuki

Au punde hazidiya (ubeti 8)

Mfano huu wa takriri konsonanti unachukua mshororo mzima kwa vile neno **Ni laki laki lukuki** limechukua mshororo wote wa tatu katika ubeti wa nane.. Takriri hii inarejelea sifa zake Mungu. Mshairi anasema kuwa Mungu ana sifa nyingi zisizoweza kuhesabika. Yaani sifa zake Mungu ni teletele. Mungu ndiye mwenye huruma, baraka, msamaha, kulaani, wivu, kuumba, n.k. Matumizi ya takriri hii inatupa uwezo wa kujaribu kupata picha ya sifa zake Mungu. Sifa zake haziwezi zikalinganishwa na bahari, maji, nambari, mchanga au pengine hata watu. Sifa za Mungu ni zaidi ya milioni. Sifa zake Mungu haziwezi zikapigiwa mfano.

Katika mshororo wa pili neno “**Na jingwi jingwi la moto**” linarudiwa katika ubeti wa 134 na na wa 220. Mshororo huu unarudiwa ili kutupa picha kamili ya namna ambavyo siku ya mwisho itakavyokuwa. Picha inayochoreka ni picha ya siku ya ajabu yenye mateso. Katika siku hii kutakuwa na moto na watu watateseka huko motoni. Tunasawiriwa picha ya namna ambavyo watu watahomeka huku wakiangamia siku hii ya mwisho. Siku hii sio siku ya furaha kwa watenda dhambi. Ni siku ya vilio na maangamizo kwa Makafiri wote kwa vile walikosa kufuata sheria za Manani. Aidha, tunachorewa picha iwapo siku hii ni siku ya kuvumiliwa kwa vile kutakuwa na moto na utawateketeza watu.

Katika ubeti wa 220 mtunzi anazidi kuisitiza namna ambavyo watu watahomeka na kuteseka kwenye moto mkubwa utakaowaka Siku hii ya Kiyama. Matumizi ya takriri hii inatupa picha kamili ya wanadamu wakiwa motoni wakichomeka. Mshairi anasema kuwa Siku hii ya Kiyama ni Siku Kuu na itakuwa na shida nyingi pamoja na mateso mazito.

Twaumiya kwa mateto

Na jingwi jingwi la moto

Na silsaya nzito

Hatuwezi kutukuwa (ubeti wa 134)

Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* amefaulu kutumia takriri konsonanti katika kazi yake kwa lengo la kusisitiza ujumbe wa utenzi wake. Aidha, Mtunzi amefaulu kuonyesha ujuzi wake wa lugha na utunzi huku akichora picha ya siku ya mwisho kwa kutumia maneno machache yanayokaririwa akilini.

3.2.3 Takriri Neno

Takriri neno ni uwezo wa mtunzi kurudia maneno katika utungo. Mbinu hii kwa maoni yetu kama tulivyoieleza katika sura ya pili hutumiwa na mwandishi kuchora picha kwa kusisitiza jambo. Takriri ya maneno yametumiwa kwa wingi na mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* ili kujenga picha inayowasilisha Siku ya Kiyama. Mfano wa takiriri neno katika utenzi huu ni kama ifuatayo:

Neno **Taa** limerudiwa katika ubeti wa 32, 179, 222, 237, 243 na wa 244. Neno hili linatumiwa ili kusisitiza kuwa Mungu ndiye mwangaza au nuru. Hili linatupa uwezo wa kuchora picha ya taa akilini na kuitumia kumrejelea Mungu siku ya mwisho. Mungu atakuwa na mwangaza usioweza kuzimwa na mwanadamu wa kawaida ama mtu yeyote yule. Mwangaza wake Mungu ndio utakaotumiwa kumulika dunia. Neno **taa** katika muktadha wa kidini kwa Waislamu na Wakristo lina maana ya kuwa na uwezo wa kusafisha au kuosha. Waislamu wanaamini kuwa ni Mungu pekee ndiye mwenye uwezo wa kuwasafisha Makafiri ili wawe weupe kama theluji. Aidha, Wakristo nao wanaamini kuwa ni Manani pekee aliye na uwezo wa kuosha dhambi ya mwasi. Kwa hivyo, Wakristo au Waislamu ni lazima wamkaribie Mungu huku wakitenda matendo yanayolingana na matakwa yake ndiyo waweze kung'ara kama taa au kama Mola. Mtunzi anapotumia takriri ya mwangaza inatupa uwezo wa kuchora picha ya **taa** tunayomlinganisha nayo Mungu. Aidha, mwangaza wake ni mwangaza wa ajabu usiolinganishwa na mwangaza wowote ule katika ulimwengu mzima. Mwangaza

kutoka kwa Mungu hauwezi kulinganishwa na mwangaza wa mwezi, jua au nyota kwa vile una nuru zaidi. Katika ubeti huu, mtunzi anatupa uwezo wa kupata picha ya mtu ambaye ana mwangaza wa kiajabu.

Akaondoka mtumi

Katamka kwa ulimi

Kamwambiya alahumi

Nakuomba mola **Taa** (ubeti 244)

Aidha, kuna baadhi ya maneno yaliyosheheni kutoka mwanzoni mwa utenzi hadi mwisho. Kwa mfano neno **moto** limetumiwa katika beti zifuatazo: Ubeti wa 12, 121, 129, 134, 187, 189, 190, 200, 204, 265, 220, 199, 266, 284, 289, 225, 226, 229, 230, 293, 294, 231, 295, 296, 297, 299, na wa 330. Katika beti hizi, mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* anasema kuwa wale watu ambao hawafuati sheria za Mungu watachomeka kwa moto Jehanamu. Waislamu wanasisitiza kuwa watu ambao sio wa dini lao ni Makafiri hivyo watapata adhabu ya kuchomeka Jehanamu siku ya mwisho kwa vile mtu yeyote asiyefuata sheria na kanuni za Kiislamu amemuasi Mola.

Aidha, kwa Waislamu na Wakristo, **moto** huu ni mkubwa na utawaka milele Jehanamu. Moto huu utamchoma mtu mmoja kwa miaka milioni huku watu wakichomwa kwa ukali na maumivu tele. Neno hili linatumiwa na msanii ili kutupa picha kamili ya moto tutakaoupata siku ya mwisho. Hivyo, siku hii inaonekana kama Siku Kuu, yaani siku ya maangamizo na hukumu kwa wanadamu wote. Picha halisi ya siku isiyo na starehe inajengeka akilini ili kuleta dhana ya mateso kwa wanadamu.

Neno jingine ambalo limerudiwa ni **Peponi**. Neno hili limetumiwa katika beti zifuatazo: Ubeti wa 225, 257, 271, 265, 276, 258, 298 na wa 303. Peponi ni mahali ambapo watu wasio

na dhambi watakwenda Siku ya Mwisho. Ni mahali pazuri penye raha na ustarehe. Peponi kwa Waislamu ni pahali ambapo wale waliofuata na kutii sheria za Mungu ndio watafaulu kufika. Aidha, kulingana na dini ili ufike Peponi ni lazima ujiepushe na raha na starehe za dunia. Bibilia na Qurani husema kuwa huko Peponi ni kwa wachache kwa vile watu wengi wameshindwa kujiepusha na raha na starehe za duniani. Peponi wanapokwenda waja, watu wote ni sawa kwa vile hakuna mtu hata mmoje ambaye anabaguliwa huko.

Neno hili **Peponi** limetumiwa ili kuleta picha ya pahali ambapo wale ambao walimfuata Mungu na kutii sheria zake watakwenda dunia itakapoisha. Aidha, tunapata picha ya pahali patulivu palipo na furaha, pahali ambapo hakuna mateso na maangamizo siku ya mwisho. Picha ya Peponi inaonekana kama mahali ambapo hakuna njaa kwa vile imejaa vyakula. Ajabu ni kwamba eneo hili limetengewa tu watu wachache sana, ambao walifuata sheria na kukosa kuhadaika na vitu vya duniani kama Waislamu. Peponi ni pahali pazuri ajabu, ambapo hapawezi kulinganishwa na popote pale humu duniani. Mtunzi anapotuelezea kuhusu Peponi, basi tunapata picha ya pahali patulivu penye raha na ustarehe.

Neno **Mola** pia limerudiwa sana na mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama*. Neno hili linatokea katika beti zifuatazo: Ubeti wa 158, 232, 237, 243 na wa 278. Mola ni jina lake Mungu. Waislamu na Wakristo wote wanaamini kuwa Mola ndiye mwenye uwezo, nguvu na uhai. Katika *Utenzi wa Qiyama* ili mtu awe mcha Mungu ni lazima awe Muislamu la sivyo, yeye ni Kafiri atakayeadhibiwa na Mungu siku ya mwisho. Neno hili linapotumika katika utenzi huu linatupa picha halisi ya kiumbe mwenye uwezo tutakayekutana naye siku ya mwisho. Picha ya kiumbe huyu inadhihirishwa akiwa na uwezo, mamlaka na ni yeye tu ndiye atakayeweza kuadhibu wanadamu au hata kuwapatia msamaha. Neno hili vilevile linamaanisha mfalme wa wafalme. Manani atajitokeza siku ya mwisho akiwa ameketi kwenye kiti cha enzi. Watu wote

duniani watakuwa chini ya kiumbe huyu ambaye amerejelewa kama Mola kwenye utungo huu.

Aidha, neno **silisili** limerudiwa katika ubeti wa 209, 214, 217, 136 na wa 138. Ni neno linalotuchorea picha ya Siku ya Kiyama kwa vile watu watafungwa kwa minyororo huku wakipata mateso Jehanamu. Tunapata picha kamili ya namna ambavyo watu watakuwa wamefungwa kwa minyororo na itawatesa kwa kuwazuia kutembea huku wakipimwa kwenye mizani. Siku hii hakuna yule ambaye atapumzika, mateso yatasukumwa na Mwenyezi Mungu kutoka kila upande. Tunapata picha ya namna ambavyo watu watatembea wakifungwa kwa minyororo huku wakilia, wakiteseka na kuangamia. Hili linadhihirisha kuwa Siku hii ya Kiyama ni siku ya maangamizo makubwa.

Wakienda kwa ukali

Ukali wa **silisili**

Na adhabu ni thaqili

Na mayowe kwandelea (ubeti 217)

Aidha, beti zaidi zinazodhihirisha takriri neno katika *Utenzi wa Qiyama* ni: Ubeti wa 113 **ondokeni ondokeni**, ubeti wa 146 **mitilizi mitilizi**, katika ubeti wa 19 na 20, neno **pasi** limerudiwa katika ubeti wa 33.

Maneno haya yote yamerudiwa na mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* ili kuweza kutupa picha kamili ya siku hii ya ajabu. Aidha, taswira inayotokana na matumizi ya maneno haya inatupa shughuli halisi itakayofanyika siku hii ya mwisho.

3.2.4 Takriri Silabi

Takriri silabi imetumiwa kwa wingi katika *Utenzi wa Qiyama*. Hii ni mbinu inayohusu urudiaji wa konsonanti na irabu, kama tulivyoeleza katika sura ya pili. Urudiaji wa aina hii

mara nyingi hujitokeza mwanzoni na mwishoni mwa tenzi mbalimbali kama ilivyo katika *Utenzi wa Qiyama*. Mshairi anaweza akatumia takriri silabi ili kuleta taswira halisi kwa kusisitiza maneno. Mtunzi anaweza kutumia mbinu hii ili kupunguza idadi ya maneno yanayotumiwa katika tungo haswa, tungo ndefu kama vile *Utenzi wa Qiyama*.

Aidha, ni mbinu ambayo inaweza pia kutumiwa na msanii ili kuonyesha umahiri wake wa ubunifu wa kutumia lugha yake na uwezo wake wa kukiuka mazoea ya kawaida katika tungo zake. Takriri silabi inajitokeza kwa wingi sana katika *Utenzi wa Qiyama*. Aidha, mtunzi wa utenzi huu ameweza kutumia takriri silabi za mwanzoni mwa mshororo na za mwishoni mwa mshororo katika utenzi huu ili kuleta picha kamili ya siku ya mwisho. Mfano wa takriri silabi za mwanzoni mwa mshororo ni katika ubeti wa 29.

Katika ubeti huu, mtunzi anatumia nafsi ya tatu wingi **wa** ili kutuelezea namna ambavyo watu waliomuasi Mungu watakavyohangaika siku ya mwisho. Mshairi anasema kuwa watu wote wenye viburi na hata wale waliojigamba duniani wakidhani kuwa wanamiliki dunia wote watachomeka siku ya mwisho bila huruma. Aidha, anatupa picha kamili ya vile watu watakavyoangamia siku hii ya mwisho kwa kuuliza maswali huku akitumia nafsi ya tatu mwanzoni mwa mshororo. Katika ubeti huu, mtunzi anatupatia picha ya vile watu watakavyoangamia bila huruma siku hii ya masiku. Hata wale walio na vyeo na utajiri duniani hawatawachwa nyuma siku ya mwisho. Watu wote watahukumiwa kwa kuzingatia viwango vyao vya dhambi.

Wawapi majababiri

Walo wakitakabari?

Wawapi wenye ziburi

Walo wakee duniya? (ubeti 29)

Kuna beti nyingi zilizotumia aina hii ya takriri silabi ili kujenga picha inayowakilisha Siku ya Kiyama. mifano zaidi ni kama ifuatayo: Ubeti wa 30, 26, 31, 38, 40, 133, 154, 163, 214, 211, 257, 258, 291, 303, 323 na wa 335.

Mshairi anatumia takriri silabi ya mwanzoni mwa mshororo **na** katika kujenga picha inayowasilisha Siku ya Kiyama katika beti zifuatazo. Ubeti wa 173, 216 na wa 221. Katika ubeti wa 216, mshairi anarudia silabi **na** ili kuleta picha halisi ya namna ambavyo watu watateseka siku ya mwisho kwa kurushwa kwa moto ulio na majoka. Vilevile mtunzi anatumia takriri hii ili kutupatia uwezo wa kuchora picha ya nyoka hawa watakaowauma watu siku ya mwisho. Hili ni dhihirisho tosha kuwa siku hii ya mwisho itakuwa siku ya maangamizo.

Wawekwe kwa kusimama

Na kelele za Zahamu

Na majoka kuwauma

Na mayowe kwendeleya

Mifano zaidi ni katika ubeti wa 19 na wa 20 ambapo **pa** linarudiwa na ubeti wa 174 ambapo **a** imerudiwa. Takriri silabi ya mwishoni mwa mshororo inatumika kwa wingi na kwa ufundi mkubwa katika *Utenzi wa Qiyama*. Takriri hii imesheheni kutoka mwanzo hadi mwisho wa utenzi. Baadhi ya silabi zilizotumiwa mwishoni mwa mshororo ni kama vile; **no, li, mu, qi, le, ki, ta, bu, di, to, la, ma, ni, ri, na, ke na ha**.

Takriri silabi hizi zinatumiwa na mtunzi ili kufanikisha ujenzi wa taswira katika uwasilishaji wa Siku ya Kiyama. Hata hivyo, takriri silabi **ni** na **li** zimesheheni katika *Utenzi wa Qiyama* zaidi ya takriri silabi tulizotaja hapo juu. Kupitia kwayo taswira ya hali ya juu inajengwa ili

kuwasilisha Siku ya Kiyama. Msanii wa *Utenzi wa Qiyama* pia anapitisha ujumbe wake wa namna ambavyo watu watahukumiwa siku ya mwisho kupitia kwa takriri silabi ya **ni** na **li**.

Katika ubeti wa 80, takriri silabi **ni** inarudiwarudiwa ili kuleta taswira kamili ya Siku ya Kiyama. Aidha, takriri silabi hii inasisitiza siku hii ya masiku. Matumizi ya takriri silabi **ni** inaleta hali ya kuonekana ya Siku ya Kiyama kama siku ya ajabu. Katika *Utenzi wa Qiyama*, kuna beti nyingi zilizo na takriri silabi **ni** iliyotumiwa na mtunzi ili kuleta picha ya vile Siku hii ya Kiyama itakavyoonekana.

Mtunzi anathibitisha katika ubeti huu vile Mtume Muhamadi atakavyoonekana kuchanganyikiwa baada ya kufufuliwa na Mungu siku ya mwisho. Waislamu wanaamini kuwa Mtume Muhamadi ndiye atakayekuwa mtu wa kwanza kufufuliwa na Mungu ili aende awatete Waislamu siku ya mwisho. Kutokana na maelezo ya ubeti huu, siku hii ya watu kufufuliwa ni siku ya ajabu kwa hivyo hata Mtume ambaye ni mfuasi wa karibu wa Mungu haelewi siku hii.

Hivi leo siku gani?

Hivi leo kuna nini?

Nambiyani nambiyani

Ruhu ipate kutuwa

Mifano zaidi ya takriri silabi **ni** inapatikana katika beti zifuatazo; Ubeti wa 11, 28, 32, 45, 113, 124, 126, 168, 174, 171, 189, 190, 208, 212, 219, 225, 237, 255, 257, 258, 270, 284, 305, 322 na wa 323. Beti hizi zimetumia takriri silabi ya **ni**.

Takriri silabi ya mwisho **li** pia imetumiwa na mtunzi katika beti nyingi ili kuleta picha ya Siku ya Kiyama. Katika ubeti wa 79, takriri silabi **li** inatumia na mshairi ili kuleta picha kamili ya vile dunia itakavyoonekana katika siku hii ya mwisho. Picha inayochoreka ni ya

dunia tupu isiyokuwa na kitu chochote siku ya mwisho. Siku hii dunia itabaki ikiwa tambarare na hata milima mikubwa itapotea na hakutakuwa na kitu chochote duniani. Tumechorewa picha ya dunia isiyokuwa na uhai wala thamani siku ya mwisho. Dunia itakayoonekana siku hii ni dunia isiyotamanika na mtu yeyote yule.

Haoni kitu dalili

Nti wala majabali

Kamuuzi Jibrili

Mbona i hivi duniya?

Mifano zaidi ya takriri silabi **li** katika *Utenzi wa Qiyama* ni; Ubeti wa 16, 39, 42, 48, 50, 53, 72, 90, 107, 112, 120, 138, 155, 157, 173, 175, 186, 209, 214, 217, 264, 265, 266, 326, 334 na wa 338.

Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* amefaulu katika kutumia takriri irabu, takriri konsonanti, takriri neno na takriri silabi katika utenzi huu. Mbinu hii ya takriri imemwezesha msanii kuonyesha ujuzi wake wa lugha kwa kutumia maneno machache kuwasilisha ujumbe katika utenzi wake. Kukaririwa kwa maneno mbalimbali kumeleta mvuto kwa kazi ya mtunzi. Aidha, sauti, semi, vifungu na maneno mbalimbali ambayo yamerudiwa yameleta picha ya siku ya mwisho akilini. Ujumbe wa hukumu kwa Makafiri pia umepitishwa kwa msomaji kwa kutumia mbinu ya takriri katika *Utenzi wa Qiyama*.

3.3 Tashbihi

Kama tulivyoona katika sura ya pili, Kuhenga (1977:15) anasema tashbihi ni mbinu ya kulinganisha kitu kimoja au zaidi na kitu kingine au vitu vingine tofauti. Aidha, vilinganishi kama vile “ja”, “mithili ya”, “mfano wa”, “kama”, “sawa na”, n.k huwa vinatumiwa katika kulinganisha vitu. *Utenzi wa Qiyama* unadhihirisha matumizi mengi ya tashbihi

inayodhihirisha ujenzi wa picha ya Siku ya Kiyama. Tunachunguza namna ambavyo mtunzi ametumia tashbihi wazi, tashbihi fiche na tashbihi ya kiutendi katika kujenga picha ya Siku ya Kiyama. Mbinu hii imetumiwa na mshairi kwa wingi katika beti mbalimbali. Tumeshughulikia tashbihi hizi kwa kuzingatia vilinganishi ili kuzijadili kwa uwazi zaidi.

3.3.1 Tashbihi za Wakati

Kilinganishi **wakati** kinatumiwa kuundia tashbihi katika ubeti wa 126. Wakati ni majira au muda wa kutendeka kwa jambo. Tashbihi ya aina hii ni tashbihi wazi, kwa vile inalinganisha maisha ya mwanadamu ya siku ya mwisho na ile ya zamani. Mungu ndiye anazungumza na wanadamu katika ubeti huu. Mungu anasema kuwa atawarejeshea wanadamu wote hali yao ya zamani ili wale waliotenda dhambi wahukumiwe. Katika ubeti huu, mtunzi anatupatia picha ya namna ambavyo watu waliofariki zamani na kubakia mifupa watakavyofufuliwa na kupewa uhai tena ili wawe vile walivyokuwa kabla ya kufa. Ujenzi wa picha hii na mtunzi inatufanulia kuwa Siku ya Mwisho, kila mwanadamu atakuwa katika hali yake ya awali ya vile alivyokuwa akiishi duniani. Picha tunayopata ni ile ya kila mwanadamu kuwa na uhai siku ya mwisho hata wale ambao walifariki. Kila mtu atafufuka na kuhukumiwa akiwa hai siku ya mwisho.

Tawatiya muilini

Kwa nguvu zake Manani

Kama vivile zamani

Kwa shida zikarejeya

3.3.2 Tashbihi za Moto

Tashbihi inayotumia kilinganishi cha **moto** inatumika katika ubeti wa 137 wa *Utenzi wa Qiyama*. Mshairi anawalinganisha watu na kuni na makaa katika ubeti huu. Siku ya Mwisho

watu watachomeka kama vile kuni na makaa huchomeka. Makafiri ambao ni Wakristo watachomeka Jehanamu kama kuni na makaa kwa sababu ya kukataa kufuata njia za Mungu. Waislamu kwa upande mwingine watakuwa Peponi kwa vile watakuwa washindi. Tashbihi hii inaibua hisia za uoga na huruma kwa wasomaji. Tunapata picha kamili ya watu wakilinganishwa na kuni na makaa siku ya mwisho. Siku hii wanadamu hawatahurumiwa katu. Ni siku ambapo wanadamu wote hawatakuwa na thamani tena. Aidha, huu ni mfano wa tashbihi wazi.

Ni kama kunwa na kowa
Libasi ukainuwa
Kula atakaotowa
Amali njema ajaa

3.3.3 Tashbihi za Mimea na Wingu

Kilinganishi mimea na wingu kimetumiwa kama tashbihi katika ubeti wa 140 wa *Utenzi wa Qiyama*. Wakristo na Waislamu wote wanaamini kuwa siku ya mwisho watu watafufuliwa na Manani. Siku ya Mwisho baada ya tarumbeta kupulizwa, watu watafufuka kama mimea na wingu. Matumizi ya tashbihi hii inatupa taswira ya watu wengi watakaofufuliwa na Mungu mara moja Siku ya Mwisho. Ni taswira inayotupatia picha ya kuona mimea na wingu ikilinganishwa na wanadamu. Siku ya Mwisho watu watatoka makaburini kama vile mimea inavyotoka baada ya mbegu kupandwa. Watu watatoka kwa wingi kama vile mawingu yanavyokusanyika wakati mvua inapokaribia kunyeshwa. Taswira inayokuja akilini ni picha ya watu wengi wanaofufuliwa na kuhukumiwa na Mungu. Picha ya dunia tupu kujaa watu kwa ghafla siku ya mwisho pia inasawiriwa katika tashbihi hii. Katika mfano huu tashbihi ya mimea na wingu ni tashbihi wazi.

Wakatoka walimwengu

Kama mimea na wingu
Naye Mtumwa wa Mungu
Aliketi changaliya

3.3.4 Tashbihi za Mwangaza

Katika utenzi huu, dhana ya tashbihi za mwangaza tunatumia kurejelea vifaa au vitu vinavyolinganishwa na mwangaza katika ubeti mbalimbali.

3.3.4.1 Taa

Taa ni chombo kinachowashwa na kutoa mwangaza ili kumulika. **Taa** ni mfano wa tashbihi wazi. Waislamu ndio wanaorejelewa kama taa katika *Utenzi wa Qiyama* ili kuonyesha kuwa wao ni mashujaa na washindi huku Wakristo wakionekana kama Makafiri na viumbe dhafu. Siku ya mwisho itakapofika, ni Waislamu pekee yao watakaong'ara Peponi kwa vile wanaamini kuwa ni wao ndio wanaofuata kanuni na sheria za Mungu huku Wakristo (Makafiri) wakionekana kama viumbe wenye dhambi na adhabu yao ni kuchomeka Jehanamu. Siku ya mwisho watendaji wema wanalinganishwa na taa. Mtunzi anatuchorea picha ya watendaji wema kung'ara kama taa Siku ya Kiyama. Watenda wema watakuwa na nuru au mwangaza ya ajabu usioweza kwisha. Watu wenye nuru ya taa ambao ni Waislamu ndio watakaokwenda Peponi. Hivyo, mshairi anatuchorea picha ya washindi waking'ara kama mwangaza huku wenye dhambi wakiteseka motoni wakiwa wanaonekana kama giza.

Rabbi atawahasibu
Jamii wenye dhunubu
Asaze wenye thawabu
Wenye nuru kama Taa (ubeti 179)

3.3.4.2 Badiri

Katika ubeti wa 181, Waislamu wanazidi kulinganishwa na mwezi au **badiri** ili kuonyesha kuwa wao ni safi kuliko Wakristo. Mshairi anatuchorea picha ya mwezi hasa Waislamu ambao ndio watenda wema wanapolinganishwa na mwezi. Mshairi anasema kuwa siku hii ya mwisho kwa kuwa ni siku ya ajabu, watenda wema watakuwa na nuru kama ya mwezi wafikapo Peponi. Watenda wema watang'ara na nuru yao itaweza kulinganishwa na ile ya mwezi. Hivyo, tunapata picha ya mwangaza wa mwezi utakayong'ara kwa watenda wema. Hii ni nuru isiyoweza kulinganishwa na nuru inayopatikana pahali popote pale duniani. Ni nuru itakayoonekana siku ya mwisho pekee. Aidha, kilinganishi hiki ni tashbihi wazi.

Mtenda zena dahari
Rabii atampa nuru
Awe kama ya Badiri
Itakapo kujiriya

3.3.5 Tashbihi za Nywele za Wanyama na ndege

Nywele za wanyama na ndege zimetumika katika ubeti wa 249 wa *Utenzi wa Qiyama* ili kuelezea mateso watakaopata Makafiri Jehanamu huku Waislamu wakifurahia Peponi. Katika mfano huu, tunapata picha halisi ya majoka au nyoka wakubwa watakaokuwa kwenye moto Siku ya Kiyama. Aidha, urefu wa nyoka hawa unalinganishwa na urefu wa unywele laini unaopatikana katika mwili wa ndege au mnyama. Matumizi ya tashbihi hii inachangia katika kuleta hisia za hofu kwa wasomaji wa *Utenzi wa Qiyama*. Mtunzi analeta picha ya nyoka wakubwa sana ambao hawajawahi kuonekana watakaowauma watu ifikapo siku hii ya mwisho wa ulimwengu. Ni siku ya masikitiko kwa watenda dhambi na furaha kwa watenda wema. Tashbihi hii ya nywele za wanyama na ndege ni tashbihi wazi.

Hiyo swiratwi maarufu

Nyaka thalatha alifu
Mapana ndiyo dhaifu
Kama unyee mmoja

3.3.6 Tashbihi za Umeme

Tashbihi ya **umeme** katika ubeti wa 251 wa *Utenzi wa Qiyama* ni tashbihi wazi. Matumizi ya tashbihi hii inaleta picha ya namna ambavyo watu watapita swiratwi kwa kasi huku wenye dhambi wakianguka chini kutoka kwa daraja hilo. Tunapata picha ya njia nyembamba kama sindano inayopitwa na waja wote siku ya mwisho. Watu wenye dhambi watakuwa waoga wa kuvuka daraja hilo. Ni daraja ambalo watu ambao hawajatenda dhambi ndio wataweza kuvuka. Kulingana na *Utenzi wa Qiyama*, ni Waislamu pekee yao ndio wanaorejelewa kama washindi hivyo, watapita daraja hili kwa kasi wakienda Peponi. Wakristo (Makafiri) nao hawataweza kupita daraja hili kwa sababu ya dhambi waliotenda. Watendaji dhambi watakapojaribu kupita wataogopa na kutumbukia shimoni. Aidha, mshairi anatupa picha ya namna ambavyo watu watapita daraja la swiratwi kwa kasi mno. Haraka ya kuvuka daraja hili unalinganishwa na mwendo wa umeme kwa sababu ni mwendo wa haraka mno siku ya mwisho.

Na ndiya hiyo khatwari
Na ghadhabu za Jabari
Watapita wenye kheri
Kama umeme kumeya

Aidha, katika ubeti wa 252 na wa 263 mtunzi amezitumia ili kutupatia picha ya kuona vile daraja hili ilivyo vigumu kupita. Mtunzi ametumia tashbihi “Kama umeme kumeta” na “Kama umeme kupita” ili kuthibitisha kuwa watu watapita daraja hili kwa kasi sana. Watu watakaoweza kupita daraja hili ndio watakaoandaliwa sherehe ya kukata na shoka kwa vile

wao ndio washindi. Beti hizi vilevile zinaleta picha ya kuthibitisha kuwa siku hii ya mwisho ndiyo Siku Kuu. Mambo yatakayojitokeza siku hii pia ni mambo ambayo hayajawahi kutukia ulimwenguni. Tashbihi hizi ni tashbihi wazi na zinathibitisha madai ya Waislamu kuwa wao ndio wateule huku Wakristo wakiwa Makafiri ambao hawatapewa nafasi ya kufika Peponi.

3.3.7 Tashbihi za Wanyama

Kilinganishi **ng'ombe** kimetumiwa katika ubeti wa 267 wa *Utenzi wa Qiyama* kuundia tashbihi. **Ng'ombe** kama tulivyofafanua katika sura ya pili ni mnyama anayejulikana kwa ujinga na uzembe wake. Mnyama huyu ametumiwa na msanii ili kuwarejelea Wakristo kama watu wazembe na wajinga. Aidha, Waislamu wanarejelewa kama wenye hekima na maarifa. Katika mfano huu, mshairi anamlinganisha mwanadamu aliyemwasi Mungu ambaye ni Mkristo na ng'ombe. Mkristo anapolinganishwa na ng'ombe inatupatia picha ya mnyama aliye na sifa ya; Ujinga, uzembe, unene, mkono birika, aliyelaaniwa, mtu anayefanya matendo yanayokasirisha, anayefanya kazi kwa njia dhaifu au asiyewajibika na kwa hivyo kusababisha kuteseka kwake kupitia kwa matendo yake. Mfano huu wa tashbihi ni fiche na unatupatia picha halisi ya vile Wakristo (Makafiri) watakavyoteseka siku hiyo ya mwisho. Hii ni kwa sababu Waislamu wanaamini kuwa Wakristo ndio waliokataa kufuata kanuni na pia walikosa kutenda kulingana na matakwa yake Mungu.

Munani enyi ziumbe
Mulokaa kama ng'ombe
Musina kumeye pembe?
Wakajibu wote piya

3.3.8 Tashbihi za Hali

Katika tashbihi hii, tunatumia hali ili kurejelea vile kitu, mtu ama jambo lilivyo. Tashbihi hali katika *Utenzi wa Qiyama* ni kama vile **dhaifu** na **Yusufu**.

3.3.8.1 Dhaifu

Tashbihi inayotumiwa kama kilinganishi cha hali fulani inapatikana katika ubeti wa 316. Katika masimulizi ya ubeti huu, mshairi anaeleza msimamo wake kuhusu Wakristo anaposema kuwa tabia za wakristo ni mbovu kwa vile tabia zao hazifanani na zile za mababu zao kwa kutumia maneno **si kama nyinyi dhaifu**. Aidha, mshairi anaeleza kuwa ni tabia za Waislamu pekee ndizo zinazoweza kulinganishwa na zile za mababu kwa sababu wanafuata sheria zote za kidini. Hisia na msimamo wa mtunzi ni kuwa Wakristo hawana adabu na heshima. Hata akili zao sio timamu kama akili za Waislamu.

Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* anazidi kulinganisha tabia za wanadamu na zile za mababu zao katika ubeti huu. Mshairi anachora taswira ya watu wawili tofauti kabisa. Mshairi anabainisha tabia za watu wa kale na zile za watu wa kisasa. Aidha, mshairi anasisitiza kuwa watu wa kale watakwenda Peponi kwa sababu ya matendo yao mema. Msanii ametumia tashbihi hii ili kuleta picha ya watu wabaya waliomwasi Mungu. Aidha, anachora picha ya watu waliokosa maadili. Watu hawa ndio watachomeka Jehanamu. Watu wasio na tabia kama zile za Ibrahimu na Yakobo watapata adhabu kali. Mshairi vilevile anasisitiza kuwa watu hawa wasio na tabia njema mahali pao ni motoni wala sio Peponi.

Picha inayojengeka kutokana na tabia za babu zetu ni picha ya watu walionyenyeeke, watu waliomtii Mungu na vilevile waliomwamini sana Manani. Aidha, anathibitisha ukweli huu kwa kusema kuwa viumbe wa sasa ni viumbe dhaifu sana kwa vile wamepotea njia. Picha ya watu ambao watachomeka Jehanamu inatokea na inaonekana wazi kuwa Jehanamu ndiyo pahali pa watu wabaya wasiostahili kuhurumiwa. Siku hii ya mwisho ndiyo siku ambayo hatima ya kila mtu itabainishwa na adhabu kutolewa kulingana na matendo ya kila mja.

Babu zetu waongofu

Wali sura takatifu
Si kama nyinyi dhaifu
Watu msiolekea

3.3.8.2 Yusufu

Katika ubeti wa 321, kilinganishi cha **kama sura za Yusufu** na **Rabi Latifu** imetumiwa kama kilinganishi cha hali ili kudhihirisha hali inayopatikana katika ubeti huu wa *Utenzi wa Qiyama*. Katika mfano huu wa tashbihi, msanii anazidi kutoa msimamo wake wa kuwaona Wakristo kama watu waliodhaifu wakilinganishwa na Waislamu. Msanii anasema kuwa nyuso za Waislamu wakiwa Peponi zinang'ara kama nyuso za Yusufu na Rabi Latifa ambao ni Mitume ya Mungu. Aidha, nyuso za Wakristo zimejaa simanzi na huzuni Jehanamu kwa vile walikosa kutenda kulingana na matarajio ya Mungu. Katika ubeti huu, mtunzi anatusawiria picha kamili ya walio motoni na wale walio Peponi. Mshairi anasema kwamba watu walio Jehanamu hali yao imedhoofika sana ilhali wale walioenda Peponi nyuso zao zinang'ara kama uso wa Yusufu. Mshairi anatumbea picha nzuri ya waja waliofaulu kufika Peponi Siku ya Kiyama.

Aidha, anasisitiza kuwa watu walio Jehanamu wanalia sana huku wakiomba maji ya kutuliza kiu. Watu walio Peponi tunachorewa picha zao kama watakaokuwa na afya tele na miili iliyo na nyama laini. Vilevile miili yao imejaa nuru inayong'ara kama mwangaza wa taa.

Sura ngema maarufu
Kama sura za Yusufu
Na tena Rabi Latifu
Ameandika wajaa

Tumeshughulikia matumizi ya tashbihi katika ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika *Utenzi wa Qiyama*. Tumeainisha tashbihi zinazojitokeza katika utenzi huu

kulingana na vilinganishi vinavyounda tashbihi hizo. Vilinganishi hivi ni kama vile; wakati, moto, mimea na wingu, mwangaza, wanyama na ndege, umeme na hali. Tashbihi hizi zimetumiwa kulingana na maudhui na dhamira ya kidini ya Siku ya Kiyama. Uteuzi wa mtunzi wa lugha umeonyesha matumizi ya hali ya juu ya lugha yake katika kuchora picha ya Siku ya Kiyama. Aidha, tashbihi wazi na fiche zimetumiwa katika utenzi huu. Tashbihi zilizotumiwa na msanii zimechangia pakubwa katika ujenzi wa picha ya Siku ya Kiyama. Wakristo wamesawiriwa kama viumbe dhaifu huku Wislamu wakipewa sifa za ushujaa kwa kutumia tashbihi mbalimbali. Msanii amefanya hivi ili kusifu dini ya Kiislamu huku akidharau dini ya Kikristo.

3.4 Tashihisi

Kama wasemavyo Kuhenga (1977:15) na Njogu na Chimera (1999:91), tashihisi ni mbinu inayotumiwa na msanii kupatia vitu visivyo na uhai sifa na tabia za viumbe vyenye uhai. Tunachunguza vile mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* ametumia mbinu hii ili kujenga picha inayowasilisha Siku ya Kiyama. Mtunzi wa utenzi huu amefaulu kutumia tashihisi nyingi za aina mbalimbali katika kazi hii.

3.4.1 Tashihisi za Upepo

Tashihisi ya **upepo** imetumiwa na mtunzi katika ubeti wa 22 wa *Utenzi wa Qiyama*. Katika ubeti huu, upepo unapewa sifa ya kuwa na uwezo wa kuvunja miguu na milima. Miguu ya wale ambao walikataa kumtii Mungu itavunywa Siku ya Mwisho na upepo. Wakristo ambao wanarejelewa na Waislamu kama Makafiri ndio watakaopokea mateso ya kuvunjwa miguu na upepo. Aidha, Wakristo (Makafiri) hawa pia wanarejelewa kama milima kwa vile walimwasi Mungu. Kwa upande mwingine Waislamu watabebwa kwa farasi huku Wakristo (Makafiri) wakipokea mateso.

Mshairi anatuchorea picha ya upepo mkali ambao haujawahi kushuhudiwa. Upepo huu umepewa sifa ya kibinadamu ya kuwa na mikono na miguu inayoweza kushika na kuvunja watu pamoja na mlima. Mfano huu unatupa picha ya siku ya ajabu ambapo hata upepo usio na uwezo wa kutenda utakuwa na nguvu za kuwaadhibu wanadamu na viumbe wengine siku ya mwisho. Kabla ya upepo kuwavunja wanadamu na milima, upepo umepewa sifa ya kufuata amri za Mungu katika ubeti wa 21. Katika ubeti huu, mtunzi anatuchorea picha ya upepo ulio na viungo vyote vya mwili ikiwemo akili, kichwa na miguu inayoweza kufuata maagizo na kutenda kulingana na maagizo ya Mungu. Huu ni mfano unaoleta hali ya kutisha.

Na pepo hiyo ni kuu
Itavundavunda guu
Na milima ilo yuu
Na majabali jamiya (ubeti 22)

3.4.2 Tashihisi za Nchi

Katika ubeti wa 65, tashbihi ya **nchi** imetumika ili kubainisha hali ya Waislamu na Wakristi siku ya mwisho. Mshairi anasema kuwa Waislamu ndio watakuwa wa kwanza kufufuliwa huku kiongozi wao Mtume akifufuliwa wa kwanza ili awatetee. Wakristo nao watakuwa wa mwisho kufufuliwa na hawatakuwa na mtetezi yeyote hivyo watakwenda Jehanamu. Huu ni mfano unaoonyesha kuwa msanii amependelea dini ya Kiislamu zaidi kuliko dini ya Kikristo. Katika mfano huu, mtunzi anatuchorea picha ya nchi iliyo na uhai. Picha ya nchi inayozungumza na mwanadamu. Siku hii ni siku ya ajabu. Ni siku ambayo hata malaika Jibrili atachanganyikiwa atakapotumwa na Mungu kutafuta kaburi la Mtume. Jibrili ataelekezwa na dunia kwa kaburi la Mtume. Picha ya dunia kupata uhai siku ya mwisho ni picha ya kutisha na kuogofya.

Tashihisi ya neno **nchi** imetumiwa katika ubeti wa 93, 114 na wa 115. Mtunzi ametumia tashihisi ya **nchi** kutoa majibu kwa kutetemeka itakapoulizwa maswali ili kuonyesha kuwa hata nchi itakuwa ikitambua Waislamu kama wafuasi wa Mola. Wakristo hawatatambuliwa na **nchi** kwa vile wao ndio watu wajinga wanaompinga Mungu. Hii ndio sababu wamerejelewa kama Ng'ombe.

Aidha, katika ubeti wa 93, 114 na wa 115, **nchi** imepewa sifa ya kibinadamu ya kutoa majibu ikiwa imekasirika kwa kutetemeka ili kutusawiria picha halisi ya siku ya mwisho. Matumizi ya picha hii, inaleta hali ya kuogofya inayojidhihirisha dunia itakapotoa jibu ikiwa imekasirika. Iwapo dunia ina uwezo wa kukasirika siku ya mwisho na kujibu Jibrili kwa mtetemeko, je wanadamu wa kawaida waliomwasi Mungu watakwenda wapi na watafanya nini? Picha ya dunia ikinena na ikikasirika inasawiriwa wazi katika mfano huu. Mathalani, katika ubeti wa 114 na wa 115 **nchi** imepewa sifa ya kibinadamu ya kutetemeka wakati ambapo Makafiri wanapofufuliwa baada ya Waislamu wote kutetewa na Mtume na kwenda Peponi. Matumizi ya tashihisi hii inaleta picha haswa ya vile dunia itakavyokuwa Siku ya Kiyama. Picha ya wanadamu kufufuka wakati ambapo nchi itakapotetemeka siku ya masiku imedhihirishwa na msanii.

Jibrili katuliya
Na nti ikamwambiya
Qaburi yake Nabiya
Nami imenipoteya (ubeti 65)

Akisa nena Mmaka
Nti ikatetemeka
Masahaba wakatoka
Na tumwa
wakamuendeya (ubeti 93)

3.4.3 Tashihisi za Kaburi

Neno **kaburi** limetumiwa ili kuleta tashihisi ya kuogofya katika ubeti wa 70. Katika ubeti huu, mshairi anasisitiza na kusawiri picha kamili ya kuogofya. Picha hii inadhihirishwa kaburi la Mtume linapokuwa na uwezo wa kutoa nuru. Ni siku ya ajabu kwa kuwa siku zote kaburi huwa na giza, lakini siku ya mwisho kaburi litatoa nuru itakayoashiria alipozikwa Nabii. Masimulizi ya mtunzi katika ubeti huu, vilevile yanatuchorea picha ya dunia isiyokuwa ya kawaida Siku ya Mwisho kwa kuwa ni Waislamu ndio wanapewa hadhi ya juu kwa vile watafufuka wakiwa wa kwanza huku Makafiri wakifufuliwa wa mwisho kwa sababu wao ndio viumbe dhaifu na pia wenye ujinga huku Waislamu wakionekana watiifu na washindi.

Mshairi aidha, anaendelea kuleta picha kamili ya Siku ya Kiyama katika ubeti wa 76 anapothibitisha namna ambavyo kaburi litakapopasuka kivyake ili Mtume aende Peponi kwa sababu yeye ndiye atawaongoza Waislamu ambao ndio Washindi. Mshairi anasisitiza hali ya kaburi kupasuka katika ubeti wa 89. Waislamu ambao ndio wafuasi kamili wa Mungu makaburi yao yatajifungua wa kwanza dunia itakapoisha. Picha nyingine inayojengeka ni picha ya Mtume kutoka kaburini akiwa hai na kuketi baada ya kufufuka. Kaburi kupewa uwezo wa kujifungua inaleta picha ya namna ambavyo siku ya mwisho itakavyokuwa. Katika ubeti huu, mtunzi anasimulia kuwa baada ya Mtume kutoka katika kaburi lake, umati mkubwa utafuata baada ya makaburi yao kupasuka. Aidha, makaburi ya Wakristo (Makafiri) yatapasuka baada ya Mtume kwenda Peponi na wafuasi wake.

Baada hayo pulika
Qaburi ikapasuka
Muhamadi akatoka
Qaburini akakaa (ubeti 76)

3.4.4 Tashihisi za Wanyama

Katika ubeti wa 96, 98, 99, 100 na wa 103 farasi wa Mtume kwa jina Buraqi ametumika katika kuunda tashihisi katika *Utenzi wa Qiyama*. Katika beti hizi, Waislamu wamepandishwa hadhi kwa kupewa farasi ambaye atakuwa akiwabeba hadi Peponi baada ya Mtume kufika. Farasi huyu atawabeba Waislamu pekee yao huku Wakristo wakiwachwa kutembea. Msanii anaonyesha msimamo wake kwa dini ya Kiislamu huku akidharau dini ya Kikristo. Mtunzi anathibitisha kuwa Waislamu ndio watu wanaofaa huku Wakristo wakionekana kama watu wasiostahili. Hiyo ndiyo sababu Waislamu wanabebwa na farasi baada ya kufufuliwa huku Wakristo wakiwachwa ili waendeleo kuteseka. Katika beti hizi, farasi wa Mtume kwa jina Buraqi anaamrisha apandwe na Mtume Muhamadi lakini farasi anakataa. Farasi anataka atolewe ahadi na Mtume kuwa atamtetea mbele zake Mwenyezi Mungu kwanza kabla akubali kumsafirisha Mtume hadi Peponi.

Katika ubeti wa 63 mtunzi analeta picha ya **farasi** kupewa sifa ya kujitetea na kukataa kufuata amri ya malaika Jibrili. Ni jambo la kusikitisha kuwa hata mnyama ataogopa kuhukumiwa kama wanadamu. Farasi huyu atakubali tu kupandwa iwapo atatetewa na Mtume. Tashihisi hii inaleta picha ya siku ya mwisho, ambapo watu wote na vitu vyote duniani vitahukumiwa. Hata wanyama wasioweza kuzungumza wanaogopa siku hiyo. Wanyama hawa kwa mfano farasi wa Mtume atakubali kupandwa na Mtume iwapo atamuahidi kumtetea wakati wa hukumu.

Katika ubeti 103, mtunzi anatusimulia kuhusu jambo lisilo la kawaida linalotokea. **Farasi** anapewa sifa ya kuwa na ujasiri wa kusimama mbele ya Mtume na kumsihi amtetea asipelekwe Jehanamu. Farasi anapopewa uwezo wa kujitetea, inadhihirisha kuwa ana maarifa zaidi hata kuliko Wakristo (Makafiri) ambao hawawezi kujitetea wanapokaribia

kuhukumiwa. Tunajenga picha ya mazungumzo haya yanayoendelea kati ya Mtume na farasi wake Buraqi. Katika ubeti huu, mtunzi ametusawiria picha kamili ya vile siku ya mwisho itakavyokuwa. Siku hii ni siku ya maangamizi na mateso. Picha ya siku hii inadhihirika hasa ikiwa hata wanyama kama farasi watakuwa na uwezo wa kuzungumza kama wanadamu wakiwasihi wanaowamiliki kuwatetea ili wasamehewe.

Basi Tumwa amrile
Farasi amrukile
Kumpanda Mteule
Yule nyama kakataa (ubeti 96)

Yule Buraqi kajibu
Songea unikaribu
Nisafi sina dhunubu
Nitekese yangu niya (ubeti 103)

3.4.5 Tashihisi za Njia

Katika ubeti wa 262, mtunzi ametumia tashihisi **njia** ili kudhihisha mateso watakayopata Wakristo watakapojaribu kuenda Peponi tofauti na Waislamu watakaopanda farasi na kujiepusha na mateso haya. Mfano huu unaonyesha mapendeleo wanaopewa Waislamu tofauti na Wakristo. Aidha, kwa vile msanii anaamini kuwa Mkiristo ni mjinga basi hataweza kujua njia ya kwenda Peponi badala yake atachagua njia inayomwelekeza Jehanamu. Katika mfano huu, njia ya kuenda Jehanamu imepewa sifa ya kibinadamu ya kuwachanganya watu. Njia hii aidha ina vijia. Vijia hivi kwa vile ni vingi vimepewa sifa ya kuwakanganya waja watakojaribu kufika Peponi. Mshairi ameipatia njia sifa ya kuwa na akili na fikra ili kutuletea picha ya namna ambavyo Wakristo ni wajinga. Hali ni tofauti kwa Waislamu kwa vile wataweza kutambua njia ya kwenda Peponi mara moja. Hii inaleta picha inayodhihirisha

vile watu watateseka siku ya mwisho. Hata njia ya kuenda Peponi hawataweza kuitambua Wakristo kwa sababu watakuwa wanateseka na kuangamia.

Na ndiya hiyo ni kiza

Tena itawapoteza

Pateleza pateleza

Hali iliyvo kukaa

3.4.6 Tashihisi za Moto

Mtunzi ametumia tashihisi ya **moto** katika ubeti wa 121. Katika ubeti huu, mtunzi anatusimulia kuwa Wakristo (Makafiri) watachomeka katika moto kule Jehanamu. Aidha, moto huu utawachoma Wakristo pekee kwa kuwa Waislamu wote watatetewa na kwenda Peponi siku ya mwisho. Katika *Utenzi wa Qiyama* mtunzi anatushauri kuwa ni vyema kuwa Muislamu kwa sababu hiyo ndiyo njia ya kipekee ya kujiepusha na mateso ya Jehanamu. Waislamu wanasawiriwa kama watu wenye hadhi ya juu kuliko Wakristo.

Moto unapewa sifa ya kibinadamu ya kuwachoma Makafiri bila huruma. Tunapata picha ya moto mkubwa unaowaka bila kuisha. Aidha, tashihisi hii inatumiwa na mtunzi ili kutuletea taswira ya joto. Tunazidi kupata picha ya siku hii kama siku ya kuteseka kwa mwanadamu kwa vile shughuli kuu itakayofanywa na Mungu pamoja na malaika wake ni ya kuwaadhibu wanadamu wenye dhambi kwa kuwatupa motoni.

Katika ubeti wa 126, 127 na wa 128 **moto** unapewa sifa ya kunena zaidi na wanadamu pamoja na Mungu. Mtunzi anatumia tashihisi ya moto ili kuleta picha ya siku ya mwisho ambayo Wakristo watachomeka bila huruma. Mtunzi anasimulia vile moto unatolewa amri na Mungu na moto huo unajibu kwa kuwachoma wanadamu. Hii inaleta picha ya namna ambavyo moto utakavyowaadhibu wanadamu bila huruma na kwa ghadhabu kubwa. Wenye

dhambi wote watateseka pakubwa Jehanamu huku wakichomeka motoni huku wakiliwa na majoka. Picha tunayopata ni picha ya hatari ya kutisha. Jambo hili linasisitizwa zaidi na mtunzi katika ubeti wa 128. Tashihisi hii imetumiwa kuchora picha ya moto wenye ghadhabu ili kuwatisha Makafiri. Vilevile tunachorewa picha ya moto utakaowaka kwa fujo na kishindo. Picha hii imeletwa na hali ya moto kupewa sifa ya labda kulia au kuzungumza kwa sauti ya juu wakati utakapowachoma Makafiri. Moto huu utawaadhibu Makafiri bila huruma na kuwatafuna bila huruma.

Mshairi anatoa picha ya vile **moto** utakavyowatesa Makafiri siku ya mwisho katika ubeti wa 231 kwa kusema kuwa moto utatoka na ukali. Mshairi anasema kuwa moto huu utakuwa na miguu na utawaendea wale ambao walikataa kumtii Mungu. Katika ubeti wa 297, picha ya vile wanadamu watakavyoteseka siku ya mwisho imesawiriwa mshairi anapopatia moto sifa ya kibinadamu ya kuweza kutafuna na kula watu bila huruma. Mshairi analeta picha ya Siku ya Kiyama kwa kusema kuwa wanadamu ambao ni Makafiri wataliwa na moto huku wakiona. Aidha, anasema kuwa wakati **moto** utakapowatafuna wanadamu, watatafunwa wakiwa wanaona ila hawatakuwa na uwezo wa kuzuia moto huo. Kauli hii ina maana kuwa wanadamu watachomeka bila huruma kwa moto wenye ghadhabu. Ni kauli ambayo imetumiwa na msanii ili kutuchorea picha ya kuona vile watu watateseka motoni bila huruma.

Zile ruhu za mateto
Ambazo kwamba nda moto
Zikajibu kwa uzito
Kumjibu Mola Taa (ubeti 121)

Wakasimikwa wakema

Ukingoni mwa kisima
Basi moto ukavuma
Kwa kelele na zawiya (ubeti 128)

;

Moto ukiwatafuna
Wali mato wakiona
Ndimi zao wakinena
Qauli wakitongowa (ubeti 297)

Tumejadili tashihisi na mchango wake katika ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama. Mtunzi ametumia ujuzi wa hali ya juu katika kubuni mbinu ya tashihisi. Aidha, msanii hajatumia lugha yake kiholele katika kuwapatia vitu mbalimbali uhai. Mshairi amefaulu kuhaiisha vitu mbalimbali ili vionekane kama viumbe watendaji. Vitu hivi ni pamoja na; upepo, nchi, kaburi, wanyama, njia na moto. Tashihisi katika *Utenzi wa Qiyama* imetumiwa ili kuendeleza maudhui na dhamira ya dini ya Kiislamu. Wakristo wameonekana kama viumbe dhaifu wanaoadhibiwa na Mungu kwa sababu ni wajinga na wazembe. Matumizi ya mbinu ya tashihisi katika utenzi huu pia inadhihirisha uwezo wa mtunzi wa kuelewa na kutumia lugha yake kwa ufasaha huku akizingatia ubunifu wa hali ya juu. Mtunzi ametumia mbinu hii ili kujenga taswira ya kuona, taswira ya joto, taswira ya mwendo na taswira ya usikivu.

3.5 SITIARI

Sitari ni ulinganishi usiokuwa wa moja kwa moja kama tulivyojadili katika sura ya pili. Sitari ni mbinu inayolinganisha vitu viwili au kitu kimoja na kingine bila ya kutumia viunganishi kama vile “ja”, “kama”, “kama vile”, n.k. Sitari ambazo zinajitokeza katika *Utenzi wa Qiyama* zimetumia vilinganishi mbalimbali kama vile wanyama, hali, vitu vya kiasili au kimaumbile na vifaa.

3.5.1 Sitiari za Vitu vya Kimaumbile au Kiasili

Katika *Utenzi wa Qiyama* vitu vinavyotumiwa kama vilinganishi vya kimaumbile ni kama vile **wadudi**, **kusi**, **kuu**, **tufani** na **giza**. Vilinganishi hivi vinatumiwa na mtunzi ili kuleta sitiari za usuli. Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* anasimulia kuhusu mateso yanayowapata Makafiri siku ya mwisho. Katika ubeti wa 22 sitiari **kuu** inatumiwa ili kulinganisha upepo unaovuma Siku ya Kiyama na kitu kikubwa kilicho na uwezo wa kukatakata vitu. Upepo huu utawaangamiza Makafiri siku ya mwisho. Kutokana na hali hii tunapata picha ya upepo uliyo na uwezo wa kuvunja vitu kwa nguvu siku ya mwisho. Kwa vile upepo utakaovuma utakuwa mkubwa mno basi imetupatia picha ya dunia isiyokalika. Picha ya dunia itakayotawaliwa na upepo mkubwa na mkali inachorwa.

Na pepo hiyo ni kuu
Itavundavunda guu
Na milima ilo yuu
Na majabali jamiya

Katika ubeti wa 23, upepo mkali utakaowatesa Wakristo baada ya wao kufufuliwa unalinganishwa na **wadudi**. Mshairi anaeleza hali ya kuonekana ya Wakristo (Makafiri) kuteseka wakiwa wanasubiri kuhukumiwa. Masimulizi haya yanaeleza kuwa ni vyema kuwa Muislamu ili kujiepusha na mateso ya siku ya mwisho. Upepo huu aidha, unalinganishwa na **kusi** katika ubeti wa 24 na utawavunja na kuwatesa Makafiri. Picha hii inazidi kutokea katika ubeti wa 24 mtunzi anapolinganisha upepo utakayovuma Siku ya Kiyama na **kusi**.

Kusi ni upepo mkali wenye baridi, unaopatikana barani Afrika hasa Afrika Mashariki na huwa unavuma katika mwezi wa Aprili hadi Oktoba. Tunasawiriwa picha ya upepo mkali unaoleta maradhi hatari kwa wanadamu. Upepo huu utakaovuma Siku ya Kiyama ni upepo hatari usio na huruma kwa wanadamu na hata kwa viumbe wasiokuwa na uhai. Picha ya

upepo unaoporomosha kila kitu inachorwa. Upepo huu ndio utakaotawala dunia nzima. Matumizi ya sitiari hii inaleta picha ya siku ya ajabu sana katika maisha ya mwanadamu.

Sitiari **tufani** imetumiwa katika ubeti wa 27 ili kudhihirisha mateso, matatizo na shida wanazopata Makafiri siku ya hukumu inapowadia. Upepo huu utaweza kulinganishwa na dhoruba au kimbunga. Upepo huu ni upepo wa ajabu. Ni upepo utakaohangaisha Makafiri na kuwauwa. Upepo wa siku ya mwisho unapolinganishwa na tufani unaleta picha ya siku iliyojaa ghadhabu.

Sitiari **giza** imetumika katika ubeti wa 262 wa *Utenzi wa Qiyama* ili kusawiri picha ya njia yenye mateso na mahangaiko itakayofuatwa na watendaji dhambi. Masimulizi katika ubeti huu yanadhihirisha kuwa Wakristo (Makafiri) watafuata njia ya mateso yenye giza kwa vile hawataweza kufahamu na kutambua njia ya kwenda Peponi kama Waislamu kwa sababu wao ni wajinga. Njia hii vilevile ya kwenda Jehanamu inadhihirisha mateso na ghadhabu itakayowapata waasi wa Mungu siku ya mwisho. Picha ya watendaji dhambi kutoona wanapoenda wala wanapotoka siku ya mwisho imechoreka ili kuthibitisha vile siku ya mwisho itakavyokuwa na mahangaiko. Aidha, **giza** usimamia kitu kisichofaa, laana, mazingaumbe, kitu kisichokuwa na mwelekeo na pia inasimamia kitu kilicholaaniwa kama asemavyo Wa Mutiso (1996:123). Picha ya barabara yenye mateso itakayofuatwa na wenye dhambi siku ya mwisho inadhihirika.

Na ndiya hiyo ni kiza
Tena itawapoteza
Pateleza pateleza
Hali ilivo kukaa

3.5.2 Sitiari za Wanyama

Sitiari nyani imetumiwa katika ubeti wa 28 wa *Utenzi wa Qiyama*. Sitiari ya nyani ni mfano wa sitiari sahili. Sitiari nyani inatumiwa ili kuwajenga wahusika ambao ni Wakristo katika utenzi huu. Mnyama huyu anatumia ili kuwarejelea Wakristo kama watu wasiokuwa na msimamo na siku yao ya kuteleza hivyo basi imewadia. Wakristo hawawezi wakalinganishwa na Waislamu kwa vile Waislamu ni watu wanaofuata njia za Mungu na matokeo ya matendo yao ni kwenda Peponi kwa raha ya milele huku Wakristo wakiadhibiwa na Mungu Jehanamu.

Mshairi anatumia picha ya mnyama mkubwa mwenye rangi ya kijivu. Siku ya mwisho inalinganishwa na nyani ili kutuchorea picha ya siku yenye mambo makuu yasiyoepukika. Vilevile mshairi anathibitisha au ameleta picha ya siku isiyo ya kawaida katika maisha ya mwanadamu. Mtunzi ametumia nyani ili kuleta picha ya siku yenye **giza** ambayo mambo hayatakuwa mepesi. Picha ya mnyama huyu inakuja akilini ili kuleta taswira ya namna ambavyo mambo yatakuwa kwa kuwa huyu mnyama nyani hapendwi na wengi. Nyani aidha, hupata chakula na makao kwa shida na maangaiko.

Tena Rabi akaghani
Aliyuu angani
Siku ya yeo ni nyani
Mwenye Enzi na wilaya?

3.5.3 Sitiari za Vifaa

Kifaa **taa** kimetumiwa katika *Utenzi wa Qiyama* kama kilinganishi katika ubeti wa 158. Picha ya Mungu ya kuwa na uwezo wa kipekee imesawiriwa na mtunzi anapomrejelea Mungu kama “**Taa**” katika ubeti huu. Mungu anarejelewa na mshairi kama taa ili kuonyesha uwezo wake juu ya Waislamu na Wakristo. Mungu ndiye ameweza kuwapatia Waislamu hekima na kuwanyima Makafiri ndio sababu Makafiri wanaonekana kama wajinga. Uwezo

wa Mungu ni mkubwa kwa kuwa amewapatia Waislamu wote kibali cha kwenda Peponi huku akiwaadhibu Makafiri.

Matumizi ya sitiari hii ya **taa** inaleta picha ya Mungu kama mwenye uwezo wa kumwokoia mwanadamu siku ya mwisho. Aidha, matumizi ya sitiari hii yanaleta picha ya Mungu kama mwenye uwezo na nguvu ya kipekee ya kuwatawala viumbe vyote siku ya mwisho. Hivyo, picha ya kila jambo litakalotendeka kusubiri maamuzi na maagizo ya Mungu inajengwa.

Endelipi muhamadi

Nalomwatiya idadi?

Jibrili karadidi

Kamjibu Mola Taa

Mathalani, sitiari ya Mola Taa imetumika pakubwa. Mungu amerejelewa kama **taa** katika ubeti wa 179, 237, 243, 244 na wa 263 katika *Utenzi wa Qiyama*.

3.5.4 Sitiari za Hali

Katika *Utenzi wa Qiyama* tunatumia neno hali kurejelea jinsi mtu, kitu au hali ilivyo. Sitiari za hali zinaonyesha hali fulani na mfano ni katika ubeti wa 182. Katika ubeti huu, watenda wema ambao ni Waislamu wanarejelewa kama **wemawe**. Aidha, msimulizi anasisitiza kuwa ni hawa watenda wema pekee ndio watateuliwa na Mola kwenda Peponi. Wakristo nao wanaonekana kama watenda dhambi na wote watachomeka Jehanamu. Masimulizi haya yanadhihirisha furaha kwa Waislamu na huzuni kwa Wakristo. Ili mtu ajiepushe na ghadhabu za moto kule Jehanamu basi ni lazima akubali kusilimu.

Katika ubeti huu, mtunzi vilevile anamlinganisha mwenye kutenda mema siku ya mwisho na kitu kizuri na thabiti. Tunapata picha ya kitu imara kinachowarejelea Waislamu watakaoteuliwa kwenda Peponi na Mungu. Vilevile picha ya watu hawa inatokea wakiwa na

urembo na uzuri wa aina yake siku hii. Katika siku hii, picha ya watu imara na thabiti inasawiriwa na inaleta tofauti kati ya Waislamu na wale Wakristo wadhaifu ambao walikataa kufuata ahadi zake Mungu pamoja na kanuni zake.

Mwenye wema ni wemawe
Mwenye owe ni owewe
Ndiyo siku ya teuwe
Rabbi takapo teuwa

Katika ubeti wa 329, msimulizi anatumia sitiari ya **karimu** ili kudhihirisha vile Mungu anavyowapenda Waislamu kiasi kwamba hadi anawasalimia. Hata hivyo, hatima ya Wakristo haijulikani kwa vile wao ndio wanaoteseka motoni kule Jehanamu huku Waislamu wakiketi pamoja na Mungu Peponi. Katika mfano huu, Mungu amelinganishwa na ukarimu. Aidha, katika mfano huu, mtunzi anatupatia picha ya Mungu kama mtu mwenye upole na utu kwa Waislamu. Sitiari hii vilevile inaleta picha ya Mungu kama mtu atakayewahurumia na kuwajali watu wake siku hii ya mwisho upepo mkali utakapovuma na kuwahangaisha Makafiri wote duniani. Mungu anaporejlewa kama mpole inajenga picha ya kiumbe asiyeweza kuwahangaisha watu wake siku ya mwisho.

Atasema mualimu
Nimetumwa ni karimu
Jamii awasalimu
Nyote awasalimia

Sitiari **kupana** imetumiwa na msanii katika ubeti wa 330 ili kujenga picha ya Siku ya Kiyama. Mshairi analinganisha radhi au kusamehewa na kitu kisichokuwa na kipimo. Anasema kuwa kusamehewa na Mungu kwa wanadamu ni rahisi na haina kipimo. Makafiri wote wanashauriwa kuingia katika dini ya Kiislamu ili waweze kusamehewa dhambi zao kama vile Waislamu wamesamehewa. Mshairi anaamini kuwa dini ya Kiislamu ndiyo dini

iliyo na tiketi ya kwenda Peponi. Picha inayojitokeza ni kuwa Mungu kila siku huwasameha waja wake bila kuwapimia kiwango. Picha ya kujaribu kufikiria kitu kisicho na kipimo kinakuja akilini. Aidha, matumizi ya sitiari hii inaleta picha inayodhihirisha ukarimu wa Mungu kwa Makafiri siku ya mwisho.

Mathalani, sitiari hii inadhihirisha kuwa Wakristo wakimtii Mungu na kumwomba msamaha basi wataweza kujiepusha na kuhangaika siku ya mwisho. Wakristo wataweza kusherehekea kwa pamoja na Waislamu iwapo watamwomba Mungu msamaha kabla ya siku ya mwisho. Aidha, njia ya kipekee ya kusamehewa na Mungu ni kupitia kwa dini ya Kiisalmu. Hivyo, ni lazima Makafiri wote waweze kukubali kusilimu. Picha ya Mungu kuwa na uwezo mkubwa wa kuwia mwanadamu radhi bila kuchoka siku ya mwisho inadhihirika katika sitiari hii. Aidha, ni kutokana na msamaha huu na matendo mema ndio chanzo cha mwanadamu kwenda Peponi siku ya mwisho.

Nayo radhi ni kupana
Wake wenu na vijana
Naye msimkasiri
Takasani zenu nia

Tumeshughulikia matumizi ya sitiari katika *Utenzi wa Qiyama* na kubainisha vile sitiari hizo zinachangia katika ujenzi wa taswira ya kuona, taswira ya mwendo, taswira ya usikivu na taswira ya joto inayowasilisha Siku ya Kiyama. Tumegundua kuwa mtunzi amefaulu kutumia sitiari za aina mbalimbali katika kazi yake. Sitiari hizi ni pamoja na; sitiari sahili, sitiari za usuli na sitiari mseto. Mshairi amefaulu kutumia sitiari hizi katika kazi yake ili kuafikia malengo yake ya utunzi. Aidha, mshairi ametumia vilinganishi kadhaa ili kuundia sitiari. Katika kazi hii, tumevigawa vilinganishi hivi vya sitiari katika makundi manne: Sitiari za vitu vya kimaumbile, sitiari za wanyama, sitiari za vifaa na sitiari za hali. Mbinu hizi nne za sitiari

zimetumiwa kuonyesha tofauti zilizopo kati ya dini ya Kiislamu na dini ya Kikristo. Dini ya Kiislamu imesifiwa sana na mtunzi huku dini ya Kikristo ikidharauliwa. Vilevile tumegundua kuwa mshairi ameonyesha msimamo na mtazamo wake kwa kupendelea dini ya Kiislamu huku akijitenga na dini ya Kikristo kwa kuonyesha udhaifu ya Wakristo.

3.6 MASWALI YA BALAGHA

Katika sura ya pili, tulieleza swali la balagha kama swali lisilohitaji jibu ama swali ambalo jibu lake liko wazi kama asemavyo Leech (1969:184). Mtunzi wa shairi hutumia mbinu hii ili kuwashirikisha wasomaji wake katika kutoa suluhu kwa jambo fulani analolizungumzia. Aidha, mara nyingi mbinu hii inapotumiwa katika kazi humwezesha msomaji kutafakari zaidi kuhusu kile kinachozungumziwa. Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* hajawachwa nyuma katika kutumia mbinu ya maswali ya balagha katika kazi yake. Tumechunguza namna ambavyo mshairi ametumia mbinu hii ili kujenga taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama.

Mtunzi ametumia mbinu hii katika ubeti wa 28, 29, 30, 31 na wa 36. Katika beti hizi mshairi anasawiri picha ya siku ya ajabu itakayowameza viongozi Makafiri. Mtunzi anasimulia kuwa uongozi wa Kafiri hautambuliwi na Mungu kwa sababu ni haramu. Ubeti huu unaeleza kuwa uongozi unaotambuliwa na kukubaliwa na Manani ni ule wa Kiislamu. Iwapo mwanadamu anataka kujiepusha na maaangamizi basi ni sharti ajiunge na dini ya Kiislamu na kufuata sheria zake. Anachora picha ya watawala wa duniani kupotea na kutoonekana tena. Katika ubeti wa 29, picha ya watu wakuu waliojipiga kifua wakidhani dunia ni yao imechorwa. Ajabu ni kuwa, watu hawa watapotea mara moja pindi tu siku ya mwisho itakapowadia kwa sababu ya matendo yao maovu.

Wawapi majababari

Walo wakitakabari?

Wawapi wenye ziburi
Walo wake duniya?

Mtunzi anasimulia katika ubeti wa 30 wa *Utenzi wa Qiyama* kuhusu masaibu na maangamizi yatakayowapata viongozi wa Makafiri. Masimulizi ya ubeti huu yanasema kuwa hakuna kiongozi yeyote wa Makafiri atakayehurumiwa na Mungu. Ni kheri mwanadamu aongozwe na Waislamu wala sio Makafiri kwa sababu uongozi wa Kiislamu ndio uongozi ambao umetoka kwa Mungu. Aidha, uongozi wa Kikristo ni uongozi wa kijinga na unawaelekeza watu Jehanamu.

Katika ubeti huu, picha ya watu mashuhuri duniani waliomwasi Mungu inachorwa. Picha hii inaonyesha vile viongozi wakuu duniani watakavyobaki wakiangamia bila huruma. Aidha, mshairi anachora picha ya dunia isiyokuwa na thamani kwa wanadamu wote. Picha ya siku ya mwisho vilevile inatokea mwanadamu atakapoangamia au atakapohukumiwa na Mungu bila kujali cheo chake. Kwa mfano katika ubeti wa 31, mshairi anaulizia walipo wale Makafiri waliojifanya wajanja na kumuasi Mungu. Vilevile anaulizia walipo wale viumbe waliojipiga vifua na kujiona mashuhuri. Picha ya wanadamu wote kuwa sawa mbele yake Mwenyezi Mungu inachorwa.

Aidha, picha ya mali ya mwanadamu duniani kutokuwa na umuhimu wowote siku ya mwisho inasawiriwa. Mshairi anasema kuwa Wakristo (Makafiri) walijishughulisha na kutafuta mali ya duniani wakidhani itawaokoa huku wakimsahau Mungu wao. Siku hii ya mwisho ni Siku Kuu na wanadamu wote watahukumiwa kulingana na matendo yao wala sio kulingana na mali wanazomiliki au vyeo vyao vya dunia. Waislamu pekee ndio watu watakaotetewa na Mtume hivyo wote watakwenda Peponi Wakristo wakibaki Jehanamu.

Wawapi masultwani

Walikuwa madiwani
Wakamba ulimwenguni
Ndisi watu afudhwaa? (ubeti 30)

Wakristo wanarejelewa kama laana katika ubeti wa 37. Makafiri hawa wanaulizwa na Mungu wanapotorokea. Mtunzi anasimulia kuwa Mungu aliwapatia Wakristo (Makafiri) chakula na vitu vyote walivyohitaji wakiwa duniani lakini kwa sababu ya ujinga yao walimsahau Mungu na kukosa kumwabudu kama wenzao Waislamu. Makafiri wanaonekana kama watu wajinga wasiokuwa na akili timamu. Aidha, ujinga huu ndio unasababisha kuangamia kwao. Mshairi katika ubeti huu ametumia swali la balagha ili kujenga picha ya waasi wakijaribu kumtorokea Mungu siku ya mwisho kwa sababu wanaogopa kuadhibiwa kwa matendo yao maovu. Picha ya Mungu inasawiriwa akizungumza na watu walio mbioni wakimtoroka.

Katika ubeti wa 38, msanii anauliza hawa watu waliomtoroka Mungu na kuabudu sanamu wanakwenda wapi? Katika mfano huu, mtunzi anataelezea ujinga ya Makafiri unaowasababisha kuhadaika kwa urahisi na kumsahau Mungu. Mshairi anasisitiza kuwa Wakristo ambao ndio Makafiri walisahau kumfuata Mungu na kufuata sanamu huku wakiabudu wanadamu wenzao.

Mshairi katika mfano huu vilevile analeta picha ya Mungu anapofananishwa na mzungu na Makafiri. Picha ya Mungu akimwadhibu mwanadamu kwa sababu amemwasi na kuabudu mzungu inasawiriwa na mshairi. Siku hii ni siku ambayo kila mtu ataadhibiwa na kuhukumiwa kutokana na matendo yake.

Wendeepi makhaluqi
Nalokiwapa riziqi
Mimi wasiniswadiqi
Wakiabudu johaa (ubeti 37)

Aidha, mshairi anasisitiza umuhimu wa dini ya Kiislamu anapodhihirisha kwenye masimulizi yake kuwa Mungu pamoja na malaika watakuwa na haja na kaburi la Mtume na wafuasi wake huku Wakristo (Makafiri) wakisahaulika. Katika ubeti huu, msanii anaeleza kuwa Mtume ndiye atakuwa wa kwanza kufufuliwa na Mungu pamoja na wafuasi wake. Wakristo nao watafufuliwa wa mwisho.

Katika ubeti huu picha ya malaika Jibrili akitafuta kaburi la Mtume duniani siku ya mwisho inachorwa. Picha hii inadhihirisha ama inaonyesha vile Jibrili atakavyoshuka mbio duniani na kuuliza umma kaburi la Mtume ili amfufue aende awatete Waislamu. Aidha, picha ya watu waliochanganyikiwa na kusahau kaburi la Mtume pia inasawiriwa. Baada ya Jibrili kuulizia kaburi la Mtume picha ya kaburi lenye nuru linaonekana. Tumepata picha ya kuona kaburi lenye nuru teletele. Haya yote ni matukio yanayodhihirisha na kutoa picha ya vile siku ya mwisho itakavyokuwa.

Kwamba yake Mukhtari
Muhamadi Mdathiri
Iwapi yake qaburi
Nti imenipoteya? (ubeti 64)

Mshairi anaelezea vile malaika Jibrili anawalilia Makafiri waliokosa kufuata njia zake Mola katika ubeti wa 72, 73, 74 na wa75 za *Utenzi wa Qiyama*. Jibrili anaonekana akiwa na huruma tele kwa vile Wakristo walijifanya wajinga na kupotoka kufuata sheria zake Mungu. Adhabu wanaopata Makafiri Jehanamu ni makubwa na machungu. Katika mfano huu, Jibrili anaulizwa na malaika Israfilu kwa nini analia. Picha ya malaika Jibrili akiwalilia wanadamu inachorwa. Picha hii inaonyesha huruma ya malaika Jibrili kwa wanadamu watakaohukumiwa kwa vile adhabu watakayopata siku hii ni kubwa mno.

Jibrili kamjibu
Kwani sili muhibu?
Atokeyapo Habibu
Aniuzapo Nabiya (ubeti 74)

Katika ubeti wa 80, mshairi anatusawiria picha ya siku hii ya ajabu ambayo haieleweki hata Mtume Muhamadi. Picha ya kuonekana ya kuchanganyikiwa kwa Mtume inachorwa hasa anapouliza Jibrili baada ya kufufuliwa kwake kuhusu siku. Mtume katika ubeti huu anaomba malaika wamwelezee kuhusu siku ya leo ndio aweze kwenda kwa Mungu ili awatete Waislamu. Hali hii inaleta picha ya Siku Kuu. Katika ubeti wa 85, Mtume anaulizia walipo wafuasi wake kwa vile hamwoni hata mmoja. Mtume baada ya kufufuliwa anaonekana akijishughulisha na kuwaokoa wafuasi wake ambao ni Waislamu. Aidha, haulizi kuhusu walipo Wakristo kwa sababu Wakristo wanaonekana kama Makafiri. Katika mfano huu, mtunzi anatumia picha ya siku isiyojulikana kwa wanadamu.

Hivi leo siku gani?
Hivi leo kuna nini?
Nambiyani nambiyani
Ruhu ipate kutuwa (ubeti 80)

Swali la balagha aidha limetumika katika ubeti wa 92 na wa 143 wa *Utenzi wa Qiyama*. Picha ya siku hii ya ajabu vilevile inasawiriwa Mtume anapoendelea kumuuliza jibrili kuhusu walipo wafuasi wake na marafiki wake aliowajua duniani kama vile Abubakari na nduguye Umari, Athmani na Aliya. Mtume anawaulizia watu hawa kwa vile ni wao ndio wanaaminika kutii na kufuata sheria za Mungu. Mtume hashughuliki na Wakristo kwa sababu wanaonekana kama Makafiri na laana.

Katika beti hizi, picha ya siku ambayo watu watapoteanwa inachorwa. Picha ya siku ambayo ndugu, marafiki na wafuasi hawajulikani walipo. Watu hawa hawajulikani walipo kwa sababu watakuwa wametengana wakisubiri hukumu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Picha ya siku ambayo ndugu na marafiki waliopendana watakosa kuungana pamoja inasawiriwa.

Akauza Mukhtari
Uwapi Abubakari
Na ndugu yake Umari
Athmani na Aliya? (ubeti 92)

Katika ubeti wa 243 na wa 157 malaika Jibrili anaonekana kuwahurumia Makafiri wanaochomeka Jehanamu kwa sababu ni wengi sana. Makafiri hawa wako Jehanamu kwa sababu walikuwa wajeuri wakiwa duniani na hata Mtume hataki kuwatetea kwa vile jukumu lake ni kuwatetea Waislamu. Picha ya Jibrili akiwaonea wanadamu huruma inachorwa katika mfano huu anapoulizwa na Mtume ni nini kimetokea ndiyo awalilie wanadamu. Mbinu hii ya maswali ya balagha katika mfano huu imetumiwa na mtunzi kuchora picha ya Siku ya Kiyama kama siku ambayo waja wote hawatahurumiwa na Mungu na kila mtu atahukumiwa kulingana na matendo yake duniani.

Akamba Tumwa
Amini
Jibrili unanni?
Kiliyo waliliyani
Likulizalo nambiya (ubeti 143)

Mshairi ametumia mbinu ya maswali ya balagha katika ubeti wa 189 ili kuchora picha ya huzuni ya siku ya mwisho atakapouliza akiwa karibu na moto kuna nini? Kutokana na swali hili la balagha picha ya watu wakichomeka motoni inachorwa. Siku hii ni siku ambayo watu wataadhibiwa kwa kuchomwa motoni na Mwenyezi Mungu na wale watakaotenda wema

pekee yao ndio watakaoepuka kuangamia. Makafiri wote watachomeka huku Waislamu wakijumuika pamoja na kufurahia Peponi.

Yule malaika motoni
Akauza kuna n'ni?
Hakuona na huzini
Jibrili kamwambiya

Mathalani, katika ubeti wa 190, mtunzi anadhihirisha matumizi ya swali la balagha Jibrili atakapomjibu mwenzake halii ni vile anawahurumia wanadamu Makafiri kwa kuwa ametumwa na Mungu ili ahakikishe kuwa watu wamejaa motoni. Katika ubeti huu, picha ya watu wengi wakijaa motoni wakichomeka inachorwa. Picha ya Jibrili akiwahurumia Makafiri pia inasawiriwa katika mfano huu.

Jibrili kwa yaqini
Malaka sili kwani?
Nimetumwa na Manani
Ufanye moto ajaa

Aidha, katika ubeti wa 192 wa *Utenzi wa Qiyama*, picha ya siku hii ya ajabu inachorwa na mtunzi wakati ambapo hata malaika wenyewe watakuwa wakiuliza maswali kwa kuwa wataona siku ya ajabu iliyo na giza isiyokuwa kama siku zingine. Katika mfano huu, mshairi anatuchorea picha ya siku ya mwisho kama siku ambayo itakuwa na giza. Ni siku ambayo waja hawataona mwangaza. Aidha, picha ya malaika wakiwa wamechanganyikiwa pia inachorwa na msanii. Ni siku ambayo itawachanganya wananchi na hata malaika wenyewe. Kwa mfano, katika ubeti wa 197, swali la balagha limetumiwa ili kuchora picha ya namna ambavyo malaika watakavyokuwa wamechanganyikiwa siku hiyo watakapoulizia alipo Mtume Bashiri na umati wake kwa vile hata wao hawataelewa walipo watu.

Vivyo hivyo ndivyo mambo yalivyo katika ubeti wa 264 picha ya wanadamu wakiwa wamechanganyikiwa siku ya mwisho inatokea wanapouliza Mungu njia ya kupitia kwa vile wanaona njia mbili na hawataweza kubainisha ni gani inawafaa. Aidha, kutokana na matumizi ya swali hili, tunapata picha ya umati mkubwa na picha ya njia mbili za kufuatwa siku ya mwisho. Picha hii inadhihirika watu wanaposubiri kuelekezwa kwa sababu wamekwama.

Yule malaka kauza
Ewe mwenzangu neleze
Yeo mbona kuna kiza?
Jibrili kamwambiya (ubeti 192)

Katika ubeti wa 266 na wa 267, mshairi ametumia swali la balagha kutuchorea picha ya namna ambavyo Makafiri watakwenda Jehanamu wakionekana wakiwa na majuto. Picha ya Makafiri wenye huzuni na njaa inachorwa kutokana na mfano huu. Hii inadhihirisha kuwa watakaoenda Jehanamu watakuwa na mwili utakaokuwa dhaifu na vilevile watakosa furaha kwa sababu ya mahangaiko ya Jehanamu. Picha ya mabawabu wanao wauliza Makafiri swali wao ni akina nani inasawiriwa. Matumizi ya swali hili pia linachora picha ya mabawabu wakionekana wakiwakejeli waasi kwa kuwa wanaelewa kuwa wanasubiri kutiwa kwenye moto kwa vile wakiwa duniani walikuwa na kiburi na kumsahau Mungu. Aidha, picha ya umati mkubwa utakaosubiri kuchomwa motoni inatokea katika beti hizi.

Katika ubeti wa 267, picha ya waliomuasi Mungu inachorwa wakiwa wanalinganishwa na ng'ombe wanapoulizwa wanaenda wapi wao waasi walio na pembe na kuwa wajinga kama ng'ombe. Katika ubeti huu, Wakristo (Makafiri) ndio wanaorejelewa kama ng'ombe kwa vile walikataa kumwabudu Mungu badala yake walimwabudu sanamu kwa sababu wao ni wajinga. Aidha, Wakristo wanarejelewa kama Ng'ombe kwa vile wakiwa duniani walikuwa

watumwa wa mzungu na kuonea fahari sanamu na vitu vinavyoletwa na wazungu hao huku wakimsahau Mola wao.

Wale bawabu motoni
Kauza m-watu gani?
Hamna nuru usoni
Wala ulimi safi ya (ubeti 266)

Munani enyi ziumbe
Mulokaa kama ng'ombe
Musina kumeya pembe?
Wakajibu wote piya (ubeti 267)

Picha ya Wakristo kulinganishwa na ng'ombe inawarejelea kama wajinga na waasi . Mathalani, picha hii inajitokeza zaidi katika ubeti wa 270 na wa 271 Makafiri wanapoelezewa kuwa wako motoni kwa vile hawajui Qurani takatifu na maandiko yake. Picha ya Makafiri hawa aidha, inachorwa wakionekana wapumbavu na wajinga wanapoambiwa na bawabu Jehanamu kuwa walipewa wakati wa kutosha wa kumtii Mungu, kufuata njia zake na kutubu ili wajiepushe na mateso haya. Makafiri hawa vilevile wanaonekana kama watu wasio na matumaini na amani. Makafiri wanaonekana kama watu wanaojutia matendo yao lakini hawana muda wa kutubu kwa vile wakati waliopewa tayari umekwisha. Taswira ya watu wajinga, wapumbavu na waasi inachorwa na mtunzi katika beti hizi.

Katika ubeti wa 285 na wa 307, mtunzi anaonyesha picha ya Siku ya Kiyama kama siku ya maangamizo wanadamu wanapoulizwa katika ubeti wa 285 ni kwa nini walimwasi Mungu. Aidha, ubeti wa 307 unadhihirisha adhabu wanaopata Makafiri Mungu anapouliza malaika wake iwapo kuna watendaji dhambi ambao hawajatiwa motoni.

Katika mfano huu, picha ya Mungu kama asiye na huruma kwa watu wake inasawiriwa haswa atakapouliza kama kuna watu ambao hawajatiwa motoni. Hili linaleta picha na vilevile linathibitisha kuwa hakuna Kafiri hata mmoja ambaye atasamehewa kwa sababu ya kushiriki katika kutenda dhambi duniani.

Mtumi akatamka
Kumuuzua malaika
Moto ulipo kiwaka
Wengine wasaliya? (ubeti 307)

Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* amefaulu pakubwa katika kukuza dhamira na maudhui yake. Msanii wa utenzi huu ameonyesha ujuzi wa hali ya juu katika kuteua na kutumia lugha katika kubuni maswali ya balagha. Aidha, msanii hajatumia lugha yake kiholela. Mbinu hii ya maswali ya balagha imetumiwa katika kujenga picha inayowasilisha Siku ya Kiyama. Kupitia kwa matumizi mazuri ya maswali ya balagha, mshairi amejenga taswira ya kuona, taswira ya joto na taswira ya usikivu ya siku ya maangamizi duniani. Katika siku hii, Makafiri wote watachomeka Jehanamu kwa sababu walikataa kumwabudu Mola huku Waislamu wanaorejelewa kama watakatifu wakisherehekea Peponi pamoja na Mungu kwa sababu walikuwa watiifu duniani.

3.7 Hitimisho

Katika sura hii, tumeshughulikia matumizi ya takriri, tashbihi, tashhisi, sitiari na maswali ya balagha katika *Utenzi wa Qiyama*. Mbinu hizi tano zimetumika pakubwa katika kujenga utenzi huu. Mbinu hizi zimetumiwa na mshairi ili kupitisha ujumbe wake wa kidini. Aidha, mshairi ameweza kuonyesha mtazamo na msimamo wake wa dini ya Kiislamu. Hili limetokana na hali kuwa msanii anapendelea dini ya Kiislamu huku akidunisha dini ya Kikristo. Wakristo katika utenzi huu wamerejelewa kama Makafiri na pahala pao siku ya

mwisho kuonekana kama ni Jehanamu. Waislamu wamerejelewa kama watakatifu watakaokwenda Peponi siku ya mwisho.

Mtunzi vilevile ameonyesha ujuzi mkubwa wa kutumia mbinu za takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha. Mbinu hizi zimechangia katika kujenga taswira za kuona, usikivu, mwendo na joto katika *Utenzi wa Qiyama*. Haya yanadhihirika na uwezo wake wa kutotumia lugha yake kiholela. Lugha ya mtunzi vilevile imeambatana na muktadha wake wa kimatumizi na kumwezesha kuafikia malengo yake. Mbinu hizi tano ambazo mshairi ametumia katika *Utenzi wa Qiyama* ni bia. Aidha, mbinu hizi zinapatikana katika tamaduni zote za ulimwengu hivyo zinaeleweka kwa urahisi kimatini.

SURA YA NNE

4.0 UMUHIMU WA TAKRIRI, TASHBIHI, TASHIHISI, SITIARI NA MASWALI YA BALAGHA KATIKA UJENZI WA TASWIRA INAYOWASILISHA SIKU YA KIYAMA

Katika sura hii tumeshughulikia umuhimu wa tamathali hizi tano katika ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama. Mbinu hizi ni takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha.

4.1 Utangulizi

Mshairi anapotunga shairi lake huwa analenga kufanikisha lengo na majukumu mahususi. Mbinu anazotumia mshairi katika kazi yake vilevile huwa na dhima mahususi kama anavyodai Leech (1969:148) anaposema kuwa mbinu fulani ya kitamathali inaweza kutumiwa na mtunzi kuhamisha maana kutoka kwa kitu kimoja hadi kwa kingine, ikiwa vitu hivyo viwili vina sifa inayofanana. Leech anasema kuwa **L** (kilinganishi) inaweza kuchukuliwa kama **F** (kilinganishwa) ikiwa zina uhusiano. Maana inapohamishwa kwa njia moja au nyingine kutoka kwa kitu kimoja hadi kingine, picha ya kitu hicho pia uhamishwa kutoka kwa “**L**” ambayo ni kilinganishi hadi kwa kilinganishwa “**F**”. Majukumu ya mbinu hizi tano ni kama yafuatayo:

4.2 Umuhimu na Ujenzi wa Taswira

Mshairi anapotunga shairi lake huwa ananua kuafikia jukumu fulani mahususi na vilevile kuleta picha ya anayoyazungumzia kwa kutumia mbinu mbalimbali kwa wasomaji wake. Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* amejenga picha au taswira ya kuona, taswira ya usikivu, taswira ya mwendo na taswira ya joto ya Siku ya Kiyama ambayo imefungamana kwa kiasi kikubwa na matumizi ya mbinu mbalimbali kama vile takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari,

maswali ya balagha na mbinu nyingine ambazo hatujashughulikia katika kazi hii. Mbinu hizi tano ambazo tumezishughulikia zimechochea fikra za msomaji kwa undani, ili msomaji aweze kupata au kuchora picha kamili ya Siku ya Kiyama na vile mambo yatakavyokuwa. Aidha, kupitia kwayo, siku hii ya mwisho imejitokeza kwa uwazi kwa ajili ya kuhamasisha umma kumtii na kufuata njia zake Mwenyezi Mungu. Vilevile, mshairi anawashawishi Makafiri ili wamfuate Mungu na wamsaidie kupigania matendo mema, huku wakijiepusha na maovu.

4.3 Tashbihi na Sitiari

Mshairi wa *Utenzi wa Qiyama* alinua kuwasilisha ujumbe wake kwa kutumia picha, ili ifikie kikundi mahususi. Mtunzi ameweza kutumia mbinu ya tashbihi na sitiari kwa nia ya kujenga taswira ya kidini ambayo haiwezi kutambuliwa kwa njia ya moja kwa moja na wanajamii. Jambo hili limetokana na hali kuwa watu huwa wamezoea kuambiwa kila siku kuwa dunia inakaribia kufika mwisho na wengi hawatilii maanani. Mshairi akaamua kutumia mbinu ya tashbihi na sitiari ili kuleta uhalisia wa siku hii, kwa kutuchorea picha ya kuonekana ya namna ambavyo watenda dhambi watakavyoadhibiwa Jehanamu, huku watenda wema wakisheherekea Peponi.

Mwandishi ameweza kutekeleza jukumu la kufanikisha ujumbe wake kwa kuwa mtu yeyote yule anayeishi katika nchi isiyokuwa na waumini au Makafiri hawezi kuelewa kuwa kuna siku ya mwisho ambapo wanadamu watahukumiwa na Mwenyezi Mungu kulingana na matendo yao ya hapo awali duniani.

Katika *Utenzi wa Qiyama*, mshairi ametumia tashbihi na sitiari ili kujenga mshikamano wa kirejelezi katika kazi yake. Wamitila (2008:483) anadai kuwa kazi ya kifasihi ina jukumu la

kujenga au kuunda taswira fulani ya ulimwengu ambao unaweza kuwa umeundwa kwenye ulimwengu halisi. Wamitila vilevile anasema kuwa ulimwengu huu ndio unadhibiti masimulizi, uteuzi wa lugha na semi ambazo zinahusishwa na wahusika pamoja na uteuzi wa ishara. Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* amefaulu kuteua lugha yake na ishara alizotumia ili kujenga picha inayosawiri hali halisi ya siku ya mwisho katika utenzi huu. Kwa mfano, mshairi ameweza kuwalinganisha Makafiri na ng'ombe ili kudhihirisha ujinga wa wanadamu utakaowaelekeza Jehanamu katika siku hiyo ya mwisho.

Tamathali hizi zimeleta mshikamano wa kimtindo kwa kudondosha maneno na kauli. Kwa mfano, mshairi ameweza kutumia maneno kama vile kusi, ng'ombe, Jehanamu, njia pana na nyani katika utenzi huu, kama tulivyoishughulikia katika sura ya tatu. Mtunzi ametumia maneno machache ili kutuchorea picha ya kuona, taswira za usikivu, taswira za mwendo na taswira za joto ya Siku ya Kiyama kwa kujiepusha na maelezo mengi. Kwa mfano, neno ng'ombe linaweza kuwa na maana ya “mjinga”, “haramu”, “asiyefaa”, “mhalifu”, “mkosa adabu na heshima” na pia neno hili linaweza kutumiwa kumrejelea yule aliyezaliwa kutokana na mapenzi haramu. Neno “Jehanamu” linamaanisha pahali pa mateso na pia penye moto na majoka. Mshairi ana jukumu la kutumia maneno ya mkato kwa kudondosha maelezo. Njogu na Chimera (1999:90) wanaunga kauli hii mkono kwa kusema kuwa lugha ya shairi ni tofauti na lugha ya kawaida kwa vile mtunzi wa shairi huwa anatumia lugha ya mkato. Lugha hii ya mkato inapotumiwa na mshairi, inambidi msomaji wa shairi kutafakari kuhusu kinachosemwa. Aidha, wakati msomaji wa shairi anapotafakari kuhusu kile kinachosemwa, picha ya kitu hicho na ujumbe unaowasilishwa hujengeka akilini mwake.

Aidha, tamathali hizi mbili, yaani tashbihi na sitiari zimetumiwa na mtunzi ili kuleta tasfida. Matumizi ya tamathali hizi yamemwezesha mshairi kuepukana na matumizi ya maneno

yanayoweza kuzua taharuki na hisia mbaya kwa msomaji. Tafida inayoletwa na matumizi ya maneno haya imemwezesha mshairi kuepukana na maneno yanayoweza kuleta utovu wa nidhamu na ukosefu wa maadili kwa kazi yake. Kwa mfano, mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* amewashambulia wafalme na masultani walioonyesha ubabe wao duniani na kumsahau Mungu, huku wakiwatawala wanadamu wenzao kimabavu duniani kwa kutumia neno ng'ombe. Neno hili haliwezi kueleweka kwa urahisi na mtu wa kawaida. Itambidi msomaji kutafakari kwa undani maana ya neno hili ndio aweze kufasiri maana yake.

Mshairi amewalinganisha viongozi na wafalme hawa waliomwasi Mungu na ng'ombe. Neno hili limetumiwa na mshairi ili kudhihirisha ujinga wa viongozi hawa waliokataa kumtii Mungu bila kujua kuwa siku yao pia itawadia na watahukumiwa vilivyo. Vilevile, mshairi anawasihi hawa viongozi wanaomiliki dunia kuwahudumia wanadamu wenzao kwa utu na ukarimu kwa vile siku ya mwisho watu wote watahukumiwa na kuadhibiwa kwa njia sawa bila vyeo vyao vya duniani kujaliwa. Kwa hivyo, mshairi ametumia mbinu hizi mbili ili kutuonyesha umuhimu wa tashbihi na sitiari katika kuchora au kuleta taswira halisi ya kuona ya namna ambavyo viongozi Makafiri watakvyoadhibiwa siku ya mwisho bila huruma iwapo hawatabadili tabia, mienendo na matendo yao kabla ya Siku ya Kiyama.

Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* ametumia mbinu ya tashbihi na sitiari katika kazi yake ili wasomaji waelewa sifa za Mungu na mwono ulimwengu wa mtunzi kuhusu dini. Katika *Utenzi wa Qiyama*, mtunzi anaeleza sifa za Mungu na hatua atakazowachukulia wanadamu siku ya mwisho. Aidha, mtunzi anaeleza msimamo wake kwa dini ya Kiislamu huku akiwarejelea Wakristo kama Makafiri.

Mbinu za sitiari na tashbihi zimetumiwa na mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* ili kuongezea ladha ujumbe kuhusu Siku ya Kiyama. Msanii ametumia vilinganishi vya moto, mimea na wingu,

wakati, nyota, wanyama, hali n.k ili kuelezea Siku ya Kiyama kwa msomaji bila msomaji kuchoka kusoma kazi yake.

Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* ametumia sitiari na tashbihi ili kuleta ucheshi anapoeleza Siku ya Kiyama. Kwa mfano, amewalinganisha Waislamu na taa huku Wakristo wakilinganishwa na ng'ombe kwa sababu ya kutofuata sheria za Mungu. Aidha, mbinu ya tashbihi na sitiari zimeteka hisia za msomaji kwa vile zimetumiwa kwa ufundi wa hali ya juu.

Mtunzi ameeleza mawazo yake kwa kutumia maneno machache. Matumizi ya sitiari na tashbihi katika *Utenzi wa Qiyama* yamemwezesha msanii kufikisha ujumbe wake wa siku ya mwisho kwa wasomaji kwa kutumia maneno machache. Kwa mfano, upepo utakaovuma siku ya mwisho unapolinganishwa na kusi umemwezesha mtunzi kujiepusha na maelezo mengi yanayohusu ukali wa upepo huo.

Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* amewashirikisha wasomaji katika kazi yake kwa kuwapa nafasi ya kutafakari na kufasiri ujumbe wa shairi kulingana na uelewa wao. Matumizi ya tashbihi na sitiari katika utenzi huu yanampatia msomaji nafasi ya kusoma, kutafakiri na kufasiri mbinu hizi katika utenzi huu kulingana na uelewa wake.

Matumizi ya tashbihi na sitiari katika *Utenzi wa Qiyama* yamemwezesha mtunzi kujieleza na kuwasilisha ujumbe kuhusu siku ya mwisho kwa kutumia mbinu ya mbadala. Aidha, matumizi ya mbinu hizi mbili na msanii yameonyesha ubunifu wake. Hii ni kwa sababu mbinu za tashbihi na sitiari zimetumiwa na mtunzi katika utenzi huu kama kivumisha, kitenzi na nomino.

Katika *Utenzi wa Qiyama*, mtunzi ametumia mbinu ya tashbihi ili kufafanua na kueleza hisia zake kuhusu dini ya Kikristo na dini ya Kiislamu. Kwa mfano, mtunzi ameonyesha mapenzi

yake kwa Waislamu anapofafanua vile watakwenda Peponi na kufurahia pamoja na Manani huku akiwadunisha Wakristo kwa kuwarejelea kama Makafiri. Aidha, mateso watakayowapata hawa Makafiri siku ya mwisho Jehanamu yanaelezwa na mtunzi. Matumizi ya mbinu hizi vilevile yameleta burudani kwa msomaji.

4.4 Takriri

Matumizi ya takriri na mtunzi katika *Utenzi wa Qiyama* yamemwezesha msomaji kutambua beti na mishororo yenye ujumbe muhimu katika utenzi huu ambayo msomaji anahitaji kumakinikia wakati anasoma. Kwa mfano, katika ubeti wa nane **ni laki laki lukuki** limerudiwa ili kuonyesha sifa muhimu za Mungu. Mshairi anasema kuwa Mungu ana sifa nyingi zisizoweza kuhesabika ili kuonyesha umuhimu wake katika utenzi huu.

Katika *Utenzi wa Qiyama*, mtunzi wa utenzi ametumia takriri ili kumtwika msomaji wake jukumu la kubainisha maana katika utenzi, ujumbe na vilevile ameweza kuwapatia wasomaji wa utenzi nafasi ya kumakinika wanaposoma maelezo ya msanii kuhusu Siku ya Kiyama.

Matumizi ya takriri na mtunzi katika *Utenzi wa Qiyama* umeleta msisitizo wa ujumbe kuhusu Siku ya Kiyama na maangamio watakayowapata Makafiri Jehanamu kwa msomaji. Aidha, wasomaji wameelezwa vile siku ya mwisho itakavyokuwa siku muhimu sana kwa wanadamu na kwamba hakuna mtu yeyote atakayesamehewa na Mungu.

Matumizi ya takriri katika utenzi huu yamemwelekeza msomaji katika maudhui ya hukumu watakayopata Makafiri siku ya mwisho. Msomaji wa *Utenzi wa Qiyama* ameweza kutambua mkinzano uliopo katika utenzi huu msanii anaposema kuwa Waislamu wote wataweza kufika Peponi kwa vile hata wenye dhambi watatetewa na Mtume. Kwa upande mwingine Wakristo

wote wanachukuliwa kama wenye dhambi na kwa sababu hiyo hakuna hata mmoja atakayehurumiwa na Mungu.

4.5 Tashihisi

Mtunzi wa utenzi huu amefaulu kuumba utenzi wake kwa kutumia mbinu ya tashihisi. Hili ni jukumu kuu ambalo mshairi ameweza kuafikia. Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* ametumia tashihisi ili kupata misamiati iliyounda utenzi wake. Mshairi amechora picha halisi ya Siku ya Kiyama anapowalinganisha watu na ng'ombe, anapodhihirisha ukali wa upepo utakaovuma siku ya mwisho kwa kulinganisha upepo na kusi na anapoipatia moto uwezo wa kuzungumza na kutisha utakapowachoma wanadamu siku ya mwisho ili kuchochea hisia za wasomaji wake, kutujengea picha ya kuonekana ya siku ya mwisho na kuwasilisha maudhui kuu ya utenzi huu. Mbinu hii vilevile imeleta uhondo kwa vile imetumiwa katika kuumba *Utenzi wa Qiyama*.

Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* amefaulu kutumia mbinu ya tashihisi ili msomaji aweze kuchora picha ya Siku ya Kiyama katika akili yake. Aidha, tashihisi imetumiwa na mtunzi kudhihirisha hisia mbalimbali kwa msomaji. Kwa mfano, msanii amedhihirisha hisia ya huzuni kwa Makafiri kwa vile wataangamia na kuteseka bila huruma Jehanamu. Waislamu kwa upande mwingine wamesawiriwa kama wenye ushindi na furaha kwa sababu watakwenda Peponi kuishi bila mateso. Aidha, vitu visivyo na uhai vimepewa sifa ya kibinadamu na mtunzi ili kuonyesha umuhimu wa siku ya mwisho kwa Waislamu.

Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* ameweza kupambanua kazi yake kwa kutumia tashihisi. Maana katika utenzi huu imebainika wazi kwa msomaji kwa sababu ya matumizi ya mbinu

hii na msanii. Mbinu hii vilevile imeleta uthabiti, urembo na mvuto wa ujumbe kuhusu siku ya mwisho inayoelezwa na mtunzi katika utenzi.

Matumizi ya tashihisi na mtunzi yamemwezesha msomaji kukumbuka ujumbe wa Siku ya Kiyama unaoelezwa na mtunzi kama siku ya maangamizo ambapo hata wanyama kama vile farasi wa Mtume watahukumiwa na Mungu.

4.6 Maswali ya Balagha

Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* alikuwa na nia ya kutunga utenzi bora. Umuhimu huu umedhihirika katika matumizi yake ya maswali ya balagha. Aidha, ameleta ubora huu kwa matumizi yake ya maneno yenye ucheshi ili kuibua hisia tofauti kutoka kwa wasomaji wake. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Qiyama*, mshairi amewaulizia walipo masultani wa dunia waliokuwa wakijiona kama miungu, kwa vile masultani hawa walijijengea makasri makubwa na wakajiona kama wenye uwezo zaidi kumliko Mungu. Aidha, masultani hawa walikuwa wakiabudiwa na wanadamu. Mshairi anauliza maswali haya ili kuwadhihaki wafalme wa dunia na vilevile anawaonyesha kuwa kuna Mungu mwenye nguvu zaidi ya mwanadamu yeyote yule. Maelezo haya yameleta ucheshi na vilevile yanaleta hali ya kujiburudisha kwa msomaji.

Aidha, picha ya masultani na viongozi wengine imedhihirika wakitawala dunia bila kujali kuwa siku ya mwisho itafika ambapo watu watahukumiwa. Mshairi vilevile ametujengea picha ya kuona ya siku ya mwisho kwa kutumia maswali ya balagha anaposema kuwa masultani waliotawala dunia hawako tena kwa vile watapelekwa kuhukumiwa kwa njia sawa na watu wa kawaida. Maelezo yanayotolewa kutokana na mbinu hizi mbili yameleta hisia changamano kwa msomaji. Hisia hizi ni pamoja na furaha, huzuni na uchangamfu.

Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* ametumia mbinu ya maswali ya balagha ili kuwashambulia wanajamii na maovu wanayoyatenda duniani. Mshairi anatuelezea adhabu watakaopata waasi wa Mungu katika siku ya mwisho, dunia itakapoisha. Maelezo haya ndiyo yanaleta picha halisi ya vile waasi watakavyoangamia siku ya mwisho Mungu atakapokujia wafuasi wake, huku waasi wakielekezwa Jehanamu penye moto, mateso, majoka na maangamio ya milele. Kwa mfano, katika ubeti wa 29 wanadamu, viongozi na wafalme waliojipiga kifua na kuonekana wenye kiburi hawako tena kwa vile wataangamia siku ya mwisho. Haya yanadhihirishwa na hali kuwa mshairi anauliza katika ubeti huu **walipo majababari, walipo wenye wakitakabari, walipo wenye kiburi** waliodhani kuwa dunia ni yao. Katika ubeti wa 267 hawa watu waliojipiga kifua wanarejelewa kama ng'ombe wenye pembe na wataangamia kwa sababu ya ujinga yao. Mshairi anasisitiza kuwa kwa vile walikuwa wajeuri basi wajitoe motoni na vilevile wajiokoe kutoka kwa mateso ya Jehanamu.

Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* amefaulu kuwashawishi wasomaji huku akichochea fikra zao kwa kutumia maswali ya balagha. Kwa mfano, mshairi anapouliza kuhusu walipo wale viongozi Makafiri waliojipiga kifua na kuwanyanyasa wenzao duniani. Mtunzi amewauliza Makafiri wa duniani mbona hawajasaidiwa na mali yao ili wasiteketee Jehanamu. Aidha, mbinu hii imetumiwa na mtunzi kwa njia inayowachekesha wasomaji wa *Utenzi wa Qiyama* hasa anapowakejeli matajiri wa dunia. Mtunzi vilevile amefaulu kuleta udhahiri wa Siku ya Kiyama, pia wasomaji wa utenzi huu wameweza kutafakarishwa na ujumbe wa msanii kuhusu siku ya mwisho.

Matumizi ya maswali ya balagha na mtunzi yamemsaidia msomaji kutambua beti zilizo na maana. Msomaji ameshirikishwa na mtunzi katika usomaji na utowaji wa majibu ya maswali

anayoyauliza mtunzi. Kupitia kwa maswali haya, msomaji ameweza kutafakari na kubainisha maana ya ujumbe unaowasilishwa na mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama*.

Aidha, mbinu ya maswali ya balagha imemsaidia msomaji kuelewa maana ya mambo yasiyo ya kawaida yanayofafanuliwa na mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama*. Kwa mfano, msomaji ameweza kuelewa vile wanadamu watakvoyofufuliwa na kurejeshwa katika hali yao ya kawaida kabla ya kuhukumiwa na Mungu. Mbinu hii vilevile imetumiwa na mtunzi ili kuonyesha hali ya kuonekana ya Siku ya Kiyama inayosawiriwa na mtunzi katika utenzi huu.

Mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* ametumia swali la balagha ili kuelezea matatizo yatakayowapata Makafiri siku ya mwisho kwa vile hawakufuata kanuni za Mungu. Aidha, mtunzi ameweza kutumia mbinu hii ili kuisitiza adhabu watakayowapata Makafiri Siku ya Kiyama huku Waislamu wakielezwa kama watakatifu na kwa hivyo watakwenda Peponi mara moja parapanda itakapolia siku ya mwisho.

4.7 Hitimisho

Katika sura hii tumefaulu kushughulikia umuhimu wa takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha katika kufanikisha ujenzi wa taswira ya kuona, kusikia, mwendo na joto inayowasilisha Siku ya Kiyama. Mbinu hizi tano kwa ujumla zina umuhimu wa kuleta urembo na udhabiti wa kinachosemwa na mtunzi katika *Utenzi wa Qiyama*. Aidha, mbinu hizi zimetumiwa kutekeleza jukumu la kuleta mshikamano wa kirejelezi, kuficha maneno mabaya yanayoweza kuzua hisia hasi kwa kutumia tasfida na vilevile mbinu hizi zimetokeleza jukumu la kuumba utenzi huu.

Katika sura ya tano tumeshughulikia hitimisho wa utafiti wetu kwa kuzungumzia kwa kifupi tuliyojadili kwa ujumla. Hivyo, katika sura hii tumetathmini malengo yetu ya utafiti,

tumepima maswali yetu ya utafiti na mwisho tumetoa mapendekezo ya vipengele vinavyostahili kuchunguzwa na wasomi wengine watakaokuwa na nia ya kuhakiki *Utenzi wa Qiyama* hapo baadaye.

SURA YA TANO

5.0 Hitimisho na Mapendekezo

5.1 Utangulizi

Katika sehemu hii, tumeshughulikia tuliyoyajadili katika kazi yetu kwa kifupi ili kuthibitisha madai yetu. Tumetathmini malengo ya utafiti wetu. Aidha, tumepima maswali yetu ya utafiti. Mwisho, tumewapendekezea watafiti wa baadaye vile vipengele vinavyostahili kushughulikiwa katika tafiti za baadaye katika *Utenzi wa Qiyama*. Utafiti wetu umechunguza vile takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha zimetumiwa katika kujenga taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika *Utenzi wa Qiyama*.

5.2 Hitimisho

Katika utafiti huu tumeshughulikia matumizi ya takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha katika *Utenzi wa Qiyama*. Katika uhakiki wetu tumejikita katika nadharia ya Umtindo. Tumeshughulikia vipengele vya kimsingi vinavyostahili kuchunguzwa tunapotumia nadharia ya Umtindo. Tumeweza pia kushughulikia yaliyoandikwa na wataalamu mbalimbali kuhusu takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha katika tenzi na kazi mbalimbali kwa ujumla.

Katika sura ya pili, tumeshughulikia ufafanuzi wa dhana ya takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha huku tukijadili kwa ukamilifu kila mbinu na aina zake maalumu. Aidha, tumejadili vile mbinu hizi tano zimetumiwa katika beti mbalimbali ili kujenga taswira ya Siku ya Kiyama kutoka ubeti wa kwanza hadi wa mwisho katika sura ya tatu. Vilevile tumeangazia umuhimu wa takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha katika ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika sura ya nne.

Tumeshughulikia vile takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha zimetumiwa katika *Utenzi wa Qiyama* kutoka katika ubeti wa kwanza hadi wa mwisho huku tukichanganua data yetu kwa kutumia maelezo na ufafanuzi. Utafiti wetu umedhihirisha kuwa mbinu hizi tano zinamchango mkubwa katika kujenga taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama. Mshairi wa *Utenzi wa Qiyama* ametumia takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha kwa kiwango cha juu kwa kutumia maneno ya kawaida katika jamii ili kueleza na kuchora picha halisi ya vile siku ya mwisho itakavyoonekana katika jamii.

5.3 Malengo ya Utafiti

Katika utafiti huu tuliniua kuafikia madhumuni mawili. Kwanza, kuchanganua takriri, tashbihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha katika *Utenzi wa Qiyama*. Tumeweza kuchanganua mbinu hizi tano katika utenzi wote kutoka ubeti wa kwanza hadi ubeti wa mwisho. Aidha, tumeweza kueleza na kufafanua mbinu za takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha huku tukionyesha vile zimejitokeza katika utenzi wote. Tumegundua kuwa takriri, tashbihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha zimetumiwa kwa wingi sana katika utenzi huu. Aidha, tumegundua kuwa kama mtunzi wa *Utenzi wa Qiyama* hangetumia mbinu hizi vizuri huenda utenzi huu haungeweza kukamilika na kuwa miongoni mwa tenzi ndefu na maarufu za zamani.

Hivyo, matumizi ya mbinu hizi tano yamechangia kwa kiwango kikubwa ujenzi wa taswira ya Siku ya Kiyama. Mbinu hizi zimeteka hisia za wasomaji na kuwapatia picha halisi ya kuona, picha ya kusikia, taswira ya mwendo na taswira ya joto ya Siku ya Kiyama. Matumizi ya takriri za aina mbalimbali kutoka mwanzo hadi mwisho wa utenzi umechangia katika matumizi ya maneno machache yanayodhibiti kile kinachosemwa kwa kuleta picha halisi ya vile siku ya mwisho itakavyoonekana.

Katika sura ya tatu na ya nne tumeweza kutathmini jinsi takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha zimechangia ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika *Utenzi wa Qiyama*. Tumeweza kuonyesha umuhimu wa tamathali hizi na mchango wake katika ujenzi wa taswira katika sura ya nne. Umuhimu wa mbinu hizi ni kama vile; Kuleta mshikamano wa kirejelezi, kuficha maneno mabaya yanayoweza kuzua hisia hasi kwa kutumia tasfida na vilevile mbinu hizi zimetumiwa na mtunzi kutekeleza jukumu la kuumba utenzi huu. Ni bayana kuwa lugha itumiwayo na mtunzi hasa mbinu mbalimbali anazotumia ndiyo nguzo muhimu katika ujenzi wa picha wa kile anachokirejelea mtunzi. Mshairi ameweza kutumia tamathali mbalimbali ili kulinganisha vitu mbalimbali vinavyopatikana katika jamii kwa lengo la kuchora picha ya hali ya vile siku ya hukumu itakavyokuwa na kuonwa na wanadamu.

5.4 Mapendekezo

Tumeshughulikia matumizi ya takriri, tashibihi, tashihisi, sitiari na maswali ya balagha katika ujenzi wa taswira inayowasilisha Siku ya Kiyama katika *Utenzi wa Qiyama*. Tunawapendekezea wahakiki wengine walio na nia ya kuchunguza *Utenzi wa Qiyama* kuchunguza vipengele vingine vya tamathali za usemi ambazo hatujashughulikia ili kufanikisha uelewa zaidi wa utenzi huu hasa katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu lugha ya utenzi huu na tenzi nyinginezo za Kiswahili za zamani ni chakavu, hivyo hazieleweki na wengi.

Aidha, kuna mchanganyiko wa maneno ya Kiarabu na lahaja ya Kiamu. Hili huenda likafanya ujumbe wa tenzi kutoeleweka kwa urahisi na kufanya wasomaji wengi kuepuka utenzi huu. Uhakiki wa takriri, tashibihi, sitiari, tashihisi na maswali ya balagha

umerahisisha uelewekaji wake. Kwa mujibu wa Wamutiso (1996:7) wataalamu wameziepuka tenzi hizi kwa sababu ya matumizi ya kilahaja na maneno ya Kiarabu.

Tunawapendekezea watafiti wengine kuchunguza dhamira na maudhui ya utenzi huu huku wakiilinganisha na tenzi nyinginezo za Kiswahili. Vilevile tunawashauri wahakiki wenye nia ya kushughulikia utenzi huu kuchunguza masimulizi katika utenzi huu kwa vile masimulizi yake yametolewa kwa wakati uliopita huku matukio ya hukumu yakitarajiwa kufanyika siku za usoni.

Marejeleo

- Abdulaziz, M. H. (1979). *Muyaka 19th Century, Swahili Popular Poetry*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Abedi, K. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Dar es Salaam: Eagle Press.
- Abraham, M. (1971). *Natural Supernaturalism: Tradition and Revolution in Romantic Literature*. New York: W.W.Norton & Company.
- _____ (1981). *Glossary of Literary Terms 7th ed*. New York: Holt Reinhert Winston Inc.
- Allen, J. W. T. (1971). *Tendi. Six Examples of Swahili Classical Verse Forms with Translation and Notes*. London: Heimann.
- Arege, T. (2012). *Narration in Swahili Narrative Poetry. An Analysis of Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Shahada ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa bado).
- Buffon, G. (1930). *Buffon's Discourse on Style*. Paris Librairie: Hatier Publishers.
- Chapman, A. (1974). *Jewish – American Literature: An Anthology*. West Bengal: Signet Press.
- Crystal, D. & Davy, D. (1969). *Investigating English Style*. London: Longman Group.
- Elliot, T. S. (1953). *Selected Prose*. London: Pennguin Books.
- Faqihi, B. (1979). *Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Dar es Salaam: Tanzania publishing House Ltd.
- Fodor, J. A. & Katz, J. J. (1964). *Semi- Sentences in The Structure of Languange*. Colorado: Englewood Cliffs
- Fowler, R. (1973). *A Dictionary of Literary Terms*. New York: Routledge & Kagan Paul Ltd.
- Frye, N. & Perkins, G. (1985). *The Harper Handbook to Literature*. New York: Harper & Row.
- Holman, C. (1936). *A Handbook to Literature*. New York: Macmillan.

- _____ (1960). *A Handbook to Literature*. New York: Odyssey Press Inc.
- Holman, C. & Harmon, W. (1986). *A Handbook to Literature*. New York: Macmillan.
- Kazungu, K. (1982). "Deviation of Foregrounding in Chosen Swahili Literary Text".
Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa bado).
- Knappert, J. (1967). *Traditional Swahili poetry: An Investigation into the Concept of East African Islam as Reflected in the Utenzi Literature*. Leiden: E. J. Brill.
- _____ (1971). *Swahili Islamic Poetry*. Leiden: E. J. Brill.
- _____ (1979). *Four Centuries of Swahili Verse*. London: Heinemann Ltd.
- Kofa, T. (2009). *Uhakiki wa Fani Katika Utenzi ya Swifa ya Nguvu Mali*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa bado).
- Kuhenga, C. (1977). *Tamathali za Usemi*. Dar es Salaam: East Africa Literature Bureau.
- Leech, G. M. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group.
- Leech, G. M na Short, M. (1981). *Styles in Fiction: An Introduction to the English Fictional Prose*. London: Longman.
- Lugwiri, P. L. (2011). *Sitiari, Taashira na Tashbiha katika Utenzi wa Tambuka*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa bado).
- Maundu, J. (2013). *Matumizi ya Takriri na Sitiari Katika Utenzi wa Rasi'lGhuli*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa bado).
- Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi. Graphics and Publishers.
- Msokile, M. (1993). *Msingi ya Uhakiki wa Kifasihi*. Dar es Salaam: East African Education Publishers.
- Mulokozi, M. M. (1999). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mulokozi, M. M. na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.

- Myers, J. Na Simms, M. (1989). *The Longman Dictionary of Poetic Terms*. London: Longman.
- Nowotny, W. (1962). *Language Poet Use*. New York: Oxford University Press.
- Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Olali, T. (2004). *The Veneration of the Prophet: The Role of Kasida Hamziyya. During the Maulidi Festival of the Lamu Archipelago*. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha London. (Haijachapishwa bado).
- Quirk, R. Et al. (1985). *A Comprehensive Grammar of the English Language*. London: Longman.
- Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.
- Simpson, P. (2004). *Stylistics. A Resource Book for Student*. London: Routledge.
- Steem. (1970). *Islam in Ethiopia*. London: L. Fracass.
- Timmamy, R. (2002). "Mombasa Swahili Women Wedding Song. A Stylistic Analysis". Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa bado).
- Toolan, M. (2004). *Language in Literature: An Introduction to Stylistics*. London : Arnold.
- TUKI. (1981). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford.
- Ullman, S. (1971). "Two Approaches to Style." Katika Streka, J. (1971). *Patterns of Literary Styles. Toleo la tatu*. Uk. (218). London: The Pennyslavia State University Press.
- Wales, K. (2001). *A Dictionary of Stylistics. Toleo la pili*. Harlow: Pearson Education.
- Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Msingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers
- _____ (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus publishers.
- _____ (2006). *Msimu wa Vipepeo*. Nairobi: Vide- Muwa publishers Ltd.

- _____ (2008). *Kanzi ya Fasihi I: Msingi wa Uchanganuzi wa Kiswahili wa Fasihi*.
Nairobi: Vide- Muwa publishers Ltd.
- Wamutiso, K. (1996). "Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry: Kasida ya Burudai"
Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu, Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa bado).
- _____ (2003). *Analysis of Swahili Islamic poetry. Five Swahili Epic on Swahili Women*.
Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa bado).
- _____ (2005). *Utenzi wa Hamziyya*. Dar es Salaam: TUKI.
- Wanjiru, M. (2014). *Matumizi ya Istiari, Tashbiha na Taashira katika Diwani ya Sauti ya Dhiki*.
Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa bado).